

**NAFASI YA HADITHI SIMULIZI KATIKA KUFUNZA MAADILI MEMA  
SHULE ZA SEKONDARI, VISIWANI ZANZIBAR**

**HAJI MAULID OMAR**

**IMEWASILISHWA IKIWA SHARTI PEKEE LA KUHITIMU SHAHADA  
YA UZAMIVU (Ph.D) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2013**

**UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI**

Mimi Profesa, Dkt.Sheikh, T. S. Y. M. Sengo, nathibitisha kwamba nimeisoma tasnifu hii, iitwayo “**Nafasi ya hadithi Simulizi katika kufunza Maadili mema shule za sekondari, Visiwani Zanzibar.**” na nimeridhika kwamba imefika kiwango kinachofaa kuhudhurishwa kwa utahini wa Digirii ya Uzamivu (Ph.D) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

.....  
Profesa, Dkt. Sheikh. T. S. Y. M. Sengo  
(Msimamizi)

Tarehe.....

**HAKIMILIKI**

Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote iwayo, kuhailishwa kwa mbinu yoyote ile ya kieloktroniki kunakilishwa kurudufiwa katika hali yoyote bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba yake.

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Haji Maulid Omar**, natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii iitwayo *“Nafasi ya Hadithi Simulizi katika Kufunza Maadili mema shule za sekondari, Visiwani Zanzibar”* ni kazi yangu mimi mweyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa popote kwa lengo la kufuzu shahada yoyote.

.....  
Haji Maulid Omar

Tarehe.....

**TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi, familia na walimu wangu walionisomesha tokea  
Msingi hadi Ndakini na majirani zangu wa Kinuni-Zanzibar.

## SHUKRANI

Utafiti huu umekamilika kutokana na Mwongozo wa **Mwenyezi Mungu**, pamoja na misaada ya watu wengi, kama itakavyodhihirika baada ya kuusoma. Sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa wale waliochangia kukamilisha utafiti huu. Wa kwanza ni msimamizi wangu, Profesa, Dkt, Sheikh TIGITI. S. Y. M. SENGO, wengine ni Profesa J. Mhoma, Profesa E. Mbogo, Profesa J. Mwiliza, Dkt Anna Kishe na Dkt J. Yambi wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Profesa Idrisa Rai, Dkt Issa Ziddy, bibi Amina Ahmed Abdurahman wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA), na Husam Abdalla Saidi wa (SUZA), Dkt Athumani S. Samzungi Mkurugenzi wa Maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dkt Mwaimu, P. A Mkurugeni wa Kitengo cha Afrika Mashariki, ( EAF ) Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Dar es Saalam na Mwalimu Hafidh Said Nassor, Mkurugenzi wa Maktaba wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA). Mwalim Kasim Suleiman Dadi, Makame Ali Makame, Hassan Gora, Hassan Hija, Vuai Ussi na Bi Asha Muhene Rashid na Ali Mwalimu Rashid na bwana Juma Simai (Mnungwi) wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar, kwa misaada yao mbalimbali katika kufanya kazi hii. Natoa shukurani kwa watendaji wa ofisi ya Makamo wa pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi-Unguja, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba.

Shukurani ziwafikie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuanzia Mkurugenzi Idara ya Elimu ya Sekondari, Mkurugenzi Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. (SUZA), Walimu na wanafunzi wa Shule za Sekondari za Benbella, Bububu, Haileselassie na Tumbatu Unguja. Shukurani pia ziwafikie, walimu na wanafunzi

wa Shule za Sekondari Michenzani (chokocho), Utaani, Kizimbani na Miti Ulaya -Pemba. Shukurani pia ziwafikie Uongozi wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kunikubalia kuwa miongini mwa wanafunzi wake. Mkuu wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii na wenziwe, pamoja na Mkurugenzi wa utafiti, Ushauri na Masomo ya Uzamili na Uzamivu, kwa msaada wao ambao ulikuwa ni muhimili kwangu wakati wote wa masomo yangu.

Shukurani za dhati kwa mama yangu mzazi, Bi Riziki Sharif Hamad wa Utaani Wete Pemba, mke wangu Bi Zainab Khamis Faki, na watoto wetu Omar, Hajra Raiyan na Arafa. Pamoja na haya yote, msaada wa Bi Zuhra S. Said wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA), Omar H. Kombo na Bi Habiba Badru wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kuicharaza kazi hii una nafasi ya kipekee. Natoa tena shukurani na kukiri utukufu, Kwake Yeye Anayestahiki, Mwenyezi Mungu, kwa kutupa uwezo wa kukamilisha kazi hii.

## IKISIRI

Hadithi Simulizi zimeanza zamani kutumika katika jamii. Hadithi zilikuwa na zinaendelea kutumika katika jamii ya watu wa Visiwa vya Zanzibar katika fani mbalimbali za kimaisha. Wazee majumbani na walimu katika Shule za Sekondari hutumia hadithi simulizi katika kufunza maadili mema. Mtafiti amefanya utafiti katika maeneo mbalimbali na kuona nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Shule za Sekondari, Visiwani Zanzibar. Utafiti umefanyika katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Data zimekusanywa maktabani, katika Shule za Sekondari na Mitaani, kwa wazee, walimu, na wanafunzi. Data kuu alizokusanya mtafiti ni hadithi za ngano, vigano na sog. Sura ya kwanza, inazungumzia usuli wa mada na kugusia nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Shule za Sekondari Visiwani Zanzibar, lengo la utafiti, madhumuni mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, eneo na mipaka ya utafiti. Sura ya pili, imebainisha maelezo mafupi ya kazi tangulizi na jinsi zilivyomsadia. Sura ya tatu, utafiti umekusanya nadharia mbalimbali kama vile ndani-nnje, mkabala wa kiislamu, ya fasihi na jamii, ya muundo na ya hisia zinazohusu fasihi simulizi na maadili. Sura ya nne, imefafanua mbinu na njia za utafiti ambazo zimeelezwa ndani ya tasnifu, kuonesha pahala pa utafiti, uteuzi, ukusanyaji wa data, vifaa vya utafiti na uchambuzi wa data. Sura ya tano, imeshughulikia uchambuzi wa data na matokeo ya utafiti. Kwa ujumla mtafiti ametumia nadharia ya Ndani-Nnje, Dhima na kazi ya fasihi, ya Kiislamu, ya muundo, na ya hisia. Sura ya sita ni uhitimisho na mapendekezo, mtafiti ametoa hitimisho na muhtasari wa mapendekezo ya kazi yake ya utafiti.



## YALIYOMO

|   |             |
|---|-------------|
| <b>UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI.....</b>                    | <b>ii</b>   |
| <b>HAKIMILIKI.....</b>                                  | <b>iii</b>  |
| <b>TAMKO LA MTAHINIWA .....</b>                         | <b>iv</b>   |
| <b>TABARUKU.....</b>                                    | <b>v</b>    |
| <b>SHUKRANI .....</b>                                   | <b>vi</b>   |
| <b>IKISIRI .....</b>                                    | <b>viii</b> |
| <b>SURA YA KWANZA.....</b>                              | <b>1</b>    |
| <b>1.0 UTANGULIZI KWA JUMLA .....</b>                   | <b>1</b>    |
| 1.1 Utangulizi .....                                    | 1           |
| 1.2 Mada ya Utafiti .....                               | 3           |
| 1.3 Tatizo.....   | 3           |
| 1.3.1 Usuli wa Tatizo .....                             | 4           |
| 1.3.1.1 Uchumaji wa Karafuu .....                       | 5           |
| 1.3.1.2 Matumizi ya Pataniga (video) .....              | 5           |
| 1.3.1.3 Matumizi ya Wavu Pepe .....                     | 5           |
| 1.3.1.4 Uvunjikaji wa Ndoa .....                        | 6           |
| 1.3.1.5 Shule Zilizo Karibu na Fukwe za Bahari .....    | 7           |
| 1.3.1.6 Matumizi Mabaya ya Madawa.....                  | 7           |
| 1.3.1.7 Wazazi Hawahimizi Watoto wao Kwenda Shule ..... | 8           |
| 1.3.1.8 Wanafunzi Wanaopata Ujauzito .....              | 9           |
| 1.4 Lengo la Utafiti .....                              | 9           |
| 1.5 Madhumuni Maalumu ya Utafiti.....                   | 9           |

|   |           |
|---|-----------|
| 1.6 Maswali ya Utafiti.....                             | 10        |
| 1.7 Umuhimu wa Utafiti.....                             | 10        |
| 1.8 Eneo la Utafiti .....                               | 11        |
| 1.9 Mipaka ya Utafiti .....                             | 11        |
| 1.10 Matatizo.....                                      | 12        |
| <b>SURA YA PILI.....</b>                                | <b>13</b> |
| <b>2.0 KAZI TANGULIZI.....</b>                          | <b>13</b> |
| 2.1 Utangulizi.....                                     | 13        |
| <b>SURA YA TATU .....</b>                               | <b>28</b> |
| <b>3.0 MIKABALA YA NADHARIA .....</b>                   | <b>28</b> |
| 3.1 Utangulizi.....                                     | 28        |
| 3.2 Nadharia ya Ndani-Nnje .....                        | 28        |
| 3.3 Nadharia ya Mkabala wa Kiislamu .....               | 29        |
| 3.4 Nadharia ya Saikolojia ya Tiba .....                | 30        |
| 3.5 Nadharia ya Umithilishaji Fasihi (kama sanaa) ..... | 30        |
| 3.6 Nadharia ya Ushunuzi-Chambuzi .....                 | 31        |
| 3.7 Nadharia ya Ubadilikaji .....                       | 31        |
| 3.8 Nadharia ya Utamaduni.....                          | 32        |
| 3.9 Nadharia ya Kijamii .....                           | 32        |
| 3.10 Nadharia ya Fasihi na Jamii .....                  | 33        |
| 3.11 Nadharia ya Kimaendeleo (Kimapinduzi) .....        | 34        |
| 3.12 Nadharia ya Msambao.....                           | 34        |
| 3.13 Nadharia ya Uaminifu .....                         | 35        |
| 3.14 Nadharia ya Uhalisia .....                         | 35        |

|  |           |
|--|-----------|
| 3.15 Nadharia ya Hisia.....                      | 36        |
| 3.16 Nadharia ya Maneno .....                    | 36        |
| 3.17 Nadharia ya Ubunifu .....                   | 37        |
| 3.18 Nadharia ya Muundo.....                     | 38        |
| 3.19 Nadharia ya Tajriba ya Maisha .....         | 38        |
| <b>SURA YA NNE.....</b>                          | <b>40</b> |
| <b>4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI.....</b>         | <b>40</b> |
| 4.1 Utangulizi.....                              | 40        |
| 4.2 Mbinu ya Maktabani .....                     | 40        |
| 4.3 Mbinu ya Kushiriki Darasani .....            | 40        |
| 4.4 Mbinu ya Mahojiano .....                     | 41        |
| 4.5 Mbinu ya Kutumia Maswali ya Ana kwa Ana..... | 42        |
| 4.6 Mbinu ya Kuwa na Mtafiti Msaidizi .....      | 42        |
| 4.7 Pahala pa Utafiti .....                      | 43        |
| 4.8 Uteuzi wa Watafitiwa.....                    | 43        |
| 4.9 Ukusanyaji wa Data .....                     | 45        |
| 4.10 Vifaa vya Utafiti.....                      | 45        |
| 4.11 Uchambuzi wa Data .....                     | 45        |
| <b>SURA YA TANO .....</b>                        | <b>46</b> |
| <b>5.0 UCHAMBUZI WA DATA .....</b>               | <b>46</b> |
| 5.1 Utangulizi.....                              | 46        |
| 5.2 Dhanna ya Hadithi Simulizi .....             | 47        |
| 5.3 Sifa za Hadithi Simulizi .....               | 48        |
| 5.4 Dhana ya Maadili Mema.....                   | 48        |

|   |    |
|---|----|
| 5.5 Mgawanyo wa Hadithi Simulizi za Vigano. Katika Kufunza Maadili mema ... | 50 |
| 5.5.1 Hadithi ya Mtu na Mwanawe .....                                       | 51 |
| 5.5.2 Hadithi ya Mize, Mboja na Wazazi.....                                 | 52 |
| 5.5.3 Hadithi ya Furaha.....  | 53 |
| 5.5.4 Bi kizee na Mjuku Wake.....   | 54 |
| 5.5.5 Hadithi ya Fisi Adhibiwa .....  | 55 |
| 5.5.6 Hadithi ya Tajiri na Masikini .....                                   | 56 |
| 5.5.7 Hadithi ya Watoto wa Tajiri na Masikini.....                          | 57 |
| 5.5.8 Hadithi ya Fisi, Chui na Sungura .....                                | 59 |
| 5.2.9 Hadithi ya Sikudhani na Majaliwa.....                                 | 60 |
| 5.2.10 Hadithi ya Asma Abeba Ujauzito wa Hassan .....                       | 61 |
| 5.2.11 Hadithi ya Mwanampate na Nyangoro .....                              | 62 |
| 5.2.12 Hadithi ya Kurwa na Doto .....                                       | 63 |
| 5.2.13 Hadithi ya Adili na Amali .....                                      | 64 |
| 5.2.14 Hadithi ya Mtoto Aliyetumwa kwa Mfalme .....                         | 64 |
| 5.2.15 Hadithi ya Viungo Vilivyokataa Kufanya Kazi .....                    | 66 |
| 5.2.16 Hadithi ya Nyuki Aliyekimbia Wenzake .....                           | 67 |
| 5.2.17 Hadithi ya Simba, Chui na Kiwaviwavi.....                            | 68 |
| 5.3.18 Mtoto mzuri Kushinda Wenzake .....                                   | 69 |
| 5.3.19 Hadithi ya Uvumilivu wa Bi Asha .....                                | 70 |
| 5.3.20 Hadithi ya Sungura na Chura .....                                    | 71 |
| 5.3.21 Hadithi ya Bwana Massoud na Wake Zake Wawili.....                    | 72 |
| 5.4.22 Hadithi ya Bwana Ali Kapewa Cheo .....                               | 74 |
| 5.4.23 Hadithi ya Kiongozi Aliyefungua Kisima.....                          | 75 |

|  |    |
|--|----|
| 5.4.24 Hadithi ya Bunuasi na Mfalme .....            | 75 |
| 5.4.25 Hadithi ya Majaliwa.....                      | 76 |
| 5.4.26 Hadithi ya Majuha Wanne Wasiojuana.....       | 76 |
| 5.4.27 Hadithi ya Dereva wa Gari.....                | 78 |
| 5.4.28 Hadithi ya Sungura na Fisi.....               | 78 |
| 5.4.29 Hadithi ya Mla Matonge .....                  | 79 |
| 5.4.30 Hadithi ya Mtepe Uliosheheni .....            | 79 |
| 5.5.31 Hadithi ya Sungura na Membe.....              | 81 |
| 5.5.32 Hadithi ya Jongoo na Nyoka .....              | 81 |
| 5.5.33 Hadithi ya Marafiki Watatu .....              | 82 |
| 5.5.34 Hadithi ya Marafiki Wanne.....                | 82 |
| 5.5.35 Hadithi ya Kipofu Aliyeombewa Dua .....       | 82 |
| 5.5.36 Hadithi ya Kichwa Kidogo Aliomba Dua.....     | 83 |
| 5.5.37 Hadithi ya Bibi Aliyekuwa Hajazaa.....        | 83 |
| 5.6.38 Hadithi ya Binti wa Shamba Kaingia Mjini..... | 84 |
| 5.6.39 Hadithi ya Tupa, Shida na Asha.....           | 85 |
| 5.6.40 Hadithi ya Sultani na Suria .....             | 85 |
| 5.6.41 Hadithi ya Mtu na Mkewe.....                  | 86 |
| 5.6.42 Hadithi ya Jogoo na Mkewe.....                | 86 |
| 5.6.43 Hadithi ya Bwana Aliyepewa Mkoba Sokoni.....  | 87 |
| 5.6.44 Hadithi ya Bibi Mjamzito .....                | 88 |
| 5.6.45 Hadithi ya Mzee Mpacho na Wajukuu Wake .....  | 89 |
| 5.6.46 Hadithi ya Kijana Aliyejifanya Msomi.....     | 89 |
| 5.6.47 Hadithi ya Babu na Jiwe .....                 | 90 |

|   |            |
|---|------------|
| 5.6.48 Hadithi ya Kijana Anaomba Starehe kwa Ndugu yake Bila ya Kujua ..... | 90         |
| 5.7.49 Hadithi ya Mfalme na Maradhi .....                                   | 91         |
| 5.7.50 Hadithi ya Sungura na Fisi .....                                     | 93         |
| 5.7.51 Hadithi ya Mama na Mtoto wa Kambu .....                              | 93         |
| 5.7.52 Hadithi ya Mtoto Aliyeomba Radhi kwa Mama yake .....                 | 95         |
| 5.8.53 Hadithi ya Makame wa Makame Atafuta Mtoto .....                      | 96         |
| 5.8.54 Hadithi ya Makumbi Yageuka Fedha .....                               | 98         |
| 5.9.55 Hadithi ya Sungura, Tembo na Kobe .....                              | 99         |
| 5.9.56 Hadithi ya Simba Mzee na Sungura .....                               | 100        |
| 5.9.57 Hadithi ya Mwanamke Aliyeolewa na Zimwi .....                        | 101        |
| 5.9.58 Hadithi ya Simba na Sungura .....                                    | 102        |
| 5.9.59 Hadithi ya Wazee Wakulima .....                                      | 103        |
| 5.9.60 Hadithi ya Nguruwe na Komba .....                                    | 104        |
| 5.9.61 Hadithi ya Simba na Mkewe na Sungura na Mkewe .....                  | 105        |
| 5.10 Maoni ya Wanafunzi .....   | 107        |
| 5.11 Maoni ya Walimu .....  | 109        |
| 5.12 Maoni ya Wazee .....   | 111        |
| 5.13 Uchambuzi wa Vianzio vya Hadithi Simulizi .....                        | 113        |
| <b>SURA YA SITA .....</b>   | <b>116</b> |
| <b>6.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>                                   | <b>116</b> |
| 6.1 Hitimisho .....   | 116        |
| 6.2 Madhumuni ya Utafiti .....  | 116        |
| 6.2.1 Madhumuni ya Kwanza ya Utafiti .....                                  | 116        |
| 6.2.2 Madhumuni ya Pili ya Utafiti .....                                    | 117        |

|       |  |            |
|-------|--|------------|
| 6.2.3 | Madhumuni ya Tatu ya Utafiti .....                           | 117        |
| 6.2.4 | Madhumuni ya Nne ya Utafiti .....                            | 118        |
| 6.3   | Lengo Kuu la Utafiti .....                                   | 119        |
| 6.4   | Nadharia Mbalimbali Zimetumika Kufanikisha Utafiti Huu ..... | 119        |
| 6.5   | Mapendekezo ya Utafiti .....                                 | 120        |
|       | <b>MAREJELEO .....</b>                                       | <b>122</b> |
|       | <b>VIAMBATANISHI .....</b>                                   | <b>131</b> |

## MAJEDWALI

|  |    |
|--|----|
| Jedwali Na. 5.1: Hadithi zenye kufunza maadili ya makuzi ya mtoto, wema na.....    | 51 |
| Jedwali Na. 5.2: Hadithi zenye kufunza maadili ya elimu, umoja na ushirikiano..... | 60 |
| Jedwali Na. 5.3: Hadithi zenye kufunza maadili ya ndoa na starehe.....             | 69 |
| Jedwali Na. 5.4: Hadithi zenye kufunza Maadili ya uongozi na biashara .....        | 74 |
| Jedwali Na. 5.5: Hadithi zenye kufunza maadili ya urafiki, dini na imani .....     | 80 |
| Jedwali Na. 5.6: Hadithi zenye kufunza maadili ya Mapenzi na tabia njema .....     | 84 |
| Jedwali Na. 5.7: Hadithi zenye kufunza maadili ya Sheria na malezi .....           | 91 |
| Jedwali Na. 5.8: Hadithi zenye kufunza maadili ya itikadi za kijamii.....          | 96 |
| Jedwali Na. 5.9: Hadithi zenye kufunza maadili ya usaliti, wivu na choyo .....     | 98 |



## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI KWA JUMLA**

#### **1.1 Utangulizi**

Katika kipengele hiki kimezungumzia asili ya neno “Zanzibar” kwa maana ya Unguja na Pemba kihistoria na kijografia, mada ya utafiti, tatizo la utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia imeelezea umuhimu wa utafiti, eneo la utafiti, mipaka ya utafiti na matatizo yaliyojitokeza.

Kuna nadharia inayozungumzia asili ya neno “Zanzibar”. Hii inatokana na neno “zinjiba” ambalo ni la lugha ya kifarsi, lenye maana ya ardhi nzuri ya watu weusi. Kabla ya kuja kwa wageni katika Afrika ya Mashariki, Zanzibar ilijumuisha mwambao wote wa Afrika ya Mashariki na Visiwa vyake kutokea Somali hadi Msumbiji na baadae, kwa sababu za kibiashara, Zanzibar ikawa na maana ya Visiwa viwili vikuu, Unguja na Pemba.

Zanzibar ina historia ndefu ya kijografia, kisiasa, kiuchumi, kielimu na kiutamaduni. Neno ”Unguja” lina asili ya Kiswahili na linatokana na neno”ungu-jaa” kwa maana Kisiwa kilicho kikubwa au eneo lenye watu wengi (masimulizi ya wazee wakaazi wa Unguja Ukuu: 2007). Wazee wengine wanasimulia kuwa neno “Unguja” linatokana na neno “Ungo-jaa” kwa maana kuwa vyakula tele. Au ibada nyingi au wema na ukarimu. Pia neno “ungujaa” lina maana kuwa nchi yenye neema, au mavuno mengi, au uchumi mzuri (kazi tangulizi TAKILUKI, 2007 na 2009). Kutokana na hali hii neno “Ungujaa” linaweza likakubalika kutokana na maana yake halisi.

Masimulizi ya wazee wa zamani wa Unguja wa kizanzibari wanasema kuwa Unguja ina asilimia kubwa ya Waisilamu. Tafsiri hizo zinaelezea kuwa “Unguja” ina

asilimia kubwa ya Waislamu. Hivyo neno “Unguja”, lina maana ya “Ungu tele” ibada, ukarimu, imani iliyojaa na ucha Mungu uliowajaa watu wa Visiwa hivi, na kuonesha jinsi imani ya Uungu ilivyoenea katika Visiwa hivi (Sengo 1985).

Kwa upande wa jina la kisiwa cha Pemba, inasemekana kuwa linatokana na neno la Kiswahili “kupemba”. Kwa maana ya “kuongoza chombo kwa uwangalifu” Tafsiri hii inatokana na hali ya kisiwa cha Pemba kuzungukwa na mkondo mkubwa na wenye hatari. Pemba pia ikiitwa “Al-jaziratul hadhara” kwa maana ya “kisiwa cha Kijani” kutokana na rutuba ya ardhi yake, kukifanya kisiwa kuwa ni bustani nzuri ((krain, 1998).

Wapo baadhi ya wataalamu wanaosema kwamba, Msumbiji kuna Pemba, hivyo Wapemba waliletwa kwa wingi kisiwani Pemba. Na hao hasa ndio walioleta jina hilo na herufi ya “n” katika lahaja ya Kisiwa cha Pemba badala ya “m” kama iliyoko katika lahaja za Kisiwa cha Unguja. Kwa mfano neno “nchuzi” badala ya “mchuzi” Mapisi ya wajaji kutoka Nyasaland, Tunduru na Kusini kwingi yamo katika familia nyingi kisiwani humo.

Kijografia; katika mwelekeo wa Kaskazini na Kusini mwa “dunia”, visiwa hivi vipo upande wa Kusini mwa mstari wa Ikweta-kutoka nyuzi  $4^0 50^0$  mpaka  $6^0 30$  Kusini. Na mwelekeo wa Magharibi na Mashariki, Visiwa vya Zanzibar vinapakana baina ya Km 30-50 nje ya ufukwe wa Tanganyika katika Mwambao wa Afrika ya Mashariki. Kisiwa cha Unguja kina eneo la ukubwa wa Km 1,464 za mraba na Pemba kina km 863 za mraba. Kwa jumla, Unguja na Pemba ina ardhi yenye eneo la Km 2,332 za

mraba (Krain: 1998). Kisiwa cha Pemba kilizushwa juu ya maji na nguvu za Volcano.Mabonde na milima na mboji nyingi za mikarafuu. Kabla ya karne nyingi zilizopita, hakikuwepo.

## **1.2 Mada ya Utafiti**

Nafasi ya Hadithi Simulizi katika kufunza Maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar.

## **1.3 Tatizo**

Tatizo ni kushuka kwa maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Tatizo ambalo limechangiwa na mambo mengi katika jamii ikiwemo kukosekana kwa mafunzo ya maadili mema yanayotokana na fasihi simulizi zinazofundishwa katika shule za Sekondari. Tatizo hili bado halijafanyiwa utafiti katika kiwango cha uzamivu. Watalamu waliofanya utafiti wa fasihi simulizi katika kiwango cha uzamivu Visiwani Zanzibar kwanza, Sengo (1985), tasnifu yake amekusanya hadithi simulizi hamsini (50) za Visiwani Zanzibar na kuzifafanua fani na maudhui kifalsafa. Hadithi hizo zimefafanuliwa kwa mtindo wa sanaa jaadiya. Pili ni Senkoro,(1997), tasnifu yake imefafanua umuhimu wa safari katika hadithi simulizi za Visiwani Zanzibar. Tasnifu imekusanya hadithi simulizi thalathini na tano (35). Katika hadithi simulizi kunakuwepo na wahusika au muhusika. Hawa hufanya safari ya kutoka nnje ya jamii yao kutokana na mgogoro wa kijamii au kifamilia. Muhusika au wahusika hufanya safari ya kutatua tatizo au matatizo. Wako mashujaa ambao baada ya safari hurudi kwao na ushindi, wako wanaorudi kwao lakini huonekana kuwa hawana umuhimu sana katika jamii yao, wako mashujaa ambao wamepata matatizo katika

safari yao, hawakufa na hurejea tena kwao, na wako wanaorejea kwao na habari za uongo. Kwa hivyo, mtafiti ameonafika nafasi ya kukusanya hadithi simulizi sitini na moja (61) na kujadili nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za sekondari, Visiwani Zanzibar.

### **1.3.1 Usuli wa Tatizo**

Historia inaeleza kuwa mara tu baada ya binadamu kuanza kuishi pamoja, ilizuka haja ya mawasiliano ambayo yaliibuwa fasihi, ambayo jamii inaitumia katika kuelekezana vipengele mbali mbali vinavyohusu maisha kwa jumla. TAKILUKI (1982), wanasema kuwa kila jamii ina Fasihi yake. Wazanzibari kama jamii nyingine wana Fasihi yao ambayo huitumiya katika kueleweshana vipengele mbalimbali vya kimaisha kama vile kimapenzi, kisiasa, kiuchumi, kidini na kimaadili.

Fasihi ni sanaa itumiayo maneno ili kutoa picha ya mwanadamu, akiwa maishani mwake, mahusiano yake na viumbe wengine, migogoro yake na mazingira, shida zake, raha, matumaini yake na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake. Pamoja na shughuli zote walinazofanya Wazanzibari, inahuzunisha kwamba wapo wale wenye nguvu zao, aidha, kutokana na utandawazi ambao Chachage aliuita “Utandawizi” umewaharibia Wazanzibari yao zaidi kuliko kuwanufaisha. Hivi sasa, vijana wengi wa kike na wa kiume ambao Shule za Sekondari wasomazo zimejengwa karibu na mahoteli ya kitalii, wanaamua kubadili utamaduni wao na kuvutika na utamaduni wa kigeni, hivyo kuathiri maadili mema ya Kizanzibari. Tatizo hili linaonekana katika sehemu za Nungwi, Pwani mchangani, Uroa, Paje na Bwejuu. Wanafunzi wa Sekondari katika sehemu hizo wanaonekana kuathirika kimaadili mema.

### **1.3.1.1 Uchumaji wa Karafuu**

Bwana Dadi wa Kilimahewa-Unguja ameelezea kuwa maendeleo ya ulimbe na utunduizi yameiwezesha fasihi simulizi za utamaduni wa kigeni kuonekana zaidi katika runinga, yamechangia kuharibu maadili mema ya wanafunzi Visiwani Zanzibar. Sehemu nyingi za Unguja na Pemba, wakati wa kuchuma karafuu, ilikuwa ni moja ya sehemu ambayo wazee walijikusanya jioni na kuchambua karafuu huku wakiwafunza watoto wao maadili mema na uimarishaji bora wa zao la karafuu. Baada ya kuingia kwa runinga, wanafunzi wengi wanapenda kuangalia runinga ambazo zinaonesha vipindi vinavyochangia kuathiri maadili mema ya Kizanzibari kama vile muziki wa kihuni, matusi na mavazi yasiyofaa. Hali hiyo huwafanya baadhi ya wanafunzi wa Kizanzibari kuchota utamaduni wa nnje na kuacha utamaduni wao wa asili.

### **1.3.1.2 Matumizi ya Pataninga (video)**

Kitengo cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (2011), wanasema kuwa pataninga huonesha matendo ambayo vijana hawatakiwi kuyaona kutokana na umri wao hasa wakiwa ni wanafunzi, kama vile picha za ngono na muziki wa kigeni. Vitendo hivyo huwapa ushawishi mkubwa vijana wa Kizanzibari na hatimaye kujiingiza katika uchafu na dhambi hizo wakiwa bado wadogo. Hali hii huengeza kasi ya muharibiko wa kimaadili ya Kizanzibari. Kwa hivyo, baadhi ya wanafunzi wa Shule za Sekondari huharibikiwa na masomo, afya na uhai.

### **1.3.1.3 Matumizi ya Wavu Pepe**

Mwalimu Ali Bakari (S.O.S), amesema kuwa baadhi ya wanafunzi wa Shule za Sekondari wanatumia vibaya wavupepe shuleni. Wengine hutumia chombo hiki kwa

kutazama picha za ngono, kusikiliza muziki na kucheza, na kusahau masomo yao. Kitendo hiki kinaharibu maadili mema ya baadhi ya wanafunzi wa Kizanzibari katika Shule za Sekondari na kurudisha nyuma maendeleo yao ya elimu.

#### **1.3.1.4 Uvunjikaji wa Ndoa**

Salama Njani (Zanzibar Leo, 24/6/2011.), ameelezea kuwa vijana wanaosoma Shule za Sekondari, wameweza kushawishika na vikundi vya vijana ambao hawana maadili mazuri katika ndoa. Aidha amesisitiza kuwa katika mazingira ya Kizanzibari, mtoto/watoto hulelewa na wazazi wake/wao wawili, baba na mama. Panapotokea kuvunjika kwa ndoa na wazee kuachana, mtoto/watoto hulazimika kumfuata ama mama au baba. Watoto wanapolelewa na mama wa kambo, hulazimika kuishi katika hali ambayo hupoteza malezi na uangalifu unaosababisha kutokea mabadiliko ya kimaadili. Uswahilini kuna tabia ya kuleleana watoto mpaka ikafika wakati wa kuoa au kuolewa.

Bwana Juma Simai (MNUNGWI 2011), amesema kuwa mwaka, 2009, wanawake wa Nungwi waliandamana kutoka Nungwi hadi Mkokotoni, kiasi cha maili kumi kwa miguu hadi kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kupinga vitendo vya ukahaba vilivyokuwa vinafanywa na wanawake kutoka Tanga (walioajiriwa kazi za hotelini.) Vitendo hivyo vilisababisha uengezekaji wa uvunjikaji wa ndoa kwa wenyeji wa Nungwi. Alisisitiza kuwa watu wa Nungwi na vitongoji vya jirani wameathirika sana na malezi ya watoto na maendeleo ya Shule za Sekondari. Kitendo hicho kiliwalazimisha wazee wa Nungwi kuamua kuvitia moto vibanda vya ukahaba, walivyojenga na wageni kwa kisingizio cha "Utalii" eneo la Pwani

Mchangani, kwa sababu vinachangia kuharibu maadili mema ya wanafunzi wa Shule za Sekondari.

Sheha wa Matemwe (Zanzibar Leo, 24/5/2011), amesema kuwa Kijiji cha Matemwe kina hoteli za kitalii na kimeweka mipaka ya utamaduni wa kigeni wa kuwa faraha na sio kwenye jamii. Ni marufuku kuyatenda yanayotendwa ufukweni, mitaani. Lakini shule ziko karibu na fukwe, kwa hivyo wanafunzi wengi wa Sekondari wanaathirika na maadili ya kigeni. Kitendo hicho kinaathiri kiwango cha masomo kwa wanafunzi, mradi kuna ruhusa hiyo, ni wazi kwamba jamii na Serikali ya mtaa wametoa idhini.

#### **1.3.1.5 Shule Zilizo Karibu na Fukwe za Bahari**

Mwalimu Ali Bakari na wanafunzi wa S.O.S (Ziara ya kimasomo Kiwengwa), Wamesema kuwa biashara ya utalii Visiwani inaingiza kipato nchini, lakini inaharibu maadili ya Kizanzibari. Kuruhusiwa kwa watalii kuvaa mavazi wanayotaka katika Visiwa vya Zanzibar kumewafanya baadhi ya vijana wa Kizanzibari kuacha utamaduni wao na kufuata maadili ya kigeni. Shule ambazo ziko karibu na hoteli za kitalii zinaonekana kuathirika zaidi. Kiwengwa, mtalii anaweza kuonekana akiwa na mavazi yasiyokubalika na kufika hadi katika shule. Kitendo hiki kinawakera wanajamii na huathiri maadili mema na maendeleo ya masomo yao katika Shule za Sekondari

#### **1.3.1.6 Matumizi Mabaya ya Madawa**

Afisa, kitengo cha ukimwi, Shaaban Saadat (2011), ameelezea kuwa uingiaji na matumizi ya dawa ya kulevya, ulevi na uvutaji bangi, Zanzibar unafanyika kwa siri

sana na kwa kutumia mbinu tafauti lakini madhara yake yanaonekana haraka sana na hasa kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari. Wanafunzi wanapoyatumia, hawawezi tena kuendelea na masomo.

Wako wanaopungukiwa na akili na baadhi huwa vichaa. Watumiaji bangi hudai ni kwa ajili ya kuingeza nguvu. Watumiaji unga wanadai wamekosa cha kufanya. Kwa hivyo madawa ya kulevya ni chanzo cha kupoteza maadili mema, cha kupata maradhi mbalimbali yakiwemo magonjwa ya akili, ukimwi na homa ya ini.

Maalim Seif Sharif Hamad (Zanzibar Leo, Mei, 2011), amesema kuwa vijana wa Kizanzibari hivi sasa wanakabiliwa na matatizo ya kuporomoka kwa maadili mema katika shule na taasisi za elimu. Hivyo, wazazi, walezi na walimu washirikiane kujenga maadili mema, badala ya wanafunzi kuwa msaada wamekuwa mzigo kwa taifa. Alisisitiza kuwa kundi kubwa la wanafunzi hawana nidhamu wanapokuwa madarasani au katika maeneo ya shule hasa wale wanaojihusisha na dawa ya kulevya.

#### **1.3.1.7 Wazazi Hawahimizi Watoto wao Kwenda Shule**

Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Haji Makungu Mgongo, (Zanzibar Leo. Mei, 17/2011) ameelezea kuwa wazazi hawatili mkazo elimu ya Sekondari na wanafunzi wanaacha masomo katika shule za Sekondari kutokana na kuwa baadhi ya wazee hawana mwamko wa kielimu. Wazee hawahimizi watoto wao kwenda shule. Kiasi kikubwa cha wanafunzi wanapofika katika shule za Sekondari huona wameshakuwa watu wazima kwa hivyo huwa na uhuru wa kuamua kuendelea na shule au kutokuendelea na shule. Kipindi hiki wanafunzi hawa hujiingiza kweye



disiko, ngoma, uuzaji wa vileo na hasa katika kipindi cha mwaka kogwa. Kwa hivyo, wanafunzi wengi wa kike na wa kiume, fikra zao huchotwa zaidi na upotokaji kuliko taalimu kutokana na kushuka kwa maadili.

#### **1.3.1.8 Wanafunzi Wanaopata Ujauzito**

Mhariri wa Zanzibar Leo, (24/5/2011), ameelezea kuwa baadhi ya wanafunzi wa kike wa Sekondari mbalimbali ambao wanapata ujauzito wakiwa bado ni wanafunzi. Kuna idadi kubwa ya vijana wanaokatisha masomo na kujiingiza katika ukahaba ikiwa umri ambao haujakomaa kuchukuwa ujauzito. Kuna kesi thamanini na sita (86), za wanafunzi, ambao, baada ya kupata ujauzito na wameolewa lakini ndoa zao hazikuchukuwa muda mrefu wakaachana na kutelekezwa na watoto.

Hali hiyo husababisha ongezeko la wajane, watoto wa mitaani, ombaomba, ukahaba na maradhi ya ukimwi. Jambo hili linaonekana kuwaathiri kimaadili mema yanayositahiki kwa wanafunzi mbalimbali wa Shule za Sekondari Zanzibar na kushusha kiwango cha elimu na maendeleo ya nchi katika jamii ya Zanzibar.

### **1.4 Lengo la Utafiti**

Kujadili nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar.

### **1.5 Madhumuni Maalumu ya Utafiti**

1. Kuzikusanya hadithi simulizi mbalimbali kutoka kwa wanafunzi, wazee na walimu wa Kizanzibari na kuzichambua ili kutafiti dhima zilizomo na jinsi

zinavyoweza kuathiri malezi ya kimaadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar.

2. Kutafiti na kuainisha maadili mema mbalimbali ya hadithi simulizi yenye mafunzo kwa wanafunzi wa shule za Sekondari Visiwani Zanzibar.
3. Kutafiti mbinu mpya na muda wa kufundishia hadithi simulizi katika kufunza Maadili mema Visiwani Zanzibar ili kuwashawishi wanafunzi wengi wa shule za Sekondari kupenda kujifunza hadithi Simulizi kwa urahisi.
4. Kuwashauri walimu wa shule za Sekondari kutumia mbinu za kisayansi na teknolojia katika ufundishaji wa hadithi simulizi ili kukuza kiwango cha elimu shule za Sekondari.

### **1.6 Maswali ya Utafiti**

1. Je, hadithi ni nini na zina nafasi gani katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar ?
2. Je, kuna mikabala ya aina ngapi ya maadili mema katika hadithi simulizi inayoweza kutolewa kwa mujibu wa wazee, walimu na wanafunzi wa shule za Sekondari Visiwani, Zanzibar ?
3. Ni mbinu gani za hadithi simulizi zinazotumika katika kufunza maadili mema kwa wanafunzi wa shule za Sekondari, Visiwani Zanzibar?
4. Ni ugumu upi wa kutumia hadithi simulizi katika kuwafunza maadili mema wanafunzi wa shule za Sekondari Visiwani Zanzibar?

### **1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Kwanza ni muhimu kwa kuongezea thamani nafasi ya hadithi simulizi katika kuwafunza maadili mema wanafunzi wa shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Pili,

utaiwezesha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kujua mbinu mbalimbali za kurahisisha ugumu uliopo katika kutumia hadithi simulizi katika kufunza maadili mema wanafunzi wa Shule za Sekondari za Zanzibar. Tatu, utawasaidia walimu wanaofundisha somo la Kiswahili kuelewa na kupata mbinu mpya za kufundishia hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za Sekondari, Zanzibar. Nne, ni kuwashauri walimu wa shule za Sekondari kutumia mbinu bora katika kufundisha hadithi simulizi na maadili mema Visiwani Zanzibar.

### **1.8 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu umefanyika katika viambo vya Visiwa vya Zanzibar pamoja na Shule za Sekondari mbalimbali zinazofundisha somo la Kiswahili.

1. Wilaya ya Wete, shule za Sekondari za Utaani, Miti Ulaya na Kizimbani.
2. Wilaya ya Kusini- Pemba, Shule ya Sekondari ya Michenzani.(Chokocho).
3. Wilaya ya Kaskazini-A, Unguja, Shule ya Sekondari, Tumbatu Kichangani.
4. Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI), Shule ya Sekondari Bembella, Hailesalassie na Bububu.

Mtafiti amechagua sehemu hizo kwa sababu zinafundishwa somo la Kiswahili na ziko sehemu mbalimbali za Zanzibar kwa kupatia taarifa zinazowakilisha nchi nzima.

### **1.9 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umefanyika katika Hadithi simulizi za vigano, sogu na ngano. Jumla ya hadithi zilizokusanywa ni 61, hadithi 21 ni za vigano, 27 ni za sogu, na 13 ni za ngano. Kila aina ya hadithi imeainishwa mikabala ya maadili mema iliyojitokeza.

### **1.10 Matatizo**

- (i) Athari za utandawazi-kudharaulika kwa fasihi simulizi katika jamii. Mtafiti wa fasihi simulizi akiwa katika jamii na kufanya kazi yake huonekana kama anafanya kazi isiyokuwa na hadhi katika shule au maskani.
- (ii) Jamii huchotwa akili ya kukubali machafu ya kigeni kuwa kigezo cha usasa, maendeleo na mafanikio
- (iii) Shule nyengine ziko mbali, mtafiti amelazimika kusafiri kwa kutumia boti za wenyeji au kukodi boti za doria za askari wa vikosi maalumu (K.M.K.M), Mkokotoni ili ufike Tumbatu na kufanya utafiti.
- (iv) Ucheleweshaji wa kupata fedha za kufanyia utafiti kutoka kwa mfadhili ambaye ni Chuo Kikuu Cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Mtafiti amelazimika kujitegemea wakati wote wa kusafiri akiwa kwenye masomo.

## SURA YA PILI

### 2.0 KAZI TANGULIZI

#### 2.1 Utangulizi

Katika kipengele hiki mtafiti amesoma machapisho mbalimbali na kuvihakiki vitabu, tasnifu na majarida yanayohusiana na mada. Pia mtafiti amesoma makala na majarida mbalimbali katika mitandao. Mtafiti amezisoma kazi hizo kwa nia ya kupata taarifa juu ya mada anayoitaftiti, kusoma na kufahamu vyema maana ya hadithi na nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar. Taaluma aliyopata mtafiti ya hadithi simulizi ilimuongoza katika kufanikisha utafiti huu. Miongoni mwa kazi hizo ni hizi zifuatazo:

TAKILUKI, (1982), wanaeleza kuwa hadithi ni masimulizi ya kinadhariya (si ya kisheria). Wamesisitiza kuwa wahusika hujenga mtiririko wa tukio unaokamilisha hadithi hiyo na kutoa maadili kwa jamii inayohusika. Pamoja na kutoa mifano ya wahusika. Kazi hiyo haikusadifu lengo la utafiti ila ilimuongoza mtafiti kuendelea na utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili Visiwani Zanzibar.

Msokile, (1992), ametoa maana ya hadithi simulizi ni sanaa ambayo huhifadhiwa kwa kichwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Amesisitiza kuwa fasihi hii hurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi.

Sengo na Ngole, (1993), wameelezea katika hadithi simulizi yao iitwayo KIBOKO na TEMBO kuwa wanyama wakubwa wanatoa maadili muhimu katika jamii hiyo husika. Kazi hiyo haikutoa ufafanuzi zaidi. Hata hivyo ilimuongoza mtafiti kujua

kuwa wahusika wakubwa wanajenga maadili hivyo aliendelea na lengo lake la kutafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Ndere, (2003), ameeleza kuwa watoto hufunzwa mambo mengi ya kijadi kwa kusimuliwa hadithi za paukwa pakawa ili kuendeleza utamaduni wa jamii. Kazi hii ilimpa fursa mtafiti kuendelea na lengo lake.

Ngere, (2004), ameeleza kwa maneno machache kuwa hadithi fupi simulizi za Kiswahili zinategemea kuweza kwa msanii katika kusimulia kufuatana na mfumo mzima wa kihistoria wa kijamii. Aidha amesisitiza kuwa hadithi moja inaweza kusimuliwa katika sehemu tafauti za kijamii. Kazi hiyo haikusadifu kutoa mchango juu ya utafiti, hata hivyo, imempa nafasi mtafiti na kumuongoza kuendelea kutafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Njogu na Chimera, (1999), wamesisitiza kuwa hadithi inaweza kubadilika inaposimuliwa na mtu mwingine lakini maudhui yake yakabakia vile vile. Makala hayo ya hadithi hayakufafanua juu ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Ndere, (2003), ameeleza kuwa hadithi simulizi ni lazima msimuliaji aipe msukumo hadithi yake ili wale wanaomsikiliza wapate mantiki ya hadithi yake, dhamira, hali halisi ya maisha. Aidha chini ya maelezo hayo amefafanua kuwa hadithi simulizi huonesha uzuri au ubaya wa watu wa kale au watu wa sasa. Kazi hii ilimpa fursa mtafiti kuwa huru na kuendelea kutafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Sengo, (1993), ameelezea kuwa fasihi simulizi inamfanya msikilizaji afikiri zaidi katika kile kinachozungumzwa au kutendwa kwani haya yote si kweli lakini inakuwa kweli katika uongo. Wamesisitiza kuwa mwanafasihi simulizi anatumia chura kistiari au kitashbiha, sungura au fisi. Kwa hakika kazi hii imetoa mwangaza juu ya mada ya mtafiti, kwa kuonyesha wahusika wa hadithi simulizi walivyo. Uchunguzi wa mtafiti unaonesha kuwa haikuonyesha nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Sengo na Ngole, (1993), wamezungumzia kuwa ufundishaji wa fasihi simulizi kwamba haukupewa kipaumbele zaidi kama fasihi andishi. Iko haja ya kufanya utafititi zaidi. Kazi hii ilimsaidia kidogo mtafiti kulingana na mada. Mtafiti alibaini kuwa aendeleo na lengo lake la kutafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar .

TAKILUKI, (1981), wametoa maana ya hadithi simulizi kuwa ni masimulizi ya kinathari yasiyo ya kishairi. Wamesisitiza kuwa wako wahusika katika hadithi simulizi, wanaweza kuwa wanadamu, wanyama, vitu, pahala, zimwi, shetani na wengineo ambao wanaweza kutumiwa kutenda matendo ya kibinadamu na kuakisi dhamira iliyokusudiwa. Kwa mfano, simba huwakilisha dhanna ya ukali, sungura huwakilisha dhanna ya ujanja, fisi woga na tamaa. Kazi hii, pamoja na kutoa mifano halisi, mtafiti ameona kuwa hadithi simulizi zina wahusika wa aina mbalimbali, lakini haikutoa maelezo juu ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Mulokozi, (1992), ametoa maana ya hadithi fupi kwamba ni aina ya kazi za sanaa ya utunzi wa hadithi inayotumia lugha iliyoandikwa. Hadithi ya aina hii inatumia tukio

moja au matukio mawili na inatumia mawanda yasiyo mapana sana, haina changamano na hutumia wahusika wachache sana. Maelezo haya yalimsaidia mtafiti kujua kuwa ziko hadithi fupi fupi zilizoandikwa ambazo si masimulizi.

Mbunda, (1996), ametoa ufafanuzi mkubwa kwamba hadithi ni msingi mkubwa wa fasihi simulizi na unachukua nafasi kubwa katika ufundishaji wa fasihi simulizi. Hata hivyo amesisitiza kuwa hadithi ni lazima zifanyiwe uchaguzi kufuatana na matakwa ya wanafunzi na mazingira yakiruhusu kupatikana kwa mtambaji maarufu mtaani ni vyema, wanafunzi waongozwe kuhusisha maudhui na maadili katika mazingira halisi ya kimaisha. Kazi hii imempa faraja mtafiti kwani iligusia kidogo katika mada lakini haikuelezea vyema nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Kirumbi, (1975), amezungumza kuwa hadithi za mapokeo zimekusudiwa kufanya kazi tatu muhimu, kufunza, kuhifadhi na kukuza lugha. Amesisitiza kuwa kwa upande wa mafunzo, hadithi zinatarajiwa kuwavutia wengi na kujifunza maadili yake na zitaendelea kuchukua muda mrefu katika masimulizi kutoka kizazi hadi kizazi. Maelezo yanatoa ufafanuzi zaidi wa hadithi simulizi kuwa zinasimuliwa, zinatoa mafunzo na kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi lakini hakufafanua nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Songonyi, (1997), amezungumzia kuwa hadithi ni njia moja wapo ya mawasiliano kwa Wakikuyu na pia ni njia ya kuendeleza utamaduni wa Wakikuyu pamoja na haya hutumika katika kuendeleza maadili na utamaduni wa Wakikuyu, Kenya, kazi



hii imemuonesha mtafiti nafasi ya hadithi simulizi kwa Wakikuyu, pia ilimuhamasisha kutafuta nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Kimani na Rocha, (1999), wametoa maana kuwa hadithi ni sanaa asilia inayotumia masimullizi na matendo ya msimuliaji na wasimuliwaji ili kurithisha utamaduni na maadili ya jadi kama inavyonekana katika kabila la Wamasai. Hata hivyo hawakufafanua zaidi inavyotumika katika jamii ya Wamasai ila ilimsaidia mtafiti kuona yuko huru kuendelea na utafiti wake wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Masebo na Nyangwine, (2002), wameelezea kuwa hadithi ni tungo za fasihi zitumiazo lugha ya nathari. Wameendelea kusesitiza kuwa masimulizi hayo hupangwa katika mtiririko wa vituko unaokamilisha kisa. Hadithi huwa na wahusika ambao ndiyo nyenzo ya kukiendesha kisa chenyewe. Kwa hivyo huwa na maudhui yenye kutoa maadili. Hata hivyo maelezo yao hayakusadifu na mada ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Mvungi, (2010), ameeleza kwa maneno machache kuwa hadithi ni masimulizi marefu kidogo yanaolenga kuadilisha na pia hadithi huonesha tukio la kawaida. Ila amesisitiza kuwa matukio yake aghalabu huwa mazuri kwa baadhi ya wahusika na mabaya kwa wengine. Hatimaye hadhira inaadilika. Kazi hiyo imetoa ufafanuzi kidogo juu ya hadithi inavyoanza na kumalizika. Hii imemsaidia mtafitia kutaka kujua nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili Visiwani Zanzibar.

Jarida la Kiswahili (TUKI:1983), limeeleza kuwa hadithi simulizi zinazoandikwa katika magazeti huwa na viwango tafauti na mara nyingi ni za hali ya chini kimaudhui lakini hupendwa na watu wengi na hata gazeti pia hupata umaarufu katika jamii hiyo, hadithi hizi huwa na maadili mbalimbali. Kazi hii imembainshia mtafiti kuwa ziko hadithi simulizi ambazo huhifadhiwa katika maadishi, kwa hivyo ni vyema kusoma magazeti na kufanya utafiti zaidi juu ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili Visiwani Zanzibar.

Kamera, (1978), amekusanya hadithi kumi na saba, zenye wahusika mchanganyiko. Kamera amehifadhi hadithi za Wairaqw ambapo hakuzungumzia mafunzo ya hadithi hizo. Kazi hii imemsaidia mtafiti kusoma hadithi za Wairaqw ili kujua mtiririko wa hadithi ulivyo na kuendelea kufanya utafiti katika mada ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Tasnifu ya Sengo, (1985), imezungumzia sanaa jadiya ya utendezi wa hadithi simulizi ambazo zimekusanya sehemu kubwa katika kisiwa cha Unguja. Kazi hii imemsaidia mtafiti kusoma hadithi mbalimbali zilizokusanywa katika Visiwa vya Zanzibar. Maudhui yalichambuliwa kifalsafa kudhihirisha elimu iliyomo ambayo ni pamoja na maadili. Kwa hivyo mtafiti alipata nafasi ya kuendelea kufanya utafiti katika mada aliyokusudia.

Balisidya, (1987), ameelezea kuwa hadithi za “paukwa... pakawa” na kuishia, ”wakaishi raha mstarehe” ahaghalabu zina nyimbo. Amesisitiza kuwamba kwa kawaida ni nyimbo huibuwa maadili ambayo husimuliwa katika mazingira ya

starehe. Mwisho amezidi kuelezea kwamba huwa na wahusika wa aina mbalimbali kama vile wadudu, wanyama, binadamu, mizimu na miungu, aidha viumbe visivyo na uhai kama mawe na miamba. Mara nyingi wahusika hawa hupewa urazini wa binadamu ili kuadilisha. Kwa kulibaini hili, kazi hii imemsaidia mtafiti kumpa ufafanuzi juu ya wahusika ambao wamo katika hadithi simulizi.

Senkoro, (1997), amezungumziya umuhimu wa safari katika hadithi simulizi. Kazi hiyo imekusanya hadithi mbalimbali. Hadithi zilizomo zimemsaidia mtafiti kujua muundo wa hadithi za Visiwani zinavyojitokeza. Hata hivyo mtafiti alijiona yuko huru kuendelea na utafiti wake kuhusu nafasi ya hadithi similizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Said, (2007), ameelezea nafasi ya mwanamke katika hadithi fupi fupi za Kizanzibari. Pia alisisitiza kuwa wizara inayosimamia elimu ifanye juhudi za makusudi za kuliingiza somo la hadithi fupi katika mitaala na zifundishwe katika shule kama kazi nyengine za fasihi andishi. Hata hivyo, hakuonesha ni aina gani za hadithi zilizopo Zanzibar na maadili yanavyojitokeza. Kazi hii imemsaidia mtafiti mambo mawili. Kwanza kuona kuwa eneo la utafiti alilolichagua bado halijafanyiwa utafiti. Pili, kuendelea na kufanya utafiti katika mada ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Mussa, (2008), amezungumzia nafasi ya ndoa katika hadithi simulizi za lugha ya Kiswahili. Amesitiza kuwa ndoa siyo jambo la kuchezewa. Ni lazima wazee wawajibike katika suala la kutoa taaluma kwa kutumia hadithi simulizi. Mwisho

amesisitiza kufanya utafiti katika sehemu nyengine za hadithi. Kazi hii imemsaidia mtafiti kutimiza azma yake ya kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Balisidya, (1987), ametoa maana ya hadithi za visasili na kufafanua wahusika wa aina mbalimbali kama vile miungu na binadamu ambao husimulia juu ya matokeo ya kiada. Amesisitiza kuwa wahusika hawa hujaribu kuielezea miviga, imani na dini za jamii. Aghalabu hadithi za aina hii hutambwa mivigani. Kazi hii imemsaidia mtafiti kujua aina nyengine za hadithi simulizi lakini haikusadifu nia ya mtafiti ya nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Mulokozi, (1989), amegusia kwamba hadithi za visakale ni masimulizi ya kimapokeo juu ya wahenga na mashujaa ya kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia kama vile hadithi ya Lyyongo. Kazi hii imemsadia mtafiti kujua kuwa baadhi ya wataalamu wa hadithi za visasili haviita visa kale. Hata hivyo haikumzuia mtafiti kuendela na kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Mulokozi, (1989), ameelezea hadithi simulizi za historia zaidi kuliko dini. Amesema kuwa mara nyingi huonesha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, kuhusu asili yao wenyewe na maana ya shabaha ya maisha kwa jamii yao. Amesistiza kuwa mara nyingi hadithi hizi huaminika kuwa ni kweli tupu, hutumika katika kuelezea au kuhalalisha baadhi ya mila na madhehebu yanayohusika. Kazi hii imemsaidia mtafiti na imempa nafasi ya kuendelea na utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Mulokozi, (1996), amegusia kwamba visakale ni hadithi ya kale kuhusu maisha, taifa, kabila au dini, mara nyingi huchanganya historia na masimulizi ya kubuni. Hadithi hizo hupatikana katika kila kabila. Maelezo hayo yalimpa nguvu mtafiti na kuendelea kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1996), wamelezea kwamba visasili ni hadithi fupi zinazotumia wahusika wa aina mbalimbali pamoja na binaadamu. Wamesisitiza kuwa hadithi hizi husimulia mambo yanayohusiana na maumbile ya watu, wanyama, miti, vitu visivyo na uhai. Pia wamefafanua kuwa mara nyengine hadithi hizo hutambwa kwenye miviga. Kazi hii imempa mwelekeo mtafiti kwa kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Ndungo na Wafula, (1993), wamegusia kwamba visasili ni aina ya hadithi ambazo huelekeza asili ya mtu au jamii au mambo mengine kama vile asili ya kifo, ndoa au dhambi. Kazi hii ilimjenga mtafiti kuendelea na kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Hamadi, (2005), amesema kwamba Wazanzibari hawana budi kuhifadhi hadithi (visasili) kama urithi walioachiwa na wazee wao, hawana budi kuuenzi, kuendeleza na kuulinda kwa nguvu zote, na kuupoteza ni sawa na kuuza utu wao bila ya pesa. Amesisitiza kuendeleza kufanya utafiti. Kazi imeshawishi utafiti ufanywe kwa kumpa nafasi zaidi mtafiti kuendelea kutafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Masebo, (2002), amesema kwamba visakale ni hadithi ambazo husimulia matokeo ya kihistoria. Yanaweza kuwa ya kweli. Amesisitiza kuwa matokeo haya hujengwa kisanaa ili kuwavutia watu. Mara nyingi wahusika wake ni binadamu ila hupewa uwezo mkubwa au mdogo mno kulingana na matukio yanayosimuliwa. Kazi hii ilimpa nafasi ya kuendelea kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Masebo, (2002), amegusia hadithi za visasili zinazotumia wahusika wa aina mbalimbali, na binadamu. Amesisitiza kwamba visasili ni hadithi zinazoonesha uasili na uhusiano, maumbile ya watu, wanyama, miti au vitu visivyo na uhai, na taratibu za jamii inayohusika. Pamoja na kutoa ufafanuzi mfupi wa kimaana. Kazi hii inatoa mchango wa hadithi za visasili katika jamii. Aidha utafiti unahusu nafasi ya hadithi simulizi katika kutoa maadili mema Visiwani Zanzibar.

Balisidya, (1987), ametoa maana na wahusika wa hadithi za tarihi ambazo husimulia juu ya tukio au matukio ya kihistoria. Matukio haya yanaweza kuwa ya kweli ila hufungwa katika sanaa ya ubunifu ndani yake kwa kadiri ya kupeleka ukweli. Amesisitiza kuwa wahusika wake ni binadamu, ila hawa hupewa uwezo mdogo mno kuyakinisha matokeo. Kazi hii imemsaidia mtafiti kuzijua aina nyengine zilizoko za hadithi simulizi katika jamii kubwa zaidi ya Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1996), wamefafanua hadithi ambazo husimuliwa matukio ya kihistoria. Aidha wameeleza kuwa matokeo yanaweza kuwa ya kweli. Ili kuwavutia watu, mara nyingi wahusika wake ni binadamu ambao hupewa uwezo mkubwa au mdogo mno kulingana na matokeo yanayosimuliwa. Kazi hii imemsaidia

mtafiti kupata ufafanuzi zaidi juu ya hadithi za tarihi. Mtafiti anajiona anayo nafasi ya kuendelea na utafiti wake wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwan Zanzibar.

Mulokozi, (1989), amefafanua kwa maneno machache maana ya hadithi za ngano zitumiazo wahusika, wanyama, miti na watu ili kuelezea au kuonya kuhusu maisha. Mwisho amesisitiza kuwa ngano ni fani iliyoenea sana katika fasihi simulizi ya Afrika, hadithi hizi za kubuni wanyama lakini pia ziko zinazihusu binadamu, mazimwi, majini na malaika, nyingi zinasimulia kwa urahisi, ujumbe na maadili yaliyokusudiwa. Kwanza kazi hii imemsaidia mtafiti kuweza kujua hadithi nyengine za ngano. Pili, imempa nafasi zaidi ya kutafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1996), wamezungumzia ngano kwa ficho la hadithi fupi zisimuliwazo ili kuwaasa watoto kwenye maadili ya jamii fulani. Mara nyingi ngano huanza kwa “Paukwa ---- Pakawa” na kuishia na wakaishi kwa “raha mustarehe”. Chanzo cha hadithi za ngano huambatana na nyimbo. Aidha wahusika wadudu, wanyama, binaadamu, mizimu, na miungu na vitu visivyo na uhai. Wahusika wa aina zote hupewa hadhi na uwezo wa kibinadamu, ili malengo ya msanii yaweze kutimizwa. Kazi hii imetoa mchango mkubwa katika kazi ya mtafiti na imemsaidia kuendelea na lengo lake la utafiti.

Ndungo na Wafula, (1993), wamegusiya kwa maneno machache kuwa ngano ni hadithi ambazo hurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi chengine, huwa na

mianzio maalumu, urudiaji wa maneno au matukio ili kusesitiza maudhui fulani. Amsisitiza kuwa huwa na matumizi ya nyimbo na kubadilisha mtindo ili kushirikisha hadhira na kufahamu vyema maadili na ujumbe ambayo hutajwa wazi kwa kutumia methali. Kazi hii imemsadia mtafiti na ilimpa ushawishi wa kuendelea na utafiti.

Said, (2005), amezungumzia maadili katika hadithi simulizi za jamii ya Wazanzibari. Amesisitiza kuwa vyombo vya habari vihamasishe jamii ili kuzithamini na kuzirithisha kwa vizazi vyao, kwa kuzisimuliya, kuzirikodi au kuziandika. Kazi hii imemsaidia mtafiti kujua kuwa hadithi za ngano ni chache sana katika jamii.

Skool, (2008), amegusiya ngano kijuu juu. Ametoa maana kuwa ni aina ya sanaa katika fasihi simulizi ambayo husimuliwa kwa lugha ya nadhari na hutumia lugha ya mdomo kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Masebo na Nyangwine, (2002), wametoa maelezo machache kuhusu maana ya hadithi za ngano kuwa ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea au kuonya kuhusu maisha. Masebo na Nyangwine wamesisitiza kuwa hutoa maadili ambayo husimuliwa katika mazingira ya starehe. Mwisho ameelezea kuwa huadili kwa kutumia stiara, kharifa, hekaya na kisa. Kazi hii imetoa mchango juu ya hadithi simulizi katika kufunza maadili. Pia mtafiti alipata nafasi na kujiona huru ya kuendelea lengo lake la utafiti.

Masebo na Nyangwine, (2002), wametoa maana ya kigano kuwa ni hadithi fupi zinazoelezea makosa au uovu kwa watu fulani na kuelezea maadili yanayofaa na mara nyingi hutumia methali kama msingi wa maadili yake. Aidha hakuna maelezo



zaidi kuhusu nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili. Kwa kulibaini hilo mtafiti aliendelea na lengo lake la utafiti nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1996), wametoa maana ya ngano/vigano kuwa ni hadithi fupi na zinasimuliwa kama mifano ya kuadilisha watu. Wamesisitiza kuwa ngano/ vigano mara nyingi hutumia methali kama msingi wa maadili. Kazi hii ilimpa nafasi ya kuendelea na lengo lake la utafiti.

Mvungi, (2010), amegusia kuhusu kigano kuwa ni usimulizi wenye kisa kimoja unaoadilisha watoto na vijana, kinaweza kusimulia kuonyesha faida na hasara kuhusu jambo linalosimuliwa. Mwisho msimulizi huwaasa wasikilizaji kwa kutumia aina fulani ya methali kama vile asiyesikia la mkuu huvunjika mguu. Pamoja na kubainisha maana hiyo, hakuna maelezo zaidi hivyo aliendelea na lengo lake la utafiti.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1996), wametoa maana na maelezo mafupi kuhusu soga kuwa ni hadithi fupi zinazosimuliwa kwa nia ya uchekehashaji na kukejeli. Mara nyingi wahusika wake ni watu wa kubuni.

Masebo na Nyangwine, (2002), wametoa maana ya soga kuwa ni hadithi fupi za kuchekecha na kukejeli. Wahusika wa soga ni watu wakubuni. Pia wahusika wanaweza kupewa majina ya watu waliomo katika mazingira ya jamii husika. Wamesisitiza kuwa Soga husema ukweli unaomiza lakini ukweli huo unajengewa kichekesho ili kupunguza ukali wa ukweli kwa hadhira.

Mvungi, (2010), amezitaja hadithi za sogu kuwa ni hadithi fupi zinazosimuliwa aghalabu na vijana kwa vijana wenzao katika kujiburudisha na kujiliwaza. Lengo kuu la hadithi hizi huwa ni kuonyeshana kiwango cha ujuzi wa shughuli fulani ambayo hujenga maadili kwa hadhira. Amesisitiza kuwa msimuliaji hutia chumvi katika sogu ili asichekwe kwa kuonekana kuwa hajui jambo, maumbile au taratibu za jamii inayohusika.

Mulokozi, (1996), ametoa maana kuhusu hekaya kuwa ni hadithi ya mapokeo iliyo ndefu kiasi, yenye masimulizi ya kulisimua na kustajabisha, yenye kuzingatia matokeo machache na isiyo changamana.

Ndungo na Wafula, (1993), wameelezea maana ya hekaya kuwa ni hadithi ambazo huwa na muhusika mmoja mjanja au mwerevu kuliko wenzake. Amesisitiza kuwa muhusika mkuu hutumia ujanja kujinufaisha kutoka kwa muhusika mwingine.

Mvungi, (2010), ametoa maana ya hekaya kuwa ni hadithi fupi au kisa fulani kinachofikiriwa, si lazima kiwe cha kweli katika maisha. Amesisitiza kuwa hekaya husimuliwa na wazee kwa lengo la kuwaelezea vijana ujanja na ujinga wa baadhi ya watu katika jamii husika. Pia huonyesha jinsi ya kujikwamua kwenye matatizo kwa hivyo hutoa maadili mema.

Kwa jumla mtafiti amesoma vitabu, tasnifu, majarida na mitandao mbalimbali na ameona kuwa ipo nafasi ya kufanya utafiti wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Kazi tangulizi nyingi

zimemsaidia mtafiti katika kumuelekeza namna kazi yake itakavyokuwa kwa mfano tasnifu ya udaktari ya Sengo Unguja na Pemba, imekusanya hadithi 50 ambazo zimechambuliwa katika fani na maudhui ya kifalsafa. Tasnifu hii inaonyesha sanaa jadiya. Kazi hii imempa nafasi mtafiti kufanya utafiti wake wa nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za sekondari Zanzibar. Pili, kazi ya Senkoro, imemsaidia mtafiti katika kujua ukusanyaji na uchambuzi wa data, kazi hii imekusanya hadithi simulizi 35 za Zanzibar. Tasnifu inaonyesha umuhimu wa muhusika katika hadithi simulizi anapofanya safari katika kutatua mgogoro au matatizo yaliyotokezea katika jamii. Tasnifu imempa nafasi mtafiti kufanya utafiti wake. Tasnifu ndogo ya Said na Masoud, zimemsaidia mtafiti katika kujua mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data. Kazi nyengine zimemsaidia mtafiti katika kujua aina mbalimbali za hadithi simulizi ambazo ameweza kuzipata katika jamii ya Kizanzibari.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 MIKABALA YA NADHARIA**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti amezihakiki na kuzielezea nadharia za fasihi simulizi/Fasihi na dhima ya fasihi simulizi kwa jamii ya Waswahili. Lengo la nadharia na dhima zake ni kutiwa katika mawanda na nadharia kwa msomi wa kiwango hiki, pia kutathmini kwa kina na kuona jinsi mtafiti alivyozitumia katika kazi hii.

Mikabala ya nadharia ni misingi madhubuti ya kumuongoza mtafiti jinsi ya kuchambua kazi yake. Utafiti huu una nadharia kumi na nane. Mtafiti ameteua nadharia tano kati ya nadharia zilizotajwa, nadharia ya “Ndani-Nnje”, ”Nadharia ya “Dhima na kazi” na “Nadharia ya fasihi na jamii na nadharia ya muundo.” na nadharia ya hisia. Nadharia nyengine zimemuongoza mtafiti katika kufikia lengo lake la utafiti.

#### **3.2 Nadharia ya Ndani-Nnje**

Hii ni nadharia mpya iliyoasisiwa na Sengo katika miaka ya 1985 na 2009. Neno “ndani-nnje” linaashiria umuhimu wa kuzingatia umbo la ndani na la nnje la kazi ya fasihi. Umbo la ndani ni msukumo wa kazi ya nnje ya kazi ya fasihi inayohusika. Kwa mfano, ndani ya “chungwa”, mnafahamika baada ya mtu kulimenya, kulikatakata, kulila, kuzikuta kokwa na vyengine vya kuliwa ama kutupwa. Mjuzi huyo wa chungwa hata fanana na mshika chungwa, akaliona nnje tu, hajui ladha au harufu. Kadhalika na jamii. Mpita njia na mkaazi hawashindani. Mwenye kuishi na

watu wenyewe, watumiyao maadili yatokanayo na jamii katika muktadha huweza kuishi vyema kuliko mtu mwengine anyepita njia.

Nadharia inabainisha jinsi fani na maudhui yavyotegemeana. Kila kimoja ni muhimu kwa chenzake. Bali licha ya usanii wa kifani, umuhimu wa kazi ya fasihi umo ndani ya maudhui. Ndiyo maana mwananadharia huyo akasisitiza kuwa mhakiki ana wajibu wa kuelewa utamaduni wa jamii anayoihakikikia kazi yake ili aweze kuwa na uchambuzi ulio sahihi na siyo wa kubahatisha.

Nadharia hii imekuwa muhimu sana kwa utafiti huu kwa vile imesaidia sana katika kuichunguza nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za sekondari Visiwani Zanzibar. Maadili ya hadithi simulizi yamo ndani ya dhamira za hadithi. Kwa hivyo, mtafiti ametumia nadharia hii kwa kuzingatia nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar. Nadharia inasisitiza kuuelewa utamaduni wa Wazanzibari, kwa hivyo, mtafiti amelazimika kuuelewa utamaduni wa Wazanzibari kwa kuishi nao na kuhoji mazingira ya kila hadithi. Jambo hilo limempa wepesi wakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data.

### **3.3 Nadharia ya Mkabala wa Kiislamu**

Sengo, Taib na Ngozi, (2005), wanaamini kuwa nadharia hii kwa wanafasihi wa sasa imeonekana kama ni mpya lakini kiuhalisia ipo zamani, nadharia inatokana na imani kuwa tokea binadamu alipoanza kuyakabili mazingira yake kwa kujitengenezea maisha yake ya kila siku. Msingi mkuu wa nadharia hii unatokana na Qur-an na hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W). Nadharia hii inachukulia kuwa msingi wa

kazi ya fasihi ni wa jamii inayohusika, lakini Muumbizi wa zao hili ni Allah (S.W). Kinachosisitizwa katika mkabala huu kuhusu fasihi ni kuwa, kila kitakachofanywa basi kiwe kinamridhisha Allah (S.W); kwa maana ya kuwa kiende sambamba na maamrisha yake, kinyume chake mkabala huo hautathamini fasihi hiyo na haitaacha kuikataza.

Mtafiti ameitumia nadharia hii katika ukusanyaji wa data kwasababu Wazanzibari wengi ni waumini wa Dini ya Kiislamu kwa kuzaliwa na kwa vitendo, kwa hivyo, maadili yao na imani ya Dini ya Kiislamu, Visiwani Zanzibar.

### **3.4 Nadharia ya Saikolojia ya Tiba**

Waasisi wa nadharia ya saikolojia na tabia ni Pavlo, raia wa Urusi na Skinner wa Marekani. Palvo (1957) na Skinner (1971), mwisho walifikia uamuzi kwamba binadamu na mnyama hujifunza vizuri na kwa hamu kubwa sana wanapopewa zawadi kila mara mtu/watu anapofanya jambo zuri. Pia hamu ya kujifunza hupungua au kupotea kabisa wakiachwa kupewa zawadi. Nadharia imemuogoa mtafiti katika kazi ili kuwapa motisha wale walegwa wa utafiti waendeleo kutoa ushirikiano mzuri zaidi.

### **3.5 Nadharia ya Umithilishaji Fasihi (kama sanaa)**

Wafuasi wa nadharia hii huifafanua fasihi kama sanaa yenye umithilishaji. Kwa mtazamo huu, fasihi hufafanuliwa katika uhusiano wake wa maisha, kwa kuiona kama nia ya kujenga tukio au hali fulani ya maisha kwa kutumia mchoro na rangi. Mtazamo huu ambao uliendelezwa na Aristotle (384 B C – 322 B C) na kufuatiliwa na wafuasi wake Abram (1981). Umithilishaji unaiona kazi ya fasihi kuwa na

mfanano na jamii inayokusudiwa kuifikia kwani kufanana huko ndiko kutakakorahisisha namna ya kuihakiki kazi ya fasihi. Nadharia hii imemsaidia mtafiti katika kumithilisha maadili mema yaliyojitokeza katika hadithi na kuangalia nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

### **3.6 Nadharia ya Ushunuzi-Chambuzi**

Nadharia hii imeanza Ufaransa, na imeasisiwa na Adolf (1889-1924) na kutiliwa nguvu na Joung. Msingi wake umejikita katika imani kwamba binadamu wote wana sifa sawa, kwa kuwa wana muundo sawa wa akili. Kwa fikira hiyo basi, wanaitakidi kuwa; matendo ya binadamu yaweza kufanana katika mambo ya kihistoria na kijamii. Adolf alisisitiza hoja hiyo baada ya uchunguzi wake katika tamaduni anuwai za binadamu kuonesha kwamba zina sifa nyingi zinazofanana.

Kila jamii ina utaratibu/mfumo wake wa maisha unaoweza kujitafautisha na ule wa jamii nyengine, basi hapana budi kuwa hata kazi zao za fasihi huwa ni tafauti tafauti, kwani kila utamaduni una kwao, hivyo ni wazi kuwa na kila fasihi ina kwao. Hatuwezi kuichukuwa fasihi ya Marekani na kuifananisha na fasihi ya Zanzibar. Nadharia hii imeweza kumsaidia mtafiti katika kujua aina ya hadithi alizozikusanya katika maeneo tafauti ya kisiwa cha Pemba na Unguja pale zilipofanana. Kwa kutumia nadharia hii, mtafiti ameweza kuchunguza tafauti hizo na kuchanganua dhima zilizoweza kujitokeza.

### **3.7 Nadharia ya Ubadilikaji**

Nadharia hii imetokana na mawazo ya Dorwn (1838). Misingi yake ni sanaa ya usomaji iliyotokana na harakati za ushirikiano, masikilizano na maingiliano ya

binadamu na mazingira yake. Pia wanaitakidi kuwa, katika maisha ya binadamu, ikiwemo sanaa yake, hubadilika kutoka hatua moja hadi nyengine, kadiri wakati unavyobadilika. Nadharia hii imekuwa ni muhimu sana kwa mtafiti kwa sababu ni kweli fasihi simulizi hubadilika katika vipindi tafauti na hadithi alizozikusanya zilionyesha dhima katika wakati tafauti.

### **3.8 Nadharia ya Utamaduni**

Kroeber na Kluckhohn, (1952), walikusanya zaidi ya “maana” 200 za Utamaduni. Kuna mitazamo miwili yenye kutatanisha kuhusu neno hilo, kwamba utamaduni ni yale mambo mazuri pekee yanayojengwa na jamii, ilhali mtazamo mwengine, utamaduni ni kila kitu kilicho kizuri na kibaya kinachotokana na jamii hiyo. Nadharia ya utamaduni hujihusisha na elimu inayohusu asili na maendeleo awali ya binadamu pamoja na elimu ya ishara ambayo huelezea namna ya kujifunza kwa uvumbuzi au kujaribu ujenzi wa utamaduni kisayansi. Nadharia hii hutumika katika kuelezea jambo kama vile sherehe za sikukuu, tamasha mbalimbali, ibada za wazi kama tambiko, hadithi za paukwa pakawa, tenzi, na aina nyengine za masimulizi, mabadiliko ya kiutamaduni, semi mbalimbali, na mambo mengineyo kama runinga, redio, magazeti na majarida, picha zinazobandikwa hadi kuwa filamu na kwa sasa kuna wavupepe. Nadharia hii imemsaidia mtafiti katika kazi hii kwa sababu alilazimika kuzisoma hadithi na kuchunguza mikabala ya maadili mema ya kiutamaduni.

### **3.9 Nadharia ya Kijamii**

Kiini cha nadharia ya kijamii ni shida kuzibainisha, ila mijadala kadha hurejelea kwa Ugiriki ya kale. Harrington, (2005), anaelezea etimolojia ya nadharia ya kijamii.



Nadharia hii inajikita katika misingi mikuu kama vile familia, elimu, dini, urasimu na utabaka hata hivyo kila jamii inayo haya. Kila mojawapo wa misingi hiyo hushughulikiwa kwa kina. Katika msingi wa familia, nadharia hii inachunguza jinsi tafauti zinavyojitokeza kati ya familia na familia za jamii moja, familia za jamii tafauti, na tafauti za jamii hadi jamii. Tafauti hizo zinahusu elimu, ndoa, malezi, imani za kidini, kanuni na miiko ya kijamii. Nadharia ya kijamii imemsaidia mtafiti na imemuongoza katika kuchunguza maadili mema katika mkabala wa elimu, ya dini na familia kwa kila hadithi aliyokusanya kwa wazee, walimu na wanafunzi.

### **3.10 Nadharia ya Fasihi na Jamii**

Nadharia hii inafunganisha fasihi na jamii hasa katika ulimwengu wa tatu. Nadharia hii inaonesha kuwa fasihi ni kielezo cha kazi halisi ya jamii, na inachukuwa kama fikira mojawapo ya kujihami dhidi ya mazingira makali. Nadharia hii inasisitiza kuwa fasihi ni mali ya jamii. Msanii huchukuliwa kuwa ni zao la jamii hivyo, huwa ameilenga hadhira fulani. Wanasosholojia Parsons, (1902-1979), kabla ilihusihwa na Comte (1798-1857), Spencer (1820-1903), na Durkheim.

Katika nadharia hii fasihi ina malengo mawili. La kwanza ni kiwango cha mtu binafsi. La pili ni cha jamii kwa jumla. Kazi nzuri ya sanaa huiathiri nafsi na hadhira yake. Huwa na lengo la kumkomboa mja kutokana na madhila yaliyosababishwa na waja wenziwe au maumbile makali. Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi inapaswa kumsaidia binadamu ajikomboa na apate matumaini maishani. Nadharia imemsaidia mtafiti kujua kuwa hadithi simulizi alizozikusanya zina dhima ya kumkomboa mwanadamu na kufunza maadili mema katika jamii.

### **3.11 Nadharia ya Kimaendeleo (Kimapinduzi)**

Kihara na Dewey, (1859-1952), na Locke (1632-1704), ni wananadharia wa kimapinduzi. Wao wanamini kuwa mtu anapozaliwa tu, ubongo wake huanza kazi ya kuyachambua yale anayoyaona na kuyasikia katika mazingira na kuyapanga akilini mwake katika mpango na maana. Iwapo mambo yatabadilika, basi kiumbe huyo atabadilisha mpango wake wa awali na kuanza kupanga nudhumu mpya, hadi lenye kupangiwa kuingia akilini/maanani. Nadharia hii imekuwa muhimu sana kwa mtafiti na imemsaidia kuona namna wahusika katika hadithi simulizi wanavyobadilika kimawazo, kiakili na kimwili katika kujengeka kimaadili, mwanzo hadi mwisho wa hadithi.

### **3.12 Nadharia ya Msambao**

Kiini cha nadharia hii ni fikra kuwa chochote kinachopatikana kina chanzo chake Rogers, (1931-2004), anasema kuwa kimsingi, nadharia hii ni kwamba fasihi simulizi ina sifa zake, visasili na kadhalika. Visa na hadithi huwa na chanzo au vyanzo vyake maalumu. Vyanzo ni pale hadithi hizo zilipoibuka kabla ya kusambaa na kuenea sehemu mbalimbali.

Nadharia hutumiwa kuweza kuelezea sababu za kuweko mfanano wa sifa za fasihi simulizi kwa jamii mbalimbali. Msambao wa fasihi simulizi unapaliliwa na kuwako kwa tafauti za kihistoria au ukaribu wa jamii fulani. Nadharia hii imemsaidia mtafiti na ameweza kubaini kuwa kwa fasihi simulizi ni mali ya jamii na si rahisi kujua chanzo chake. Hadithi simulizi zina msambao katika jamii na huonekana katika sehemu mbalimbali vya visiwa vya Zanzibar.

### **3.13 Nadharia ya Uaminifu**

Nadharia hii huangalia fasihi simulizi kwa mujibu wa watendakazi wake au uaminifu wake. Parsons, (1902), ameona kuwa kuna mahusiano ya haja za jamii yoyote inayohusika na jinsi mahusiano hayo yanavyozua kuridhika na kudumu kwa mfumo wa jamii fulani.

Mtazamo huu unachukulia kuwako kwa amali au sifa fulani za fasihi simulizi kunatekeleza malengo mahsusi katika jamii hiyo. Fasihi simulizi, kwa mujibu wa nadharia hii inadhamiriwa kuhifadhi na kudumisha amali, maadili na kaida za jamii. Nadharia hii imemsaidia mtafiti kufahamu kuwa baadhi ya wahusika wa hadithi simulizi za Zanzibar wanaonekana katika hadithi nyingi kama vile sungura, simba, fisi, Makame wa Makame, Miza na Mboje.

### **3.14 Nadharia ya Uhalisia**

Nadharia hii ina maana ya uwakilishaji wa uhalisia wa mambo katika kazi ya fasihi. Nayo ilizuka katika karne ya 19 hususan kwa sababu za kupinga mkondo wa utanashati wenye maringo/mikogo/dharau/kedi. Plato (427-347 B.C) na Aristotle (384-322) wanaona kwamba mhalisia huamini katika matokeo ya mambo ya ukweli na anazingatia ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajriba. Kwa hivyo, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matukio yanayoweza hasada za kijamii zilizopo. Mhakiki anaazingatia nadharia hii ya uhalisia huchunguza namna mtunzi anavyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia pamoja na wahusika aliowasawiri katika kuwabebesha matukio na matendo wanayowakilisha kwa jamii inayohusika.

Kwa jumla msanii anatarajiwa kusawiri wahusika na mandhari inayokubalika katika jamii ya wakati wake. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia. Nadharia imemsaidia mtafiti kujua kuwa uhalisia wa fasihi simulizi ni tafauti na fasihi andishi, katika fasihi simulizi wanyama, vitu na vichaka hubeba sifa za kibinadamu.

### **3.15 Nadharia ya Hisia**

Nadharia hii huiangalia fasihi katika uhusiano wake na umma wake, ambapo msisitizo unatiliwa katika mguso unaotolewa na kazi ya fasihi kwa hadhira yake. Kila kazi ya fasihi hulenga kwa njia moja au nyengine, mtu au watu fulani (hadhira) hata kama hadhira hiyo ni nafsi ya mtunzi husika. Finnegan (1970) na Okpewho wanaona kwamba kazi ya fasihi hutoa mguso wa aina fulani kwa hadhira ili ifikirike na kujiuliza maswali au hata kutoa funzo fulani. Aidha kuna nyakati ambapo hadhira hutekwa kabisa na wahusika katika kazi ya fasihi mpaka hadhira hiyo ikajitambulisha na wahusika hao kiasi cha kupoteza utambulishi wao asilia, hata kama ni kwa muda tu.

Nadharia hii imekuwa ni muhimu kwa mtafiti. Mtafiti ameitumia nadharia hii katika kuona jinsi msimuliaji anavyotumia mbinu ya mguso kwa hadhira, na pia hadhira kwa msimuliaji. Pili, kuona jinsi wasimuliwaji wanavyoshiriki kimatendo na jinsi yanavyotoa mguso kataka kujifunza maadili mema.

### **3.16 Nadharia ya Maneno**

Wataalamu wametumia kigezo cha “neno” kama njia ya kutafautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile uchoraji na uchongaji. Aristottle (384-322 B.C) na Abraham

wameona kuwa fasihi ni sanaa inayotumia maneno ili kuwasilisha maudhui na hoja zake. Wanaposema kwamba fasihi ni sanaa inayotumia maneno huwa tayari wameliacha wazi suala kuhusu maneno yaliyoandikwa au kusimuliwa. Neno liwe limeandikwa au limetamkwa, ni neno. Lakini siyo kila neno huenda likaorodheshwa kama fasihi.

Fasihi huwasilishwa kwa maneno lakini maneno hayo hutumiwa kwa njia maalumu ili kuyatenganisha au kuyabainisha na maneno ya kawaida, kwa hivyo ni vyema kuchukulia fasihi sio kama maneno bali kama sanaa itumiayo maneno ya kisanaa au mateule. Na matumizi ya maneno hayo katika fasihi huashiria usanii wa namna fulani. Usanii huo ndiyo unaofanya maneno ya fasihi yawe tafauti na maneno ya kawaida japo mofolojia na fonolojia yake ni sawa. Nadharia imemsaidia mtafiti kujua kuwa fani na maudhui ya hadithi yanategemeana kiusanii, kwa hivyo, kufahamika kwa dhima na maadili ya kazi ya fasihi inategemea kiwango cha kazi ya sanaa kilichojitokeza katika hadithi inayosimuliwa.

### **3.17 Nadharia ya Ubunifu**

Kazi ya fasihi kwa kawaida huwa yamithilisha au kujaribu kuunda upya maisha kwa njia moja au nyengine, ukweli ni kwamba yaliyotungwa si maisha halisi moja kwa moja. Kwa mtazamo wa Jakobson (1896-1982), Shklovsky (1893-1984), na Tomashevsky (1890-1957), wanaona kwamba fasihi si maisha halisi ni tokeo la ubunifu wa mtumzi, yaani mtunzi ana uwezo wa kubuni visa na wahusika wake kwa njia ambayo haikanyagi hali halisi ya maisha ya jamii. Nadharia inasisitiza kwamba mtunzi asikiuke kaida zinazotawala maisha halisi ya jamii. Nadharia imemsaidia mtafiti katika kusikiliza vyema hadithi za fasihi simulizi na kuona ubunifu wa

maisha yaliyojitokeza katika kila hadithi inayosimuliwa na kufahamu vyema dhima na maadili yaliyojitokeza.

### **3.18 Nadharia ya Muundo**

Wataalamu wengi wamejaribu kuzingatia baadhi ya vigezo vinavyoitambulisha fasihi, hasa ikiwekwa katika mkabala mmoja na tanzu nyengine za maisha ya jamii. Dhanna ya ubunifu ni njia nzuri ya kutafautisha fasihi na uhalisia pamoja na ulimwengu halisi. Finnegan (1970), Ferdinand De Saussure, (1957 – 1913) na Okpewho (1992), wanasema kuwa kazi ya fasihi yapaswa kuchukuliwa kama muundo, kama mpangilio maalumu. Kila kazi imepangwa kwa muundo wa hali ya juu na viungo vyake vinategemeana.

Nadharia imemsaidia mtafiti kusikiliza vyema muundo wa kila hadithi iliyosimuliwa au kuisoma kuanzia kianzio cha hadithi, fani na mtiririko mzima uliyojenga maudhui. Pili, kujua vianzio mbalimbali vya hadithi simulizi vilivyojitokeza katika hadithi za jamii ya watu wa Zanzibar.

### **3.19 Nadharia ya Tajriba ya Maisha**

Nadharia hii ni ya kijadi. Njogu na Chimera, (1999), na Rousseau, (1712-1778), wanasema kuwa nadharia hii ndiyo mama wa nadharia zote na ndiyo iliyowahi kumtenga mtu na wanyama wengine wote. Nadharia imejikita na imani kwamba “kuishi kwingi ni kujifunza mengi” siyo kuona mengi tu lakini pia ni kunasa mengi katika bongo za watu na kuchuja na yale yaitwayo maadili. Mwenye uwezo wa kuhifadhi maadili mengi katika ubongo huitwa mwenye busara au mwalimu au

mwanafalsafa. Mwanafalsafa wa dini na imani, au siasa, itikadi wana uwezo wa kuwafundisha watu maadili kwa sababu hukusanya elimu ya muda wa miaka mingi.

Wananadharia wa mtazamo tajriba ya kimaisha wanaona kwamba ili mtoto akue, awe mtu mwema maishani ni lazima ubongo wake mchanga, mkembe, na mtupu upitie mikononi kwa wanafalsafa au fundi aliyeelimika na anayetambulikana barabara, ambaye pia ni mwalimu. Lengo kuu ni kumfundisha mwanafunzi awe na maadili mema anapofikia umri wa kuwa mtu mzima. Nadharia hii imekuwa muhimu kwa mtafiti. Nadharia imemsaidia mtafiti kujua kuwa walimu na wazee ni muhimu katika kufunza maadili mema ya jamii. Hadithi wazisimuliazoo walimu na wazee katika jamii huwa na lengo la kufunza maadili mema kutoka kizazi hadi kizazi kingine.

Kwa jumla nadharia hizi, kila moja ina nafasi yake katika kazi ya mtafiti. Hakuna nadharia ambayo ilijitosheleza katika utafiti huu pekee, ila kunahitajika mshikamano baina ya nadharia moja na nyengine katika kukamilisha kazi hii ya utafiti. Katika kazi hii nadharia hizi zimegawika makundi mawili. Kwanza ni nadharia zilizomuongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data. Pili ni nadharia zilizomuongoza mtafiti katika uchambuzi wa data. Nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data ni nadharia ya ndani nje, mkabala wa kiislamu, fasihi na jamii, ya muundo, na nadharia ya hisia. Nadharia nyingine zimetumika katika ukusanyaji wa data ni nadharia ya Saikolojia ya tiba, umithilishaji, ushunuzi, udadilikaji, ya utamaduni, ya kimaendeleo, ya msambao, ya uaminifu, ya maneno, ya ubunifu, na ya Tarjaba ya Maisha.

## **SURA YA NNE**

### **4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti ameoredhesha mbinu na njia mbalimbali ambazo amezitumia wakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data. Njia ni taratibu zinazotakiwa kufanywa na mtafiti ili kupata jambo unalolitaka. Mbinu ni njia za kupitia kufanya utafiti na kuweza kupata data. Mbinu na njia mbalimbali zimetumika kwa lengo la kukamilisha kazi ya utafiti. Sura imebainisha mfuatano wa matokeo, uteuzi wa walengwa wa utafiti, pahala ulipofanyika utafiti, utaratibu wa ukusanyaji wa data ulivyokuwa na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu.

#### **4.2 Mbinu ya Maktabani**

Mbinu hii ya kusoma maandishi ilimuwezesha mtafiti kusoma vitabu, tasnifu na majarida mbalimbali yenye kuafikiana na mada yake. Mtafiti aliweza kosoma baadhi ya hadithi ambazo alizikuta katika tasnifu, vitabu, majarida na wavupepe. Mtafiti ametumia mbinu ya Maktabani ili kusoma vitabu, majarida na magazeti mbalimbali na kupata kazi tangulizi, kupitia nyaraka mbalimbali zilizohusu mada, kusoma ripoti za tafiti zilizokusanywa, kusoma makala mbalimbali ya fasihi simulizi ambayo yalifanana na mada inayohakikiwa na kupata taarifa ambazo zimemsaidia mtafiti kufikia lengo lake.

#### **4.3 Mbinu ya Kushiriki Darasani**

Mbinu nyengine iliyotumika ni kushiriki darasani ili kumpa nafasi mtafiti kuona hali halisi ya wanafunzi wanavyotolewa hadithi simulizi katika Shule za Sekondari. Pia



mbinu hii imemsaidia kuchunguza matumizi ya mbinu zilizotumika katika ufundishaji wa hadithi simulizi, kusikiliza hadithi zilizosimuliwa darasani au mitaani na kubaini faida na hasara zitokanazo na hadithi hizo. Mtafiti ameweza kuona uhalisia wa matendo yatokanayo na msimuliaji, wasikilizaji wa hadithi simulizi na kupata data sahihi. Mbinu hii pia imemsaidia mtafiti kuteua walimu ambao amewapa hojaji zake za utafiti. Kwa jumla mtafiti ametumia mbinu shirikishi katika utafiti huu ili kusikiliza, kuona hali halisi ya matendo yatokanayo na hadithi, kukusanya na kuchunguza aina mbalimbali za hadithi simulizi darasani au nje ya darasa na mitaani. Mbinu hii imemsaidia mtafiti kufikia lengo lake.

#### **4.4 Mbinu ya Mahojiano**

Mbinu ya mahojiano imetumika katika utafiti huu ili kupata data za moja kwa moja zilizomuwesha mtafiti kupata data sahihi kutoka kwa wazee, wanafunzi na walimu na baadaye kuyaweka katika maandishi. Pia mbinu hii imeambatana na kanda za kurikodia sauti ili kuhakikisha kuwa hadithi inaandikwa kama ilivyosimuliwa. Mbinu hii imemuwezesha mtafiti kukutana ana kwa ana na walimu na wanafunzi ambao walikuwa na uwezo mzuri wa kujieleza na kujua faida na hasara zitokanazo na nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili shule za sekondari Visiwani Zanzibar. Mbinu hii pia imetumika mitaani kwa wazee ambao wamekuwa hawawezi kujieleza kwa njia ya maandishi, aidha mtafiti alitumia mbinu hii kwa wazee ambao wamemsimulia hadithi simulizi na kuzinukuu na baadaye alizihakiki ili kupata data alizozitaka. Kwa jumla mtafiti ametumia njia ya mahojiano kwa kuwauliza maswali walengwa na kupata data kwa wasioweza kujieleza kwa maandishi na kuzirikodi hadithi simulizi na baadaye ameziweka katika maandishi kama zilivyosimuliwa.

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano ili kupata ufafanuzi zaidi kwa hadithi simulizi alizozikusanya na baadaye kuzihakiki kwa makini na kupata data sahihi kutoka kwa wazee, wanafunzi na walimu. Pia njia hii ilimsaidia mtafiti kupata mawazo na maelekezo yenye kufaa kutoka kwa wazee, wanafunzi na walimu mbalimbali. Mtafiti aliitumia mbinu ya mahojiano ili kuwa karibu zaidi na walegwa wa utafiti na alijenga mahusiano ya karibu yaliyomuezesha mtafiti kupata ufafanuzi wa kina kwa kila hadithi ambayo alihitaji ufafanuzi zaidi kwa watu wenye uwezo wa kujieleza. Pia kupata ufafanuzi wa vianzio vya hadithi simulizi.

#### **4.5 Mbinu ya Kutumia Maswali ya Ana kwa Ana**

Mbinu ya maswali ya ana kwa ana imetumika katika utafiti na watafitiwa waliweza kujibu maswali bila ya woga au hofu kwa hivyo wameweza kujibu kulingana na ufahamu wao. Mbinu hii ameitumia mtafiti kwa watafitiwa ambao haikuwa rahisi kwao kutoa data kwa njia ya majadiliano. Mtafiti alitumia mbinu hii ili kupata data za uhakika na kwa haraka kwa kuwateuwa wasaidizi maalumu wa somo la Kiswahili kila shule ya Sekondari ya Zanzibar ambao walimsaidia kusimamia kujazwa hojaji hizo hata hivyo baadhi ya hojaji zilichelewa kufika kutoka kwa wasaidizi hao. Kwa jumla mtafiti ametumia njia ya mahojiano katika utafiti kwa sababu alitayarisha hojaji zilizolenga kwa watafitiwa na waliweza kujibu bila ya hofu kulingana na ufahamu wao.

#### **4.6 Mbinu ya Kuwa na Mtafiti Msaidizi**

Mtafiti alilazimika kuwa na mtafiti msaidizi. Kuna sababu mbalimbali zilizomfanya mtafiti kuwa na mtafiti msaidizi. Kwanza, Tumbatu watu wengi wanapenda

kuzungumza lahaja ya Kitumbatu kwa hivyo, mtafiti msaidizi anafahamu Kitumbatu na Kiswahili fasaha. Hali ili imesaidia kufanikisha kazi ya utafiti. Pili, mtafiti msaidizi amehitajika katika mitaa mbalimbali ili kuwajua wazee ambao mtafiti amewahitajia. Ilikuwa ni vigumu kwa mtafiti pekee kuwajua wazee wa mitaa aliyoitafiti na walikoishi. Pili, kutokana na utamaduni wa Wazanzibari ni vyema mgeni anapoingia katika mtaa kuwa na mwenyeji ili aeleweke na watu kwanza ndipo afanye utafiti wake. Tatu, baadhi ya watafitiwa walikuwa hawapendi kurekodiwa lakini kutokana na jitihada za mtafiti msaidizi na walimu wa shule za Sekondari zilizokuwa zinafanyiwa utafiti waliweza kukubali. Kwa jumla mtafiti msaidizi amekuwa ni muhimu sana katika utafiti huu kutokana na sababu za kitaalimu na kiutamaduni wa Kizanzibari.

#### **4.7 Pahala pa Utafiti**

Utafiti huu umefanyika katika baadhi ya maeneo ya Visiwa vya Zanzibar. Mtafiti alianzia Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI), Shule za Sekondari za Mkoa wa Mjini-Magharibi, kisha alikwenda Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwa upande wa Pemba, mtafiti alianzia Mkoa wa Kaskazini na mwisho Mkoa wa Kusini. Mtafiti aliziteua Shule zilizomo katika maeneo hayo kwasababu zinafundisha somo la Kiswahili fasihi ingawa ziko shule nyengine zinazofundisha somo la Kiswahili.

#### **4.8 Uteuzi wa Watafitiwa**

Uteuzi wa watafitiwa ulizigatia kiwango kilicho bora. Kila Mkoa una Wilaya mbili Mtafiti ameteua Wilaya moja katika kila Mkoa. Wilaya mbili za Unguja ambazo ni Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Kaskazini ‘A’. Pemba ni Wilaya ya Wete na

Wilaya ya Mkoani. Wilaya ya Mjini mtafiti ameteua shule nne za Sekondari na Wilaya ya Kaskazini ni shule ya Tumbatu. Aidha mtafiti ameteua kila shule walimu wawili, wanafunzi kumi wanume na wanafunzi kumi wanawake. Kila mtaa mtafiti ameteua wazee watano wanawake na watano wanaume.

**Jedwali Na. 4.1: Watafitiwa wa Pemba**

| SKULI                   | Wanafunzi wanawake | Wanafunzi wanaume | Walimu   | Wazee wanaume | Wazee wanawake |
|-------------------------|--------------------|-------------------|----------|---------------|----------------|
| 1.KIZIMBANI             | 8                  | 8                 | 2        | 3             | 3              |
| 2.UTAANI                | 8                  | 8                 | 2        | 3             | 3              |
| 3.MITIULAYA             | 8                  | 8                 | 2        | 2             | 4              |
| 4.MICHENZANI (CHOKOCHO) | 8                  | 8                 | 2        | 4             | 4              |
| <b>JUMLA</b>            | <b>32</b>          | <b>32</b>         | <b>8</b> | <b>12</b>     | <b>14</b>      |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Kizimbani, Utaani, Mitiulaya na Michenzani (2011)**

**Jedwali Na. 4.2: Watafitiwa wa Unguja**

| SKULI             | Wanafunzi wanawake | Wanafunzi wanaume | Walimu    | Wazee wanaume | Wazee wanawake |
|-------------------|--------------------|-------------------|-----------|---------------|----------------|
| 1.TAKILUKI        | 10                 | 10                | 2         | 4             | 4              |
| 2.BEMBELLA        | 10                 | 10                | 2         | 4             | 4              |
| 3.BUBUBU          | 10                 | 10                | 2         | 4             | 4              |
| 4.HAILESALLA SSIE | 10                 | 10                | 2         | 4             | 5              |
| 5.TUMBATU         | 9                  | 9                 | 2         | 4             | 4              |
| <b>JUMLA</b>      | <b>49</b>          | <b>49</b>         | <b>10</b> | <b>20</b>     | <b>21</b>      |

**Chanzo: Takiluki, Shule ya Sekondari ya Bembella, Bububu, Hailesalassie na Tumbatu (2011)**

Jumla ya walimu wote = 18

Jumla ya wanafunzi wote = 162

Jumla ya wazee wote = 67

**Jumla ya walengwa wote wa utafiti = 247**

#### **4.9 Ukusanyaji wa Data**

Data zimekusanywa kulingana na utaratibu uliobuniwa na mtafiti. Mtafiti alifika katika maeneo ya shule za Sekondari akiwa na vifaa vyake na kukutana na watafitiwa baada ya kujitambulisha kwa mwalimu Mkuu wa kila Shule iliyohusika na utafiti. Katika sehemu nyengine mtafiti alifuatana na mtafiti msaidizi katika ukusanyaji wa data shuleni na maskanini.

#### **4.10 Vifaa vya Utafiti**

Vifaa vilivyotumika katika utafiti ni karatasi za maswali ya hojaji, karatasi nyengine zimetumika kwa kuwapa wanafunzi waandike hadithi simulizi wanazozijua, kaseti na kamera zimetumika. Vifaa hivi vyote vimemsaidia mtafiti kuchambua data vizuri zile zinazohitajika.

#### **4.11 Uchambuzi wa Data**

Uchambuzi wa data umefuata hatua mbalimbali kama zifutazo:

Kwanza, kuzisoma hadithi zote na kuchagua hadithi za vigano, sogu na ngano na baadaye kuziweka kulingana na mikabala yake. Pili, kuchambua dhima na maadili mema yatokanayo na kila kikundi cha hadithi simulizi zilizokusanywa kuanzia hadithi za vigano, sogu na ngano kulingana na mkabala uliojitokeza. Aidha mtafiti ametumia mfumo wa namba na njia ya jadewali katika kufanikisha kazi hiyo. Tatu, uchambuzi kuhusu hojaji za wanafunzi, walimu na wazee zilizokusanywa katika maeneo ya utafiti kwa kutumia mbinu ya kiwango na mbinu ya ujumla. Nne, uchambuzi wa vianzio vya hadithi simulizi na ufafanuzi wake.

## SURA YA TANO

### 5.0 UCHAMBUZI WA DATA

#### 5.1 Utangulizi

Sura hii imezingatia uchambuzi wa hadithi simulizi zilizokusanywa kutoka shuleni na maskanini. Jumla ya hadithi 61, zimechambuliwa kwa kuzingatia Kiswahili fasaha. Hadithi hizi zimekusanywa kutoka Mkoa wa Mjini-Unguja, Wilaya ya Kaskazini A, Wilaya ya Wete-Pemba na Wilaya ya Kusini –Pemba. Hadithi 21 ni za Vigano, hadithi 27 ni za Soga na hadithi 13 ni za Ngano. Uchambuzi wa hadithi hizi umezingatia mfumo wa namba, hadithi 1-21 ni hadithi za vigano, 22 - 48 ni hadithi za soga na hadithi 49 - 61 ni hadithi za ngano. (Ziko katika kiambatanishi.)

Utafiti umezichunguza hadithi hizo na kuona nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Mtafiti ametoa maana ya dhanna ya maadili. Kwa mfano, kamusi ya Kiswahili Sanifu inaelezea kuwa maadili ni tabia, hulka au mazoea ya usawa, haki na uadilifu. Au funzo linalopatikana kutokana na hadithi, mkasa au kadhia.

Kwa mujibu wa Bi Asha Muhene, katika Dini ya Kiislamu maadili yamegawika katika miaka saba saba (7:7:7). Katika kipindi cha miaka 7 ya mwanzo, mtoto hufunzwa maadili yanayohusu kuwajua watu wa karibu na familia yake, kucheza na wenzake vizuri na umuhimu wa kufanya kazi ndogo ndogo zilizopo nyumbani. Huu ndiyo msingi wa mwanzo wa maadili ya mtoto wa Kizanzibari.

Miaka 7 ya kipindi cha pili, mtoto ameshakuwa mkubwa, anafundishwa maadili ya dini, kusali, kuheshimu wakubwa wake, kusoma, kuvaa mavazi ya kiheshima.

Katika kipindi cha miaka 7 ya tatu, mtoto anafunzwa maadili ya utu uzima, ya kujielewa na kujitambua, kufanya kazi za kijitegemea na kuwajua vyema watu wa ukoo wake. Utafiti umeonyesha kuwa hadithi ni utanzu unaopendwa sana na watoto na watu wazima na unaofunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari. Kwa hivyo, hadithi hufunza maadili katika jamii ya watu wa Zanzibari wa rika na mazingira tafauti.

Katika utamaduni wa Wazanzibari, ziko hadithi wanazozisimulia wazee kwa kuanzia na “paukwa ....pakawa” na baadaye ikafuatia methali yenye kutoa taswira ya lile jambo litakalosimuliwa ikiwa ni baya au zuri. Hadithi kama hizo ni nyingi katika jamii. Utafiti umebaini kuwa wazee wa Kiswahili hupedelea sana methali katika matumizi mbalimbali. Kwa hivyo hadithi kama utanzu unaofunza maadili hujitokeza kuwa na methali katika kianzio cha hadithi au ndani ya hadithi au mwisho wa hadithi. Aidha, mtafiti amebaini kuwa kuna hadithi ambazo zinaanza na “paukwa ...pakawa”, kinafuta kisa na kumalizia na” wakaishi raha mustarehe”.

Wazanzibari wana utamaduni wa kukaa maskanini au kwenye baraza, hapo watu hunywa kahawa au kupumzika. Sehemu kama hizo hupatikana sana hadithi za sogha ambazo huchanganyika na utani au ucheshi ndani yake. Utafiti umebaini kuwa anayefanya hivyo huwa na lengo la kufunza maadili zaidi kuliko kuchekesha. Mtafiti alikuwa amechunguza nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za sekondari Visiwani Zanzibar.

## **5.2 Dhanna ya Hadithi Simulizi**

Hadithi simulizi ni miongoni mwa tanzu za Fasihi Simulizi. Tanzu hii ina vitawi vyake mbali mbali kama vile sogha, visasili, ngano, vigano, hekaya na tarehi na

kumbukumbu. Hadithi simulizi hutegemea utamaduni wa jamii husika. Hivyo, kila jamii ina fasihi yake kulingana na mazingira, wakati na maadili yaliyokusudiwa kufuatwa na jamii hiyo. Hadithi simulizi Visiwani, zimeanza zamani sana. Simulizi hizo, aghalabu, husimuliwa wakati wa usiku kwa njia ya kuwafanya watoto wasilale mapema ili wapate chakula cha usiku.

### **5.3 Sifa za Hadithi Simulizi**

Hadithi Simulizi ni hadithi ambazo husimulia habari katika mtiririko wa aina maalumu wenye sifa zifuatazo:

- (i) Huelezea tokeo au matokeo katika mtiririko maalumu.
- (ii) Huwa na wahusika watendaji katika matokeo yanayosimuliwa.
- (iii) Hutumia lugha ya kimaielezo. Lugha hiyo wakati mwengine na mazungumzo.
- (iv) Utambaji au utoaji wake huambatana na vitendo na ishara.

### **5.4 Dhana ya Maadili Mema**

Kiango na wenzake, wanasema katika kamusi ya Kiswahili sanifu kuwa maadili ni funzo linalopatikana kutokana na hadithi, mkasa au kadhia. Tafsiri hii inatuongoza katika mambo mawili ya kimsingi. Kwanza, maadili yanaweza kupatikana kwa kusoma au kisikiliza hadithi. Kuisikiliza hadithi na kuifamu unajifunza maadili yatakayokuongoza kuishi vyema katika familia au jamii yako.

Mtafiti alipokuwa akifanya utafiti katika Shule mbalimbali za Sekondari na kuwauliza walimu, walimueleza kuwa wanafunzi wanajifunza maadili mbalimbali katika hadithi zisimuliwazo darasani au nyumbani kwao. Maadili wanayojifunza humuongoza mwanafunzi kufikia lengo ambalo mwalimu au mzazi amekusudia kwa



watoto wake. Aidha walisisitiza kuwa kwa kutumia hadithi simulizi maadili yanafika haraka kwa walengwa. Pili katika tafsiri hiyo ni kwamba maadili yanaweza kupatikana katika mkasa. Mkasa ni jambo ambalo limetokea katika mtaa, kwa mtu au jamii. Mkasa au mikasa hutoa maadili ambayo mtu au watu huweza kujifunza. Mtafiti aliulizia iwapo katika Shule za Sekondari hutokea mikasa. Jibu ni kweli, shuleni hutokea mikasa kama vile majumbani. Maadili yanayotokana na mikasa huweza kufunza wanafunzi kufanya vyema masomo yao. Maadili kwa wasemavyo Khamisi Akida na wenzake katika kamusi ya Kiswahili Sanifu kuwa ni onyo au mafundisho yatolewayo kwa njia ya hadithi au shairi na yenye nia ya kufundisha au kutoa mafundisho mazuri. Tafsiri hii ilimuongaza mtafiti katika mambo mawili ya kimsingi. Kwanza ni kuelewa kuwa maadili ni onyo au fundisho ambalo humfuza mtu kuishi katika jamii yake katika mwelekeo unaotakiwa. Pindipo akiukiuka, anaweza kuharibikiwa au kutengwa na jamii inayohusika. Mtafiti alipouliza katika Shule kuwa yanakuwepo maonyo au mafundisho ambayo wanafunzi huweza kujifunza, jibu ni kweli kuwa yako maonyo au mafundisho mbalimbali ambayo wanafunzi huyapata ama, kwa wanafunzi wanaoendelea au wale waliomaliza masomo. Kutokana na hivyo, wanafunzi huweza kuendelea vyema masomo yao. Walimu walisisitiza kuwa wale watakaodharau onyo hilo huweza kuharibikiwa, inaweza kuwa pale pale shuleni au wakiwa nje ya Shule.

Pili, maadili yanapatikana kwa kusikilza shairi. Shairi la fasihi simulizi linaposomwa, wasikilizaji hupata maadili papo kwa papo. Shairi la fasihi simulizi linaweza kuenea kwa haraka sana katika jamii, kwa hivyo, maadili husambaa kwa haraka. Mtafiti aliwauliza walegwa wa utafiti katika maeneo yao kuwa iwapo

ushairi wa fasihi simulizi unasaidia kuenea kwa maadili. Jibu ni ndiyo. Aidha walisisitiza kuwa wakati wa sasa hivi, shairi la fasihi simulizi (wimbo) linaosikilizwa kwenye radio, runinga n.k maadili yake huenea kwenye jamii kwa haraka. Utafiti umeonesha kuwa hadithi hufunza maadili mema wanafunzi katika Shule, mitaani au majumbani. Maadili hayo yamegawanyika katika mikabala tafauti.

Hadithi simulizi zinazosimuliwa katika Shule, majumbani na maskanini huwa zinafunza maadili maalumu yanayokusudiwa katika jamii hiyo. Mtafiti alielezwa na walengwa kuwa jamii hukusudia kufunza jambo fulani kwenye kikundi cha watoto, wanafunzi au watu wazima, kwa hivyo kwa kutumia hadithi huwa na nafasi kubwa katika kufunza maadili hasa katika jamii ya Zanzibar.

### **5.5 Mgawanyo wa Hadithi Simulizi za Vigano. Katika Kufunza Maadili mema**

Vigano ni hadithi fupi fupi ambazo zinasimuliwa kwa mifano na mara nyingi hutumia methali kama lugha ya ishara katika kufunza maadili kwa wasikilizaji wake. Kwa mfano, kigano kinaweza kuelezea kuhusu mzazi aliyempenda mno mwanawe wa pekee hivyo hakuweza kumkemea au kumrudi na hatimaye mtoto na mzazi wake hufikwa na matokeo mabaya katika maisha yao. Kwa mfano “Mchelea mwana kulia mwisho hulia yeye”. Kwa hivyo, baada ya msimuliaji kuanza na kianzio cha hadithi, cha “paukwa.....pakawa” inafutia methali na baadaye kuaza hadithi yenyewe.

Mvungi, T.A (2010), anasema kuwa kigano ni usimulizi wenye kisa kimoja unaoadilisha watoto na vijana. Aidha kigano kinaweza kusimulia mtu mvivu na hatimaye akamalizia na njaa. Amesisitiza kuwa mwishowe msimulizi huwaasa

wasikilizaji kwa kutumia aina fulani ya methali. Kwa hivyo, wakati mwengine methali huonekana katika hadithi simulizi, mwanzo au mwisho wa hadithi baada ya msimuliaji kusimulia kisa chenyewe.

Hadithi za vigano zimegawanyika katika mikabala ifutayo katika kufunza maadili kwa Wazanzibari:

1. Hadithi zenye kufunza maadili ya makuzi ya mtoto, wema na ubaya.
2. Hadithi zenye kufunza maadili ya elimu, umoja na ushirikiano.
3. Hadithi zenye kufunza maadili ya ndoa na starehe.

**Jedwali Na. 5.1: Hadithi zenye kufunza maadili ya makuzi ya mtoto, wema na ubaya**

| Namba | Jina la hadithi              |
|-------|------------------------------|
| 1.    | Mtu na mwanawe               |
| 2.    | Miza, Mboje na wazee wake    |
| 3.    | Furaha                       |
| 4.    | Bi kizee na mjukuu wake      |
| 5     | Fisi adhibiwa.               |
| 6.    | Tajiri na Masikini.          |
| 7.    | Watoto wa tajiri na maskini. |
| 8.    | Fisi, chui na sungura.       |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Bububu ( 2011)**

### **5.5.1 Hadithi ya Mtu na Mwanawe**

Hadithi inafunza jamii ya Wazanzibari kuwatii wazazi wao katika kutekeleza mambo mema ambayo yatawaletea maendeleo katika familia zao. Maadili hayo yanawakilishwa na kile kitendo cha mtoto alipoambiwa na mama yake kuwa kipindi cha mvua kimekaribia kwa hivyo atowe mpunga na akauanike lakini mtoto akasema

kuwa atauanika kesho. Siku ya pili ilipofika ikanyesha mvua kubwa sana. Hii ikawa ni chanzo cha kukosa chakula kwa wiki nzima kwa mtoto na mama yake. Aidha hadithi inasisitiza kuwa mama na mtoto wake, wameweza kuweka chakula cha akiba katika maisha yao. Huu ulikuwa mpunga ambao haukuanikwa. Hali hiyo ilisababisha mama kumwambia mtoto wake auanike au wataula mbichi. Jamii ya Wazanzibari inafunzwa maadili kuwa ni vyema unapoweka akiba iweze kukusaidia wakati wowote wa shida bila ya masharti. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili kwa jamii ya wazanzibari umuhimu wa malezi bora na kujiwekea akiba. Watoto wasikilize kuwatii kwa kutekeleza wanayoambiwa na wazazi wao.

### **5.5.2 Hadithi ya Mize, Mboja na Wazazi**

Hadithi inasimulia mtoto aliyekuwa akilelewa na mama wa kambu. Mama huyo akawa anamtesa sana. Hadithi hii inafunza maadili jamii ya Wazanzibari kuwa si vyema kuwabagua watoto. Maadili hayo yana wakilishwa na kitendo cha mamaake Miza kwenda kunini na alipofika porini akachimba shimo na kumtumbukiza. Mama yake alipofika nyumbani akasema hamjui alipo. Hiki ni kitendo kibaya katika jamii yao.

Pili, hadithi inafunza maadili kwa jamii ya kina baba kuwa ni vyema wanapoondoka nyumbani na kwenda safari, wanaporudi wafuatilie mwenendo au taarifa za watoto wao waliowaacha majumbani kwao. Wakumbuke kuwa baadhi ya wake zao wanaweza kuwatendea mambo mabaya watoto wao. Kitendo hiki kinawakilishwa na mama yake Mize alipokwenda kunini na kumchimbua shimo. Aliporudi alisema kuwa hajui Miza alipo. Hiki ni kitendo kibaya na si vyema kukifuata katika jamii ya Wanzanzibari.

Tatu, hadithi inafunza maadili ya watoto wawe na tabia ya kucheza pamoja na kupendana kwa hivyo, ikiwa mzazi alifanya uovu na kuonekana na mtoto, huweza kufichua uovu huo. Kitendo hiki kinawakilishwa na Mboja alipokwenda porini na kuimba wimbo uliomjulisha baba yao amefika na kuwaletea zawadi, moja yake na moja ya Miza. Kuokolewa kwa Mboja, kulirejesha utulivu katika familia lakini aibu ikamfika mama yao. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii ya Wazanzibari kama vile kutowabaguwa watoto katika familia, kuwatafutia zawadi watoto wote, mzee anaporudi safari ni vyema kufuatilia taarifa za familia yake. Hadithi ina nafasi ya kufunza wazee kuacha tabia mbaya ya kuwaondosha watoto wasiowapenda na kuwapeleka mahala ambapo wanaweza kupoteza maisha yao.

### **5.5.3 Hadithi ya Furaha**

Hadithi hii inafunza maadili jamii ya Wazanzibari kuwa wanapokuwa na watoto ambao ni wanafunzi si vyema wakajishughulisha na mambo ya anasa, ikiwa ni mtoto wa kike au kiume. Maadili hayo yanawakilishwa na kitendo cha Furaha, ambaye alikuwa ni mwanafunzi aliyejishughulisha na starehe na kuacha kushughulikia masomo yake. Mwisho alipata uja uzito, akafukuzwa shule, nyumbani kwao na pia alipokwenda kwa mwanamme aliyempa uja uzito alimfukuza. Furaha alitanga tanga na mtoto wake wa kike na mwisho alifariki na mtoto wake wa kike. Pili, hadithi inafunza maadili kuwa, asiyefunzwa na mamaye basi hufunzwa na ulimwengu. Furaha alikosa kujifunza maadili mema nyumbani kwao. Alipofunzwa na wanakijiji aliwakatalia, hatimaye ulimwengu ulimfundisha yeye na mtoto wake wa kike. Wote wawili walifariki. Maadili haya yanawakilishwa na kitendo cha Furaha baada ya kupata uja uzito alianza kufukuzwa shule, kwao na hatimaye kwa mwanamme

aliyempa ujauzito. Wazanzibari wanaadilishwa kuwa katika kutafuta elimu ni vyema kutojishughulisha na vishawishi vya anasa au mapenzi. Si vyema kwa mwanafunzi kujiingiza katika anasa kwasababu hataweza kufaulu masomo yake vizuri. Jamii inajifunza maadili kuwa mtoto si wa mtu mmoja, ila ni wa jamii. Kwa hivyo anapotenda jambo jema huwa ni la jamii na ikiwa baya hasara itakayopatikana huwa ya jamii nzima. Kitendo cha Furaha kufariki dunia na mtoto wake wa kike ni hasara kwa kijiji chao. Na pia kitendo cha kijana wa kiume aliyempa ujauzito na kumfukuza ni hasara kwa jamii nzima. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa wanatakiwa kushirikiana katika kuishi maisha mazuri. Kuwaelimisha watoto wao kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Anayetafuta elimu hatakiwi kujishughulisha na mapenzi. Wazazi wawaelimishe watoto wao elimu ya jinsia ili kujiepusha na vishawishi vya wanaume. Wazee wasiwe na hasira za kuwafukuza watoto wao wanapokosea ila wawaelimishe wajue makosa yao.

#### **5.5.4 Bi Kizee na Mjuku Wake**

Hadithi hii inafunza maadili kuwa jamii kuwa baadhi ya bibi wanapowalea wajukuu wao, wanawapenda kupita mpaka, hatimaye kila jambo analolitaka mjuku kwa bibi yake hufanyiwa. Mwisho mjuku hukua na kujifunza maadili yasiyokubalika katika jamii ya Kizanzibari. Kitendo cha Bi kizee kukaa na mjuku wake na kila analolifanya mjuku akawa hana makosa, kinadhihirisha kuwa mjuku huyo alijifunza maadili yasiyokubalika na jamii. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii ya Wazanzibari katika kuwatanabaisha jinsi baadhi ya akina bibi wanavyowalea wajukuu wao malezi mabaya. Wajue kuwa, mchelea mwana kulia,

mwisho hulia yeye. Mtoto umleavyo ndivyo akuwavyo na udongo upatize ungali maji.

#### **5.5.5 Hadithi ya Fisi Adhibiwa**

Hadithi hii inafunza maadili jamii ya Wazanzibari kuwa kuna watu wema na watu wabaya. Baadhi ya watu wanatumia nguvu zao kuwatendea ubaya wale wanyonge.

Kitendo cha wanyama wadogo waliokutana siri kujadili uovu wa fisi kinadhihirisha uovu wa wanyama wakubwa kuwatendea maovu wanyama wadogo wadogo. Pili, kitendo cha wanyama wadogo wadogo kufanya mkutano kwa siri kinadhihirisha kwamba umoja ni nguvu. Kwa hivyo hadithi inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa wanapooa wanafanyiwa maovu na baadhi ya viongozi wao ni vyema kufanya mikutano ya siri na kujadili matatizo yao ili kupata ufumbuzi. Kitendo cha Sungura kuomba muda wa siku saba, kimeweza kumuondosha Fisi aliyekuwa tishio katika jamii. Kwa hivyo, hadithi inafunza maadili mazuri kwa jamii, kwani kila chenye mwanzo hakikosi kuwa na mwisho.

Tatu, hadithi inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa wasiwe na tamaa kupita mipaka. Aidha wasiwe na maamuzi ya pupa au haraka haraka yatakayowaletea madhara. Kitendo cha fisi kumrukia Sungura mara baada ya kufungua mlango, kinaonyesha pupa au tamaa ya kupata nyama. Wazanzibari wanakumbushwa jinsi ya kukabiliana na jamii ya watu wenye kutaka kuwadhuru au kupoteza maisha yao. Wazanzibari wanatakiwa kujifunza hekima na maadili mazuri yatakayowaletea ukombozi na kuondosha unyonge katika nchi yao. Nne, hadithi inawafunza maadili Wazanzibari kuwa jamii nyengine za Afrika Mashariki, zina

maadili yake katika kumpokea mgeni na kumkarimu. Ikiwa ni mgeni mbaya au mzuri ni vyema kujifunza misingi iliyowekwa ili kuleta ukombozi. Kitendo cha Sungura kilichotokea nyumbani kwake cha kumuonyesha fisi nyama mbalimbali ambazo zilitakiwa kuliwa kwa misingi ya kimaadili ya utamaduni wa kisungura, ilikuwa silaha ya kumuondosha fisi katika jamii ya wanyama wadogo wadogo. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii ya Wazanzibari kuwa viongozi wasiwadhulumu ndugu zao. Wazanzibari waache tabia ya kuwa na tamaa kupita mpaka, wakumbuke kuwa maadui wako katika jamii, ni vyema kuwatenga au kuwaondosha kabisa. Na wakati wengine wanalazimika kujitolea muhanga ili kuondosha matatizo.

#### **5.5.6 Hadithi ya Tajiri na Masikini**

Hadithi hii inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa atakayemfanyia mwenzake ubaya na yeye hafi duniani bila ya kumfika yale aliyomtendea mwenzake. Maadili haya yanawakilishwa na kitendo cha masikini aliyeonekana na tajiri nyumbani kwake akila mkate kwa kutoelea harufu ya nyama inayotoka katika nyumba ya tajiri. Masikini alimshukuru tajiri kwa ubinadamu wake kwa sababu imekuwa ni mazoea kwenda nyumbani kwa tajiri kula mkate na kutolea harufu ya mchuzi kutoka nyumbani kwa tajiri. Tajiri alimgeukia masikini na kumwambia kuwa tabia hiyo ndiyo iliyosababisha kuwa anapokula chakula huwa havina ladha. Masikini alishitakiwa na ikabidi alimpe Tajiri shilingi ishirini. Masikini hakuwa na fedha za kumlipa kwa siku hiyo mahakamani. Baada ya kesi, jaji alimfuata Masikini nnje ya mahakama na kumpa shilingi ishirini kwa masharti kuwa aende nyumbani kwa tajiri na akaiangushe itowe sauti. Masikini aliogopa lakini mwisho



alikuwenda. Alipoiangusha, Jaji alikuwepo na alimtaka tajiri achukuwe mlio wa shilingi ishirini, tajiri akashindwa. Pili, hadithi hii inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa wanapokuwa mitaani wajuwe kuwa kuna masikini na matajiri. Matajiri wawasaidie masikini ili waishi katika maisha mazuri au kula vyakula vizuri kama matajiri. Kitendo cha masikini kwenda nyumbani kwa tajiri kula mkate na kutoelea harufu nzuri ya vyakula vinavyotoka kwa tajiri, kinafunza maadili jamii ya wazanzibari kuwa kuna masikini wasioweza kutimiza hata chakula cha mlo mmoja kwa siku. Tatu, hadithi hii inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa wakumbuke kuwa siyo matajiri wote wanaimani ya kuwasaidia masikini. Kuna baadhi ya matajiri ambao huwadhalilisha masikini. Kitendo cha masikini kuonekana na tajiri nyumbani pake akiwa anakula mkate kwa kutoelea harufu ya vyakula vitokavyo kwa tajiri, kilisababisha masikini kushitakiwa mahakamani na kulipa shilingi ishirini lakini wakili aliweza kumpa masikini shilingi ishirini na kutaka akaiangushe chini na itowe sauti nyumbani kwa tajiri ili tajiri aokote mlio wa pesa. Tajiri jambo hilo lilimshinda. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii ya Wazanzibari kuwa matajiri wawasaidie masikini katika mitaa yao wanayoishi. Wakifanya hivyo, Mwenyezi Mungu atawaongezea baraka. Kinyume chake ni mfarakano katika jamii. Dharau haifai katika maisha yao ya kila siku. Mwisho, Masikini na yeye anaweza kumdhalilisha tajiri hata ikiwa ni mbele ya vyombo vya Sheria, kwa hivyo, wanajamii waheshimiane.

#### **5.5.7 Hadithi ya Watoto wa Tajiri na Masikini**

Hadithi ya watoto wa Tajiri na masikini inatoa maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa watoto wanapenda kucheza na watu mbalimbali bila ya kujali ubinafsi au

ukabila. Watoto wa bi Tajiri walikuwa na tabia ya kupita kwa mzee masikini wakati wakirudi chuoni. Mzee masikini aliwatolea hadithi kuwa “mtenda wema hutendea nafsi yake na mtenda uovu humrejea mwenyewe”. Kitendo hiki cha watoto wa Bi tajiri kupita kwa masikini kilimkera sana mama yao. Siku moja aliandaa chakula Bi tajiri na kutia sumu. Alimpelekea masikini kwa lengo la kumuua. Watoto wa bi Tajiri walipopita kwa mzee masikini walitolewa hadithi na baadaye wakupewa kila mmoja kipande cha mkate ambao ulitoka kwa bi tajiri. Punde walipofika kwao watoto walianza kuanguka. Walipelekwa hospitali na kuonekana kuwa wamekula chakula chenye sumu. Baada ya uchunguzi wa mfalme, aligundua kuwa ni mkewe aliyepika mkate na kuutia sumu na kupeleka kwa mzee masikini.

Pili, hadithi inafunza maadili kwa jamii ya wazanzibari kuwa ukimuelekezea mwenzako kidole kimoja, basi ujuwe kuwa vidole vitatu vimekuelekea wewe mwenyewe. Chuki aliyokuwanayo bi tajiri na kutaka kumuua mzee masikini, ilimrejea mwenyewe baada ya kupeleka mkate wenye sumu ambao bila ya kutarajia walipewa watoto wake waliporejea chuoni na hatimaye kuanguka walipofika kwao. Tatu, hadithi inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa panapotokeya jambo ni vyema pakafanyika uchunguzi. Watoto wa bi tajiri walipofika kwao walianguka, wakapelekwa hospitali. Baada ya uchunguzi wa daktari walionekana kuwa wamekula chakula chenye sumu. Kitendo hiki baada ya uchunguzi wa polisi kulijulikana kuwa ni mkate aliopika mama yao ambapo aliupeleka kwa mzee masikini kwa lengo la kumuua. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii ya wazanzibari kuwa wasiwe na roho mbaya na waishi vizuri katika jamii yao. Wawe na moyo wa kusaidiana na kupendana. Wazanzibari na watoto wao wanapoumwa wapelekwe hospitali kwa uchunguzi zaidi wa afya zao.

### **5.5.8 Hadithi ya Fisi, Chui na Sungura**

Hadithi ya Fisi, Chui na Sungura inafunza maadili kwa Wazanzibari kuwa binadamu wanatabia ya kufanyiana uadui. Kwa hivyo, ni vyema kukaa kwa tahadhari. Na mtu anapoona dalili za kuangamizwa, ni vizuri akajiepusha kwanza. Ubaya ukiendelea inafaa muuonewa akamuangamiza adui yake haraka sana na kuhakikisha kuwa adui harejei tena. Kitendo, cha Fisi na Chui kutamani kumla Sungura na wanyama wengine wadogo kinathibitisha kuwa jamii ilikuwa na uonevu. Siku moja wanyama waliweka mkutano kuwaua Fisi, Simba na Chui. Uamuzi ulifikiwa lakini utekelezaji wake ulikuwa ni “nani atafanya kazi hiyo? “Sungura alijitokeza. Sungura alifanya ujanja na kumueleza Fisi kuwa nyumbani kwao kuna nyama nyingi ya karamu. Fisi aliingia tamaa kwenda nyumani kwa Sungura. Walikuta moto na jiwe moja kubwa lililopata moto na kugeuka rangi nyekundu. Fisi alikubali kuwa ile ni nyama, na alitakiwa alishwe kimila (tambiko).

Sungura alikula jiwe na lilimuunguza kifua na tumbo, hatimaye akafariki. Kwa hivyo, Fisi aliuliwa na Sungura. Pili, hadithi hii inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa maadui wako katika jamii yao, wanaishi nao lakini ni vyema kupambana nao mmoja baada ya mmoja. Katika hadithi hii, Sungura na wanyama wengine wadogo, wamefanikiwa kumuuwa Fisi lakini bado yuko Chui na Simba. Kunahitajika mbinu nyengine bora zaidi ili kuwaondosha Simba na Chui. Kwa hivyo, maadui katika jamii haweshi. Kila siku huzuka wapya. Chui na simba wako katika jamii ya Wazanzibari. Wazanzibari hawako na wasiwe tayari kuliwa mmoja mmoja au vikundi. Tatu, hadithi hii inafunza maadili kwa jamii ya Wanzanzibari kuwa wasifanye papara wala tamaa katika kutekeleza maamuzi yao. Kitendo cha

Fisi kumrukia Sungura kwa hafla na kujenga tamaa kuwa amepata chakula kilimfanya Sungura kuona kuwa kifo kipo karibu naye kwa hivyo akafanya mbinu ili amuuwe Fisi. Sungura alimpeleka Fisi kwake kwa ujanja na hatimaye akamuua Fisi. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa wenye nguvu wasichukuwe madaraka ya kuwadhulumu wanyonge katika jamii. Wazanzibari wakishirikiana, wakubwa na wadogo, maadui hawatapata nafasi ya kuwadhulumu vitu au mali zao, wakumbuke methali isemayo umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

**Jedwali Na. 5.2: Hadithi zenye kufunza maadili ya elimu, umoja na ushirikiano**

| Namba | Jina la hadithi                  |
|-------|----------------------------------|
| 9.    | Sikuzani na Majaliwa             |
| 10.   | Asma abeba ujauzito wa Hassan    |
| 11.   | Mwanampate na Nyangoro           |
| 12.   | Kurwa na Doto                    |
| 13.   | Adili na Amali                   |
| 14.   | Mtoto aliyetumwa kwa Mfalme      |
| 15.   | Viungo vilivyokataa kufanya kazi |
| 16.   | Nyuki aliyekimbia wenzake        |
| 17.   | Simba, Chui na kiwaviwavi        |

**Chanzo: Shule ya Sekondari Utaani (2011)**

**5.2.9 Hadithi ya Sikudhani na Majaliwa**

Hadithi ya Sikudhani na Majaliwa inafunza jamii kuwa wanafunzi wanapopewa ushauri na walimu wao katika shule ni vyema kuufanyia kazi ili wafanikiwe katika maisha. Hadithi inaeleza kuwa Sikudhani na Majaliwa walikuwa wanafunzi wa darasa la kumi na mbili. Mwalimu wao aliwapa ushauri kuwa mwenye kutafuta

elimu lazima afanye juhudi bila ya kujali muda. Majaliwa alifuata ushauri wa mwalimu wake akafaulu na Sikudhani aliupuuza ushauri, hakufaulu. Pili, hadithi inafunza kuwa wanafunzi wanapotafuta elimu ni vyema wasishughulike na mambo mengine ambayo yataharibu masomo yao. Majaliwa na Sikudhani walikuwa wanafunzi wa darasa la kumi na mbili. Sikudhani alijishughulisha na mambo ya starehe badala ya masomo. Majaliwa alitumia muda wake katika kutafuta elimu. Majaliwa alifaulu na Sikudhani hakufaulu. Kwa hivyo, katika kutafuta elimu Wazanzibari wasishughulike na mambo mengine. Tatu, hadithi inafunza kuwa ni vyema wanafunzi kushirikiana katika kudurusu masomo yao ili wafanye vizuri mitihani yao. Hadithi inaeleza kuwa Majaliwa na Sikudhani walikuwa wakishirikiana katika masomo yao lakini baadaye Sikudhani alianza tabia ya kutoshirikiana na wanafunzi wenzake. Kitendo cha Sikuzani kujiingiza katika starehe kilisababisha kutofaulu mtihani wake wa mwisho wa mwaka. Kwa hivyo, ni vyema wajenge ushirikiano katika masomo. Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Hadithi inafunza kuwa anayetafuta elimu ni lazima ajitahidi. Utafutaji wa elimu unahitaji muda wa kutosha kwa msomaji. Mwisho wanafunzi ni lazima wawe na muda wa kutosha wa kudurusu masomo yao na kujenga ushirikiano wa pamoja darasani.

#### **5.2.10 Hadithi ya Asma Abeba Ujauzito wa Hassan**

Hadithi ya Asma abeba ujauzito wa Hassan, inaifunza jamii kuwa mtaka yote hukosa yote. Asma ni kijana aliypewa huduma mbali mbali na wazazi wake ili asome na baadaye awasaidie wazazi wake. Alipofika Shule, alihadaiwa na mwanafunzi mwenzake aliyeitwa Hassan, Asma aliacha masomo akajiingiza katika dimbwi la

starehe na hatimaye kubeba ujauzito. Alipomueleza Hassan alikataa na kumwambia asimfate fate. Mama yake Asma aliposikia habari hiyo, alishtuka sana, alikumbuka kuwa mtoto wake wa kike kasha baleghe, alipaswa kumpeleka kwa nyanya wake akafundwe, baba yake alikataa sana kumfunza nyumbani. Alishikwa sikio, kweli kipya ni kinyemi lakini kovu zisingeumbwa. Pili, vijana wanakumbushwa kuwa wawasikilize wazazi na watu wazima wao. Haraka haraka haina baraka. Tatu, hadithi inafunza kuwa wanapokuwa wanafunzi, wasiwe na haraka ya kujiingiza katika maisha. Kitendo cha Asma kujiingiza katika dimbwi la starehe kulimsababisha kupata ujauzito na kufukuzwa shule. Asma alichangia kifo cha mama yake. Mwisho alifukuzwa nyumbani na baba yake. Mtaka yote hukosa yote. Hadithi imepata nafasi ya kufunza kuwa wanafunzi wa Kizanzibari wasijiingize kwenye starehe wanapokuwa shuleni, wafuate ushauri wa wazee wao na wajiepushe na vikundi vinavyojali anasa kuliko masomo.

#### **5.2.11 Hadithi ya Mwanampate na Nyangoro**

Hadithi ya Mwanampate na Nyangoro inafunza jamii kuwa shuleni ni pahala pa kutafuta elimu na siyo mapenzi. Kila mwanafunzi anatakiwa asome na atimize malengo yake ya kitaalimu na kimaisha. Kitendo cha Mwanampate aliyekuwa mwanafunzi wa kidato cha sita kusaidiana kimasomo na Nyangoro, kilijenga msingi wa starehe zaidi kuliko kimasomo. Mwanampate na Nyangoro waliahidiana kuoana baada ya kumaliza masomo yao, Mwanampate alihadaika na kijana mwengine na hatimaye akapata ujauzito na kufukuzwa Shule. Pili, hadithi inafunza kuwa kuna mapenzi ya kweli na mapenzi ya udanganyifu, ni vyema wakajifunza mapenzi ya kweli na uadilifu. Katika hadithi Mwanampate na Nyangoro

walipendana na kuahidiana kuwa wanandoa baada ya kumaliza masomo yao. Haya yalikuwa mapenzi ya kweli na uadilifu ingawa wote walikuwa wanafunzi wa darasa moja. Baada ya muda, Mwanampate alishawishika na kijana mwengine wa kitajiri, akapata ujauzito na akafukuzwa shule. Kijana aliyempa ujauzito akamfukuza. Kitendo hicho cha udanganyifu kikasababisha kwa Mwanampate kuichukia shule, na kijana aliyempa ujauzito wa mapenzi ya udanganyifu. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii ya Kizanzibari kuwa shuleni ni pahala pa masomo na sio pahala pa kufanya starehe. Wanafunzi waepukane na vishawishi vya starehe ya udanganyifu. Wakumbuke methali inayosema “mkataa pema pabaya panamwita.”.

#### **5.2.12 Hadithi ya Kurwa na Doto**

Hadithi ya Kurwa na Doto inafunza jamii kuwa ndugu waliozaliwa tumbo moja ni vyema kushirikiana katika maisha ili wafanikiwe. Kurwa na Doto walikuwa ndugu waliopendana, wote walijishughulisha na masomo yao. Doto alionekana kutojishughulisha na masomo yake lakini dada yake, alimshauri kuendela na masomo. Wote walimaliza shule vizuri. Doto akawa daktari na Kurwa akawa mwalimu. Kwa hivyo, Wazanzibari wanatakiwa watilie mkazo elimu ya ualimu na tiba katika jamii. Pili, hadithi inafunza kuwa mgaa gaa na upwa hali chakula kitupu.

Doto alitaka kukatisha masomo yake lakini Kurwa alimsisitiza. Mwisho wakamaliza vizuri. Wote wawili walipata ajira ya ualimu na udaktari katika kijiji chao. Hadithi ina nafasi ya kufunza kuwa wazee wawapeleke watoto wao shule ili wapate elimu. Wazanzibari wanapopata matazizo katika shule wasikate tamaa wakarudi nyumbani, ila iwe sababu ya kuendelea mbele. Wanapomaliza masomo watafute ajira katika nchi yao. Mwisho wakumbuke kuwa umoja ni nguvu katika jamii.

### **5.2.13 Hadithi ya Adili na Amali**

Hadithi hii inafunza kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kitendo cha Adili na Amali kwenda msituni wakagombana na baadaye kila mmoja aliamua kutafuta embe zake peke yake. Hali hii ilionyesha kuwa hakuna umoja baina yao. Kitendo hicho alikigundua babu yao. Lakini baada ya kufika nyumbani, babu yao alimpa kila mtu vijiti viwili na kumuamuru avivunje, wakashindwa, lakini baadaye akawapa kila mtu kimoja na wakaweza kuvivunja.

Pili, hadithi inafunza kuwa wanajamii washirikiane pamoja. Wawe na umoja. Kitendo cha Adili na Amali kugombana na ikawa kila mmoja anaokota embe zake porini, kuliwapa nafasi vijana wengine waliokuja kuokota embe porini na hatimaye Amali akaumia. Hekima alizotumia babu yao kuwapa vijiti viwili wavivunje lakini wakashindwa, kimewafunza maadili mema kwa jamii ya Wazanzibari kuwa umoja na ushirikiano ni muhimu katika maisha. Jamii ya Wazanzibari inajifunza maadili mema juu ya ulezi wa watoto ambao watakuwa kizazi cha baadaye. Kitendo cha mzee Juma kuishi na kuwapenda wajukuu wake na kutatua migogoro. Kinadhihirisha kufunza maadili wajukuu wake. Hadithi ina nafasi ya kufunza maadili jamii kuwa ndugu wa damu moja huwa hawapigani, hushikamana na kusaidiana katika maisha yao. Wakumbuke methali isemayo kuwa vikombe vikikaa pamoja haviachi kugongana seuze watoto wa binadamu.

### **5.2.14 Hadithi ya Mtoto Aliyetumwa kwa Mfalme**

Hadithi ya mtoto aliyetumwa kwa mfalme inaifunza jamii kuwa katika maisha kuna masikini na tajiri. Masikini na mtoto wake na tajiri na mali yake. Kitendo cha



masikini kuumwa na kumtuma mwanawe akamwite mfalme kinaonesha jinsi masikini anavyoweza kusaidiwa na mwanawe. Pamoja na umasikini wao, mtoto alipokosa huduma kwa mfalme alikwenda kutafuta tiba sehemu nyengine na kufanikiwa. Pili, hadithi inafunza wanajamii kuwa wasidharauliane na watembeleane ili kujenga udugu na umoja. Masikini na mwanawe baada ya muda wa siku nyingi waliweza kujikimu kimaisha. Hata hivyo walisema wakamtembelee Tajiri kwa vile siku nyingi zimepita. Pamoja na wema na ukarimu huo, Mfalme aliwafukuza maskini na mtoto wake. Tajiri aliona kuwa masikini na mtoto wake wamekwenda kumuomba. Kwa upande mwingine, mfalme aliumwa na alihangaika sana kutafuta dawa, mwishowe ilibidi afike nyumbani kwa masikini na mwanawe. Walikaribishwa vyema na akahudumiwa kwa kila kitu. Mwishowe mfalme aliomba radhi.

Hadithi inafunza kuwa maradhi hayachagui maskini au tajiri. Kwa hivyo ni vyema kutafuta dawa. Masikini alipoumwa alimwambia mwanawe akamtafutiye dawa, alihangaika na mwishowe akapata. Tajiri naye alipoumwa alitafuta dawa kila sehemu akashindwa lakini baadaye akatibiwa na masikini na mwanawe kwa hivyo maradhi hayachagui tajiri au masikini. Nne, hadithi inafunza kuwa panapotokezea ugomvi, watu hawanabudi kusameheyana na kuombana radhi. Tajiri alikuwa anamuona masikini kuwa kila siku anakwenda kumuomba mpaka ikawa hamfungulii tena mlango kwa shida yoyote ile. Masikini na mwanawe walipoona tajiri amewadharau kwa shida zao, walianza kutafuta njia nyengine za kujisaidia. Mwisho, tajiri alipata maradhi na ikabidi afike nyumbani kwa masikini na mwanawe. Tajiri aliomba radhi na alimtaka masikini na mwanawe wamsamehe. Hadithi

imefunza kuwa wanajamii wasidharauliane, wasibaguane na wapendane ili wawe na maisha mazuri.

#### **5.2.15 Hadithi ya Viungo Vilivyokataa Kufanya Kazi**

Hadithi ya Viungo vilivyokataa kufanya kazi inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa kuna mambo katika jamii, kabla ya mtu kuamua jambo ni lazima afikirie madhara yake. Kitendo cha mguu kufanya pupa la kugoma kwenda kuchukua chakula cha tumbo, kiliungwa mkono na mkono, meno kutotafuna, ulimi kutoviringa na kulainisha chakua na kukipeleka tumboni. Tumbo ingawa lilipata nafuu ya kupumzika, lilikaa kimya kwa muda na kufikiri. Baada ya muda mfupi, viungo vyote viivyogoma vilianza kulegea. Tumbo likaviuliza viungo, “je munaona sasa na nyinyi munaanza kulegea?” Tushirikiane faida ni yetu sote.

Pili, hadithi inafunza kuwa ushirikiano ni muhimu katika maisha. Bila ya ushirikiano, hakuna maendeleo. Pia sehemu moja inapoathirika na nyengine itafuatia. Kitendo cha mguu kugoma kwenda kuchukua chakula, mikono iliunga mkono, ulimi na meno bila ya kufikiria athari zake. Baada ya muda mchache, viungo vyote vilianza kulegea, kutokuwa na kuishiwa nguvu kwa tumbo kusita kufanya kazi. Viungo hivyo havikufikiria mwanzoni kuwa ikiwa tumbo halifanyi kazi na wao hawatafanikiwa, kwa hivyo, ushirikiano ni muhimu katika jamii. Wazanzibari wanapoona wenzao wamegoma, wasiunge mkono migomo ila kwanza wafikiri madhara yake. Sio kila mgomo una faida. Hadithi ina nafasi kwamba, watu wanapotaka kufanya jambo ni lazima kwanza wafikiri kabla ya kutenda jambo lenyewe ili wasije wakupata hasara. Ushirikiano katika kutenda jambo ni muhimu

sana kwa sababu mtu peke yake hawezi kukamilisha mambo yote ni lazima apate wasaidizi.

#### **5.2.16 Hadithi ya Nyuki Aliyekimbia Wenzake**

Hadithi ya Nyuki aliyekimbia wenzake inafunza watu kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kitendo cha nyuki aliyekuwa akifanya kazi na wenzake kutengeneza sega la asali, akaamua kuwakimbia wenzake kwa sababu aliona kazi anayoifanya ni kubwa na ujira wake ni mdogo. Alipokimbia alipata matatizo na alifahamu kuwa kazi ya kufanya watu wengi ni vigumu kuifanya mtu mmoja. Kwa hivyo alirejea kwao. Alishirikiana na wenzake.

Hadithi inafunza watu kuwa ni vyema mtu kufanya kazi na jamii yake au kwao kuliko kujitenga au kwenda kufanya kazi nchi za jirani. Kufanya kazi na jamii yako ni vizuri. Wazanzibari wajifunze kuwa wazalendo. Pili, hadithi inafunza watu kuwa wafanye kazi kwa bidii ili wapate maendeleo. Kila mfanyakazi afanye kazi kulingana na ujuzi na maarifa yake. Kitendo cha nyuki kufanya kazi kwa mgawanyo kimesababisha kupata chakula cha kutosha na kujiwekea akiba siku za masika au shida. Tatu, hadithi inafunza watu kuwa kazi ndiyo uti wa mgongo na maendeleo. Kitendo cha nyuki kukaa pamoja na kufanya kazi kimeweza kuonyesha matunda ya umoja wao katika kazi.

Alipoamua kuwahama nyuki wenzake, aligundua kuwa kazi imekuwa ngumu mno, kwa hivyo, nyuki aliporejea kwao alifanya kazi kama kawaida. Hadithi inafunza watu kuwa majungu na fitina ndiyo adui wa maendeleo. Kitendo cha nyuki aliyekuwa akifanya kazi na wenzake, aliona kwamba anategewa na anapata manufaa

kidogo. Alihama na akapata tabu. Aliporejea aliona kazi inaendelea kama kawaida. Kwa hivyo, majungu na fitina yanarejesha nyuma maendeleo ya kijamii. Waliomshawishi atoroke, hawakutoroka. Walikuwa wanafanya kazi kama kawaida. Hadithi ina nafasi ya kufunza watu kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Wazanzibari wafanye kazi kwa bidii na waepukane na majungu.

#### **5.2.17 Hadithi ya Simba, Chui na Kiwaviwavi**

Chui alitoka katika nyumba yake na kuacha mlango wake wazi. Aliporudi aliukuta mlango wake umefungwa na kiwaviwavi ameshaingia ndani. Chui bila ya kujua ni nani aliyefanya vile alitoa amri mlango ufunguliwe lakini akashindwa. Akaja simba, akatoa amri mlango ufunguliwe, lakini naye akashindwa. Akatoka chura akatoa amri lakini akaambiwa ndani kuna jini bahari na anatoka bahari ya saba, na yuko tayari kuangamiza Simba, Chui na anayehodisha. Chura akajibu yeye ni jini wa bahari na anatoka bahari ya ishirini na saba. Atamuangamiza aliyemo ndani na atakuwa jivu.

Hadithi inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa nguvu pekee hazitumiki ila papatikane hekima na busara. Chui alitoka katika nyumba yake na kuacha mlango wake wazi. Aliporudi aliukuta mlango wake umefungwa na kiwaviwavi ameshaingia ndani. Chui bila ya kujua ni nani aliyefanya vile alitoa amri mlango ufunguliwe lakini akashindwa. Akaja simba, akatoa amri mlango ufunguliwe, lakini naye akashindwa. Akatoka chura akatoa amri lakini akaambiwa ndani kuna jini bahari na anatoka bahari ya saba, na yuko tayari kuangamiza Simba, Chui na anayehodisha. Kusikia hivyo, kiwaviwavi alitoka na wanyama wote, simba, chui na chura walishangaa. Pili, hadithi inazindua jamii kuwa si vyema mtu unapoondoka nyumbani kwake kuwacha mlango wazi. Akiwacha mlango wazi, humjui ni nani

atakayeingia. Kwa hivyo, anayeingia ndani si rahisi kutoka ila waswahili husema “ndaro udume” na akushindaye kwa tonge mshinde kwa kutoeya. Hadithi hii inafunza watu kuwa katika ulimwengu kuna watu au mataifa makubwa na mataifa madogo lakini si vyema kuliogopa taifa kubwa kwa nguvu zake. Jambo la muhimu ni kutumia maarifa na uzoefu wa kimaisha.

**Jedwali Na. 5.3: Hadithi zenye kufunza maadili ya ndoa na starehe**

| Namba | Jina la hadithi                    |
|-------|------------------------------------|
| 18.   | Mtoto mzuri kuwashinda wote.       |
| 19.   | Uvumilivu wa bi Asha               |
| 20.   | Sungura na chura.                  |
| 21.   | Bwana Massoud na wake zake wawili. |

**Chanzo: Takiluki (2011)**

**5.3.18 Mtoto mzuri Kushinda Wenzake**

Hadithi inasimulia kitendo cha kuwachagua wachumba waliokuja nyumbani kwa baba yake “mtoto mzuri” wakakataliwa kwasababu walikuwa ni masikini. Hadithi hii inafunza jamii kuwa watoto wa kike wakishavunja ungo (ukubwa) ni vyema wapewa mume, ili waepukane na aibu, wasije wakapata matatizo ya kuwa na mimba kabla ya kuolewa. Kitendo cha kuwachagua wachumba waliokuja nyumbani kwa baba yake “mtoto mzuri” wakakataliwa kwasababu walikuwa ni masikini. Pili, hadithi hii inafunza maadili kwa wazee wa kiume kuwa si vyema kuchagua mchumba ili apate utajiri. Mapenzi hayachaguwi tajiri au masikini, ila ni makubaliano ya wanandoa. Kitendo alichokifanya baba yake “mtoto mzuri” alichagua wachumba. Alitaka apate mchumba tajiri, hatimaye mtoto wake akapata uja uzito kabla ya kuolewa. Tatu, hadithi inafunza watoto wa kike kwa wakati wa

sasa hivi wanakosa wachumba wa kuwaoa. Wajihadhari na kubeba ujauzito wa mitaani. Kitendo cha mtoto wa kike kupata ujauzito mitaani, baadaye akaamua kutafuta dawa za kutoa ujauzito huo hatimaye asifanikiwe na akafa, chatosha kuwa ni fundisho na onyo kwa utovu huo wa dini na maadili. Ni kitendo cha aibu sana kwa jamii inayojigamba kwamba ni ya kiislamu. Hadithi inatanabaisha swala zima la uzingatiifu wa kuanzia uchumba hadi ndoa. Ushauri na uteuzi ufanywe kwa makini. Vijana wadogo hawana uwezo huo ndio maana umri, tajriba na uadilifu vina umuhimu wake katika swala la ndoa, lakini mtoto akililia wembe apewe. Hao vijana wa kizazi kipya, kwa upya wao usiokuwa na wazazi wakitaka yao, wachiwe kheri nusu shari kuliko shari kamili.

### **5.3.19 Hadithi ya Uvumilivu wa Bi Asha**

Hadithi ya kuoa mke mwengine siyo kosa, mtu anaweza kuoa wake hadi wanne kulingana na imani ya dini ya Kiislamu lakini anatakiwa kutoa huduma sawa kwa wake zake wote. Asipoweza kuwahudumia ni matatizo. Kitendo cha mume wake bi Asha aliyeamua kuoa wake wengine wawili na kushindwa kumpa huduma bi Asha kama inavyotakiwa, alimtesa mke na mtoto wake. Pili, hadithi inafunza kuwa mstahamilivu hula mbivu. Baada ya mume wa Bi Asha, kuowa wake wengine alistahamili na mtoto wake. Mwisho wake wapya walioolewa waliachwa mmoja mmoja. Kitendo cha mume wa Bi Asha kukaa na wake zake kwa muda wa mwaka mmoja na mwisho aliamua kuwaacha mmoja baada ya mwengine kutokana na kushindwa kuwahudumia.

Tatu, hadithi inafunza kuwa mwenda tenzi na omo hurejea ngamani. Si vizuri kumzarau mtu aliyeanza maisha naye tokea zamani kwa sababu amepata mtu

mwengine mpya. Kitendo cha Bi Asha kukaa kimya baada ya mume wake kuoa wake wengine kwa miaka mine bila ya huduma. Mwisho, mumewe akarejea tena na kuanza maisha mapya na Bi Asha. Hadithi inahimiza waliooana na walioolewa kuwa na tabia njema. Pili, mke wa mwanzo anatakiwa awe mstahamilivu na mvumilivu katika maisha yake na mumewe, mwisho, mume asimuache mke wake nyumbani bila ya huduma.

### **5.3.20 Hadithi ya Sungura na Chura**

Hadithi ya Sungura na Chura inafunza kuwa ni vyema kuwa na marafiki lakini kila mmoja anawajibu wa kutunza siri za rafiki yake. Kuzitoa siri za rafiki yake zinaweza kukuletea maafa yeye na rafiki yake. Pili, hadithi hii inafunza kuwa marafiki wawili kuheshimiana. Kitendo cha Sungura kumuona chura ni sawa na mwanamke, ndiyo chanzo cha ungomvi baina yao na hatimaye kutoleana siri zao. Tatu, Wazanzibari wanatakiwa wasiwe na tabia ya wizi. Hadithi inaelezea kuwa ilifikia wakati Sungura na Chura walikuwa na barua ya ushenga. Njiani waliiba ndizi, na nyengine wakazificha.

Sungura na Chura waliwatafuta na mtoto wa binaadamu aliweza kuigundua siri hii na wakakamatwa. Wazanzibari wanatakiwa kupeleka madai na malalamiko katika sehemu zinazohusika. Ni vyema kupata wawakilishi mahiri na wenye uwezo wa kubuni na kufikiri kwa kina. Wakipeleka malalamiko katika sehemu zisizo husika watapata matatizo wao na vizazi vyao. Kitendo cha Sungura na chura kwenda kwa binadamu kupeleka barua ya malalamiko kuwa binaadamu wanawala “wanyama pori”, kwa hivyo, waache tabia hiyo, kilileta athari kwa wanyama mbele ya

binadamu. Wizi hauna faida katika jamii, kila mtu anatakiwa ajitegemee. Pili, hakuna siri ya watu wawili hapa duniani. Mwisho jamii inatakiwa ijuwe kuwa udhaniaye ndiye kumbe siye hasa katika dunia ya leo, kwa hivyo kila mtu awe na tahadhari katika maisha na rafiki yake.

### **5.3.21 Hadithi ya Bwana Massoud na Wake Zake Wawili**

Hadithi inasimulia kuwa Bwana Massoud alimpiga mke mkubwa hadi akafa kwasababu alichuma mbaazi bila ya ruhusa. Jambo hili halikuwa la kweli, aliyechuma mbaazi alikuwa ni mke mdogo lakini maganda alikwenda kuyaweka nyumbani kwa mke mkubwa akijua kuwa mume wake atakasirika na kumpiga. Hadithi ya Bwana Massoud na wake zake wawili inafunza kwamba wanapokuwa na wake wawili au zaidi wasiwe na tabia ya hasira na uamuzi wa haraka. Bwana Massoud alimpiga mke mkubwa hadi akafa kwa sababu alichuma mbaazi bila ya ruhusa. Jambo hili halikuwa la kweli, aliyechuma mbaazi alikuwa ni mke mdogo lakini maganda alikwenda kuyaweka nyumbani kwa mke mkubwa akijua kuwa mume wake atakasirika na kumpiga. Pili, hadithi inafunza maadili kwa Wazanzibari wanawake na wanaume kuwa wivu ni hatari na unaweza kusababisha kifo/vifo.

Bwana Massoud alipojaribu kuchunguza safari ya mke mdogo kwenye makaburi aligundua kuwa wimbo aliouimba alionyesha kuwa, mke mdogo ndiye aliyechuma mbaazi. Kwa hivyo bwana Massoud alimkamata mkewe, akampiga na kumuumiza sana. Tatu, hadithi inafunza kuwa si vyema kumpiga mke wake hadi kumuumiza. Dini hairuhusu kipigo kama hicho. Bwana Massoud alimpiga mke wake wa kwanza, na wa pili na kuwaua. Kwa hivyo hata huyo wa tatu aliyemuoa anaweza kumpiga



na kumuwa pindipo akifanya makosa. Nne, hadithi inafunza maadili kuwa watoto wanavyolelewa ndivyo wanavyokuwa katika jamii. Ingawa wake wa Bwana Massoud walikuwa na wivu baina yao, lakini watoto walikuwa wakipendana na kucheza pamoja. Kwa hivyo, hadithi hii inafunza maadili ya kuwalea watoto vizuri hata ikiwa wazazi wao ni tafauti.

Hadithi inafunza jamii ya wanaume kuwa wawe na uadilifu katika ndoa zao. Bwana Massoud alikuwa na wake wawili, mke mkubwa na mke mdogo, kila mmoja akiwa na mtoto mmoja lakini, mke mdogo alikuwa ndiye kipenzi zaidi kwa Bwana Massoud. Kitendo hiki ndicho kilichojenga chuki na wivu na kusababisha kifo cha mke mkubwa na hatimaye mke mdogo. Sita, hadithi inawafundisha wanajamii wote kuwa mazoea yanatabu ukishazoea kuwa na mke ni vigumu kukaa ujane. Kwa hivyo, ni vyema kuwa na mke, na kuishi naye kwa salama, atunze watoto na mali za mume. Hadithi inafunza jamii kuwa atakayefanyia watu ubaya na watu wanaweza kukumfanyia ubaya hapa hapa duniani. Mwenyezi Mungu anampenda mtu mwenye kusubiri. Pili, wale wenye wake, wajenge uvumilivu na wajiepushe na hasira za haraka haraka. Tatu, wivu na choyo ni vitu vibaya na Wazanzibari hawanabudi kijiepusha nao. Mwisho, wawe waadilifu katika ndowa na malezi mazuri kwa watoto wao.

Soga ni hadithi ndogo ndogo ambazo zinaambatana na utani ambao huchanganyika na uchekeaji kwa wasikilizaji. Katika hadithi ya soga hujitokeza tokeo ambalo huweza kuonyesha kubeza, kukejeli au kuzarau. Hali hiyo ndiyo inayopelekea hadhira kupata kicheko au burudani. Soga huambatana na utani. Huweko maadili muhimu ndani yake kwa jamii husika.

Mgawanyo wa hadithi za sogu katika mikabala ifuatayo:

1. Hadithi zenye kufunza maadili ya uongozi na biashara
2. Hadithi zenye kufunza maadili ya urafiki, dini na imani.
3. Hadithi zenye kufunza maadili ya mapenzi na tabia njema

#### **5.4.22 Hadithi ya Bwana Ali Kapewa Cheo**

Hadithi ya Bwana Ali amepewa cheo inaifunza jamii kuwa cheo ni dhamana unapokuwa kazini na unaweza kuondoshwa ukapelekwa pahala pengine wakati wowote. Hadithi inaelezea kuwa Bwana Ali alipopandishwa cheo, alipita mitaani kutangaza cheo chake, kugawa pesa ovyo ovyo akiwa amelewa. Kitendo hiki kilisababisha shirika lake kufilisika na baadhi ya watendaji wake kutolewa kazini, akiwaomo Bwana Ali. Hadithi inafunza maadili kwa wanajamii kuwa hairuhusiwi kunywa pombe. Au mtu kutumia madaraka yake vibaya akiwa kazini. Pili hadithi inatoa elimu kuwa mtu anapopata kazi akumbuke kuweka akiba kabla ya kuacha kazi ili mafao yake yamsaidiye.

#### **Jedwali Na. 5.4: Hadithi zenye kufunza Maadili ya uongozi na biashara**

| <b>Namba</b> | <b>Jina la hadithi</b>       |
|--------------|------------------------------|
| 22           | Bwana Ali kapanda cheo.      |
| 23.          | Kiongozi aliyefungua kisima. |
| 24.          | Bunuasi na Mfalme.           |
| 25.          | Majaaliwa                    |
| 26.          | Majuha wanne wasiojuwana.    |
| 27           | Dereva wa gari.              |
| 28.          | Sungura na fisi.             |
| 29.          | Mla Matonge.                 |
| 30.          | Mtepe uliosheheni.           |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Tumbatu na Takiluki (2011)**

#### **5.4.23 Hadithi ya Kiongozi Aliyefungua Kisima**

Hadithi ya kiongozi aliyefungua kisima inaifunza jamii kuwa baadhi ya Viongozi wanapofika katika shughuli, yanatokezea mambo wasiyoyatarajia, ambayo ni mabaya kwao na jamii. Hadithi inaelezea kuwa kiongozi alifungua kisima. Kiongozi alipofika kwenye kisima alikitazama ndani ya maji na baadaye akawauiza wananchi kuwa wanafuga mamba au la. Wananchi walijibu kuwa hawafugi mamba ila ni sura ya kiongozi wao. Hii ilikuwa ni kejeli iliyotokezea katika kisima hiki. Kwa hivyo, hadithi inafunza maadili kwa Wazanzibari kuwa ni vyema mtu kujua analolitamka kusema hadharani ili lisilete karaha mtaani. Wakumbuke msemu usemao kheri kujikwaa kidole kuliko kujikwaa ulimi. Kwa jumla hadithi ina nafasi ya kufunza wanajamii kuwa wasipende kuuliza kila wanachokiona kwa kejeli au dharau hadharani.

#### **5.4.24 Hadithi ya Bunuasi na Mfalme**

Hadithi ya Bunuasi na mfalme inaifunza jamii kuwa wasiwe na pupa katika kuamua jambo. Hadithi inaelezea kuwa mfalme alimwambia bunuasi amuandikie majina ya watu wasioona katika mji wake. Hafla Bunuasi alichukuwa tawi la mti na kuliburuta mbele ya Mfalme. Mfalme akamuliza Bunuasi” ni nini anachokifanya?”, hatimaye Bunuasi akamuandika mfalme katika daftari la watu wasioona. Kitendo cha Mfalme kuuliza kwa haraka haraka anachokifanya Bunuasi mbele yake ni dalili ya kuwa Mfalme alikuwa na pupa katika uwamuzi wa utawala wake. Na pia kitendo cha Bunuasi kumuandika mfalme katika daftari la watu wasiona ni ishara kuwa Mfalme huyo hajui vyema mambo yanavyofanyika katika jamii au utawala wake. Kwa hivyo hadithi inafunza maadili Wazanzibari kuwa viongozi wanatakiwa kujua

wanachokisema na kuuliza, pili wasiwe na pupa katika kuamua mambo katika jamii yao. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa jamii ya viongozi na raia kuacha tabia ya kufanya uamuzi wa haraka haraka na pia kuwa waweze kuyajuwa mambo yanayotendeka katika nchi yao.

#### **5.4.25 Hadithi ya Majaliwa**

Hadithi ya Majaliwa inaifunza jamii kuwa ni vyema mtu anayekwenda kwenye mkusanyiko wa watu. avae nguo nzuri au kujistiri vyema maungo yake ya mwili. Majaliwa alikuwa kiongozi wa kikundi lakini alikuwa na tabia ya kwenda kwenye mkutano akiwa na mavazi yaliyochanika chanika. Siku moja mtani wake, alimchoma kijiti cha mbavu huku akihutubia. Majaliwa alishikwa na tahayuri. Hadithi inaifunza jamii kuwa na mavazi ya kujistriri mwilini, yaweza kuficha aibu ya mtu. Waswahili husema mtu anapofika mbele za watu wanakuangalia umevaa nini na wala hawakuulizi umekula nini.

#### **5.4.26 Hadithi ya Majuha Wanne Wasiojuana**

Hadithi inasimulia visa vya majuha wane wasiojuana. Kila Juha anaona mwenake ni juha zaidi. Hadithi ya majuha wanne inawafunza wanajamii elimu kwa kila kisa alichosimulia Juha. Kwanza, hadithi inafunza maadili ya maamkizi katika dini ya Kiislamu. Juha wa mwisho aliyefika aliwasalimia majuha wenzake. Maamkizi aliyowasalimia yalikuwa ni ” assalam alikum Majuha” haya si maadili mazuri, kwa jamii ya Kiislamu. Waislamu husalimiana “assalamu Alaikum” na kuitikiya “alaikum msalaam” kwa ufupi. Kinyume chake ni ujuha unaojitokeza. Hadithi inafunza maadili kwa jamii ya waislamu kuwa wasikubali kuwa majuha na

kukashifiwa Dini yao. Pili, kisa cha Juha wa kwanza kinaifunza jamii kuwa inapotumwa jambo hawanabudi kulifikiria kabla ya kulitekeleza. Wawe na elimu na ujuzi katika kazi zao. Juha anakata kigogo cha kuni na kabla ya kuanguka anapeleka mgongo wake ili kiangukiye mgongoni. Huu ni ujuha, hatari na inaweza kusababisha kifo. Ni ishara kuwa baadhi ya wafanyakazi wanafanyakazi bila ya kuwa na elimu na ujuzi kwa kila wanachokifanya. Watu hawa huleta maafa au vifo katika jamii, ni vyema Wanajamii wakaepukana na ujuha huo.

Hadithi inafunza jamii ya kuwa kuna watu katika jamii wana ukosefu wa ufahamu. Wanafanya mambo kinyume na inavyotakiwa. Mwisho wake ni kifo au maafa. Juha wa pili, alikwenda kungoa jino moja kwa shilingi hamsini na aliporudi nyumbani, mkewe akagomba kuwa ametumiya pesa nyingi kwa jino moja. Juha alirudi hospitali akangowe meno yote. Akarudi na kuyangowa yote. Ikiwa katika jamii kuna mtu mkorofi au mtu mbaya inatakiwa yule mbaya aondoshwe kwenye jamii na wala wasiadhibiwe watu wengine wasio wakorofi kwa sababu ya yule mkorofi.

Hadithi imetoa elimu kwa jamii kuwa ukiwa askari hunabudi kutumia akili na sheria za kazi, si hivyo, unaweza kupoteza maisha yako na mali za watu katika jamii. Juha aliajiriwa dukani, na alitakiwa akija mwizi amuuwe. Kabla ya kumuuwa alitakiwa amulize, na kama hajajibu swali ampige bunduki. Alipokuja mwizi akamuliza ‘‘wewe nani?’’ Akajibu mimi ‘‘mtu’’. Akamuachia na kuiba mali za watu. Juha akazunguka nyuma, akamkuta punda, akamuliza hakujibu, akamuuwa. Huu ni Juha. Pili inawataka matajiri kuchukuwa tahadhari na wale wanawaachia silaha kulinda mali zao katika jamii zao.

Walinzi wasiokuwa na elimu na maarifa wanaweza kutumia silaha hizo na kuleta maafa kwa matajiri na mali zao katika jamii. Siyo kila mtu anaweza kupewa silaha na kulinda. Tano, Juha wa nne, anatoa elimu kwa wanajamii kuwa si vyema kuwafata wake zao jikoni na kudokoa nyama. Kitendo cha kudokoa nyama jikoni ni taswira ya watu ambao wanaweza kuchukuwa mali katika jamii na kuiharibu bila ya taarifa. Pindipo jamii itagundua, watu hawa huingiwa na hatiyani. Ni vyema kuepukana na tabiai kama hii. Kwa ujumla hadithi ya majuha wanne inaifunza jamii kuwa wasalimiane salamu vizuri kama Dini inavyoelekeza, kuacha tabia ya udokozi, kufanyakazi kwa juhudi, akili na maarifa.

#### **5.4.27 Hadithi ya Dereva wa Gari**

Hadithi inaelezea kuwa dereva wa gari alisimamishwa na polisi wa barabarani na kuulizwa amepakia abiria wangapi. Jibu ni kuwa amechukuwa abiria ishirini na tatu na mmakonde mmoja. Gari hili limeruhusiwa kuchukuwa abiria ishirini na tatu. Mmakonde alistahamili, alipofika mbele alikataa kutoa nauli yake kwa sababu dereva wa gari alikwisha kumdharau. Gari aliloendesha dereva ni “mbavu za mbwa” hii ni taswira inayoosha gari chakavu la mbao. Hadithi inaifunza jamii ya nadereva kuwa wawe na lugha nzuri wanapozungumza na abiria wao garini.

#### **5.4.28 Hadithi ya Sungura na Fisi**

Hadithi ya Sungura na Fisi inafunza inaikumbusha jamii kuwa maisha ya mjini kwingi kuna wajanja wanaopenda kula mali za watu bila ya woga. Watu wanapokuwa katika biashara zao wawe makini na wateja wao. Hadithi inaelezea kuwa Sungura alikwenda hotelini akaagiza chakula, akala akashiba. Sungura alichukua panya aliyeoza na akamtumbukiza katika chakula alichokibakisha katika

sahani. Aliwaita wahudumu na kuwafokea na kudai kuwa atamwambia bosi wao. Wahudumu walitoa fedha wakampa Sungura ili asitoe siri hiyo. Kwa hivyo, Sungura ni taswira ya watu wajanja wenye kuishi kwa kutegemea mbinu chafu. Hadithi inaelezea kuwa Fisi naye alikwenda hotelini, akala akashiba. Baadaye Fisi akatia mende katika chakula. Akawaita wahudumu na kuwafokea. Wahudumu wakatoa fedha chache na kumpa fisi ili asitoe siri ile. Fisi kwa tamaa zake alizikataa. Akazua fujo na hatimae akapata kipigo hotelini. Hadithi inaifunza jamii kuwa wanapofanya biashara wawe waangalifu na wateja wao. Fisi ni taswira ya watu wenye tamaa, kila wanachopata hakiwatoshi na hatimaye humalizikia katika maisha mabaya. Kwa jumla hadithi inafunza jamii kuwa baadhi ya wateja wanaokuja katika biashara si waaminifu.

#### **5.4.29 Hadithi ya Mla Matonge**

Hadithi inaelezea kuwa alikuwepo mtu anayependa kula matonge katika karamu za harusi bila ya kutafuna. Kabla ya kumaliza mazungumzo, mwenyewa alitokea. “Mla matonge” ni taswira ya mtu mwenye tabia mbaya kwenye mkusanyiko wa watu na akaleta uharibifu katika jamii. Kwa hivyo, wanajamii wanatakiwa kuepukana na kuwa waharibifu katika mkusanyiko wa shughuli zinazofanyika kama vile harusi. Kwa jumla hadithi ya Mla Matonge inafunza wanajamii wawe na tabia nzuri katika mkusanyiko wa watu.

#### **5.4.30 Hadithi ya Mtepe Uliosheheni**

Hadithi inaelezea kuwa mtepe uliosheheni magunia ya tende ya mwarabu mmoja aliyetaka yapelekwe Lamu. Mchukuzi mmoja alidhani kuwa ni ukwaju, bila ya kufungua wakaaza kuutupa baharini. Baadaye wachukuzi wengine na nahodha wao

akabaini kuwa si ukwaju ila ni tende. Wakarudi mkondoni kutafuta lakini kila anayeingia baharini anakufa. Hadithi ya Mtepe uliosheheni inafunza jamii kwa Wazanzibari kuwa wawe waaminifu wanapopewa bidhaa kusafirisha na wawe wasimamizi wazuri katika mtepe. Hadithi inaelezea kuwa mtepe uliosheheni magunia ya tende ya mwarabu mmoja aliyetaka yapelekwe Lamu. Mchukuzi mmoja alidhani kuwa ni ukwaju, bila ya kufungua wakaaza kuutupa baharini. Baadaye wachukuzi wengine na nahodha wao akabaini kuwa si ukwaju ila ni tende. Wakarudi mkondoni kutafuta lakini kila anayeingia baharini anakufa. Taswira ya Mtepe “kama ni nchi” na “tende” ni mali au utajiri. Nahodha ni kiongozi ambaye ni mweledi katika nchi yake. Baharia wanabeba taswira ya baadhi ya viongozi katika nchi ambao hawana elimu katika sehemu wanazofanyia kazi hatimaye ni hasara kwa jamii. Ndani ya mtepe muna tende, inatupwa baharini kwa kudhani kuwa ni ukwaju. Nahodha alipobaini na kurudi, kila baharia aliyezamia alifariki. Kwa jumla hadithi inafunza wanajamii kuwa wawe wasimamizi wazuri wenye elimu na kulinda mali ya jamii.

**Jedwali Na. 5.5: Hadithi zenye kufunza maadili ya urafiki, dini na imani**

| Namba | Jina la hadithi          |
|-------|--------------------------|
| 31.   | Sungura na membe.        |
| 32.   | Jongoo na nyoka.         |
| 33.   | Marafiki watatu.         |
| 34    | Marafiki wanne.          |
| 35.   | Kipofu aliyeombewa duwa. |
| 36.   | Kichwa kidogo aomba dua. |
| 37.   | Bibi aliyekuwa hajazaa.  |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Hailessalassie na Michenzani (2011)**



### **5.5.31 Hadithi ya Sungura na Membe**

Hadithi ya Sungura na Membe inafunza jamii kuwa wajihadhari na marafiki wanaowapenda sana. Mwisho, urafiki unaweza kuleta faida au hasara. Hadithi inaelezea kuwa Sungura na Membe walialikwa harusini, walipita mtoni kukoga. Sungura alikoga mwanzo na baadaye membe akampa sungura nguo zake ili akoge. Sungura alizikamata nguo mpaka akachoka, kumbe rafiki yake ameshapita chini kwa chini mpaka harusini. Harusini, membe aliimbba nyimbo ya kumpiga fumbo sungura. “kashiki bamba” hii ni lugha ya ishara kuwa sungura kashika kitu kilichokuwa sicho, na ni bamba lisilo thamani. Baada ya Sungura kurudi nyumbani. na harusini imeshamaliza. Pili, marafiki wanaweza kukupa kitu cha hadaa au kisichokuwa cha kweli. Nyimbo aliyokuwa akiimba membe ilionyesha kuwa sungura keshadanganywa.

### **5.5.32 Hadithi ya Jongoo na Nyoka**

Hadithi inaeleza kuwa jongoo na nyoka walikuwa marafiki sana. Nyoka alialikwa harusi lakini hana macho ila ana miguu, kwa hivyo alikwenda kuanzima macho kwa rafiki yake, jongoo. Alikwenda harusini na kushindwa kuyarejesha macho aliyoyaaazima. Kitendo cha nyoka kuanzimwa macho na kukataa kuyarejesha kunaonyesha kuwa baadhi ya marafiki wakiazima jambo la thamani, hawarejeshi tena. Kwa hivyo hadithi inafunza wanajamii kuwa wako marafiki wema na wabaya. Pili, hadithi inatoa elimu kuwa kuna watu katika jamii, imani yao ndiyo iliyowaponza katika maisha waliyonayo hivi sasa. Imani ya jongoo aliyokuwanayo ndiyo iliyompelekea kumuazima macho yake nyoka. Kwa jumla hadithi inasisitiza wanajamii kuwa ahadi ni deni, ukiazima kitu ukumbuke kukirejesha. Pili, kwenye jamii kuna marafiki wazuri na wabaya.

### **5.5.33 Hadithi ya Marafiki Watatu**

Hadithi ya marafiki watatu, Kizingiro, Miliso na Kizingiro inatoa elimu kwa wanajamii kuwa mtu anapotumwa kitu dukani ni vizuri kukielewa au kufahamishwa vyema na yule anayemtuma ili asiye akasumbuka madukani. Hadithi inaelezea kuwa Kizingiro alimtuma Miliso dukani akanunuwe zungusho. Katika utamaduni wa Kizanzibari unapokwenda dukani na ukasema unataka zungusho, analolifanya mduka ni kukuzungusha duka au mahali pengeni. Mduka huwa anaelewa kuwa hakuna kitu hicho dukani ila mteja anatakiwa uzungushwe kwenye maduka. Wenye maduka hufanya hivyo huku wakicheka. Mwisho anaporejea nyumbani, atawakuta watu wanamcheka na kumuuliza kuwa amelipata zungusho au hakulipata. Hadithi inawafunza watu wanaofika Zanzibar, wanapotumwa dukani watafakari vizuri kile walichotumwa dukani ili wasije wakapata tabu.

### **5.5.34 Hadithi ya Marafiki Wanne**

Hadithi ya marafiki wane inaifunza jamii kuwa katika utani kunaweza kukaleta maafa makubwa. Hadithi inaelezea kuwa marafiki wanne walikuwa na tabia ya kutaniana. Mmoja alimwambia rafiki yake kuwa anajua sehemu ambayo mke wake huwa anakwenda. Alimjibu harusini. Rafiki yake alimuelezea kuwa hutoka na bwana aliyekuwa akipita mbele yao wakati huo. Bwana alizimia. Kitendo cha “kuzimia” ni lugha ya ishara kuwa alifahamu bwana huyo ni mume mwenzake katika jamii. Wanakula sahani moja.

### **5.5.35 Hadithi ya Kipofu Aliyeombewa Dua**

Hadithi ya Kipofu aliyeombewa dua inaifunza jamii kuwa katika ulimwengu wako wacha Mungu, Mwenyezi Mungu amewateuwa na wanaloliomba wanapata. Hadithi

inaelezea kuwa alitokea mtu mwema na mwenye baraka, aliwaombea watu dua na Mwenyezi Mungu akaikubali dua yake. Kipofu aliyeombewa dua na mcha Mungu akaona kwa muda mfupi. Alimuona jogoo, kwa muda mfupi, akarudia upofu wake. Na ikawa kila anachokisikia yeye huliza, kuliko jogoo. Hadithi inaifunza jamii kuwa waliokuwa na vipaji au elimu wawasaidiye wanajamii ili kutatua matatizo.

#### **5.5.36 Hadithi ya Kichwa Kidogo Aliomba Dua**

Hadithi ya kichwa kidogo aliomba dua inaifunza jamii kuwa jambo alilokupa Mwenyezi Mungu ndilo lenye kheri na wewe, si vyema kuomba jambo ambalo unaliona kwa wenzako. Hadithi inaelezea kuwa kichwa kidogo aliomba dua kwa Mwenyezi Mungu kuwa ampe kichwa kikubwa. Alifanya ibada na kupitisha kichwa chake kwenye matundu ya dirisha ili kuangalia nnje. Mungu alimwitikia dua yake, lakini kichwa chake kilikwama katika dirisha, “kikakwama katika dirisha na kupiga kelele” hii ishara kuwa aliloliomba na kupewa halina kheri na yeye. Watu walikuja na kuvunja nondo na kutowa kichwa chake. Kitendo cha kuvunja nondo za dirisha ni ishara kuwa kichwa kikubwa alichokitaka kitamletea matatizo mbalimbali. Kwa hivyo, hadithi inafunza maadili kwa jamii ya Wazanzibari kuwa kwa Mwenyezi Mungu hakuna kubwa, ukimuomba atakupata, mwanadamu awe na ustahamilivu na subira katika maisha. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kuwa Mwenyezi Mungu ni mkubwa na mwingi wa kuwakirimu waja wake.

#### **5.5.37 Hadithi ya Bibi Aliyekuwa Hajazaa**

Hadithi ya bibi aliyekuwa hajazaa muda mrefu inaifunza jamii kuwa ni vyema mtu akaelewa vyema jambo analoliomba kwa Mwenyezi Mungu. Hadithi inaelezea kuwa

bibi huyo alikwenda matembezi na akakiona “kijoka sindano”. Baadaye akamuomba Mwenyezi Mungu ampe mtoto kama kile kijoka sindano. Punde, bibi, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu alipata ujauzito na kuzaa Mtoto kama kijoka sindano. Hadithi inaifunza wanajamii kuwa watafakari na jambo wanaloliomba kwa Mwenyezi Mungu. Pili taswira ya “kijoka sindano”ni mtoto ambaye hakuwa na manufaa kwa wazee kama vile walivyotarajia ila wazee watakuwa na mithili ya mtoto.

**Jedwali Na. 5.6: Hadithi zenye kufunza maadili ya Mapenzi na tabia njema**

| <b>Namba</b> | <b>Jina la hadithi</b>                              |
|--------------|---|
| 38.          | Binti wa shamba kaingia mjini                       |
| 39.          | Tupa, Shida na Asha                                 |
| 40.          | Sultani na Suria                                    |
| 41.          | Mtu na mkewe  |
| 42.          | Jogoo na mkewe                                      |
| 43.          | Bwana aliyepewa mkoba sokoni                        |
| 44.          | Bibi mjamzito                                       |
| 45.          | Mzee Mpacho na wajukuu wake                         |
| 46.          | Kijana aliyejifanya msomi                           |
| 47.          | Babu na jiwe  |
| 48.          | Kijana aliyeomba penzi kwa ndugu yake bila ya kujua |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Bembella na Kizimbani (2011)**

**5.6.38 Hadithi ya Binti wa Shamba Kaingia Mjini**

Hadithi ya binti wa shamba kaingina mjini inaifunza jamii kuwa wanawake walioolewa shamba na kuhamishiwa mjini kuwa makini katika mazingira yao. Wanawake wanatakiwa kujifunza au kuuliza mambo yaliyoko mjini kabla ya kuigaiga. Hadithi inaelezea kuwa binti wa shamba alipofika mjini, ndani ya nyumba aliona kioo kilichomuhadaa kwa sura yake mwenyewe na kufikiri kuwa ni mwanamke mwengine. Kitendo cha kukivunja kioo na kumtafuta mwanamke aliyemuona ni ishara ya kuwa na wivu na kutoelimika na mazingira mapya ya mjini. Hadithi inaifunza jamii ya wanawake waliolewa kutoka shamba na kuja mjini,

kushirikiana na waume zao. Jambo wasilolifahamu, wawaulize waume zao badala ya kuchukuwa hatua za kuharibu. Wakumbuke kuwa mjini kuna mengi.

#### **5.6.39 Hadithi ya Tupa, Shida na Asha**

Hadithi ya Tupa, Shida na Asha inatoa elimu kwa wanajamii kuwa wazee wasiwaite watoto wao majina mabaya. Mtoto akizaliwa apewe majina mazuri. Mzee Tupa alimposea mwanawe mke. Mwanamke na mwaname hawakuwahi kuonana ila siku ya harusi. Mwanamke alipotakiwa kauli yake kama yuko tayari kuolewa na shida, alikataa. Hata hivyo, harusi ilifanyika lakini bi harusi alikimbia kwa mume wake na kuelekea kwa manamke aliyempenda kabla ya kuoana. Jina la ‘Shida’ kwa bi harusi lilijenga taswira ya “tabu, dhiki au matatizo” kwa hivyo mwanamke aliweza kukimbia kwa sababu ya jina tu. Pili, hadithi inawafunza wazee kuwa ni vyema watoto wakapewa uhuru wa kuchagua mchumba badala ya kufanya harusi za kulazimisha. Pili, harusi za kulazimisha zinawaletea wazee aibu mitaani. Tatu, si vyema bi harusi kumtoroka mume wake wa ndoa mtaani Kwa jumla hadithi inaifunza jamii kuwa wazee wasiwaite watoto wao majina mabaya, watoto wachaguwe wachumba wanaowataka na wanapoolewa wasiwatoroke waume wao mitaani na kwenda kuishi na mtu mwengine asiye wa ndoa.

#### **5.6.40 Hadithi ya Sultani na Suria**

Hadithi ya Sultani na Suria inawafunza wanajamii kuwa elimu ya amali ni muhimu katika maisha. Hadithi inaelezea kuwa mtoto wa mfalme, Sultani alitaka mke ambaye anajua kupika chakula kizuri. Katika kijiji hicho, kulipigwa mbiu ya mgambo na watu mbalimbali walifika. Suria alikuwa mtu wa mwisho kimpangilio

kutokana na umasikini wa wazee wake. Mtoto wa Mfalme alipokionja chakula cha Suria alikila mpaka akakimaliza, kwa hivyo Suria na Sultani walioana. Hadithi inafunza maadili kuwa mapenzi hayachagui tabaka au kabila “Sultani” ni taswira ya utajiri na “Suria” ni taswira ya unyonge au umasikini. Lakini waliweza kuoana kutokana na elimu ya ujasiri amali wa kupika chakula. Kwa jumla hadithi inasisitiza kuwa elimu ya ujasiri amali, kuondosha matabaka na kuimarisha ushirikiano katika jamii.

#### **5.6.41 Hadithi ya Mtu na Mkewe**

Hadithi inaelezea kuwa bwana mmoja alikwenda kuiba ndizi ambayo ilikwisha fanyiwa dawa za miti shamba. Walipokula, bwana alivimba tumbo na kupasuka. “Ndizi” ni taswira ya mali isiyokuwa yako na’ kuvimba tumbo na kupasuka” ni dalili ya kuwa unapochuma mali zisizokuwa za halali, iko siku zitakutoka hadharani kwa hivyo, ni vyema Wazanzibari kuacha kula mali za haramu. Wakumbuke methali inayosema kuwa cha myonge utakitapika hadharani. Kwa jumla hadithi ya mtu na mkewe inaifunza jamii kuwa kutafuta mali za halali ili waishi vyema katika jamii.

#### **5.6.42 Hadithi ya Jogoo na Mkewe**

Hadithi inaelezea kuwa mke wa jogoo alikuwa anahofu ya kuzaa kwa sababu watoto wataliwa na kipanga. Jogoo alimwambia mkewe asiwe na hofu atampeleka mkewe wakati wa kuzaa ili azae bila ya woga. Mke wa jogoo ilipofika wakati wa kuzaa alilia na kusema:

“ntaka ntaka ntakazaa ntaka zaa”

Hii ni taswira inayojitokeza kuwa mwanamke anapofika wakati wa kujifungua au kuzaa huwa anakabiliwa na hali ngumu katika nafsi yake na anahitaji msaada kwa upande wa mume wake au jamii. Ilipofika siku ya kuku kutoa watoto wake nnje, alipita mwewe, jogoo alikimbilia vichakani na kuku jike akawafunika watoto wake mabawani. Siku nyengine kipanga akipita hupata nafasi ya kuchukua kitoto cha kuku kimoja kimoja. Jogoo akiulizwa husema kipanga amekuja kwa ghafla. Taswira ya jogoo kukimbia ni kuonyesha woga na mapenzi ya hadaa kwa mama na watoto. Kwa hivyo hadithi inafunza madili kwa jamii kuwa wako akina baba ambao wanawachia ulezi akina mama tu, wakati wote. Ikitokea maradhi au tatizo lolote lile huwa la mama peke yake. Baba haonikani na akiyaona matatizo huwa anakimbia. Wanajamii wanatakiwa waishi maisha ya kushirikiana. Wasiwe kama kuku na jogoo. Hadithi inaelezea kuwa mwisho kuku jike anagundua kuwa ujanja wa jogoo ilikuwa ni mapenzi ya hadaa na kumshambulia:

“huna uume taa huna uume taa, waacha watoto waliwa”

Jogoo hujibu “sinchezele, sinchezele, anganikamata miie, anganikamata mie”. Taswira hii inaonyesha kuwa jogoo anamuogopa kipanga asiye akamchukua. Alihiari akachukuliwe koo au mwanawe. Katika jamii wako watu kama hawa wanaowakimbia wake zao wakati wa matatizo na wao kuishi sehemu nyengine mpaka matatizo yamalize. Kwa jumla hadithi inaifunza jamii maadili kuwa iwe na mapenzi bora na kushirikiana katika kulea watoto.

#### **5.6.43 Hadithi ya Bwana Aliyepewa Mkoba Sokoni**

Hadithi ya bwana aliyepewa mkoba wa sokoni inaifunza jamii kuwa walioowa au kuolewa wawe wastahamilivu katika ndoa zao. Mwanamme anajukumu la kutafuta

chakula, mavazi, malazi, na kumfundisha mambo bora mke wake, kulingana na dini yao. Haya yanahitaji ustahamilivu. Mke naye anastahiki kumfuata mumewe na kumtii kulingana na dini yake. Hadithi inaelezea kuwa bwana alimpelekea mkewe muhogo mchungu kama shubiri. Hii ni taswira ya chakula ambacho si kizuri katika jamii. Baada ya siku tatu, mke alichukuwa mkoba na kuandika jina la kumkejeli mume wake. Kila aliyemuona na mkoba huo sokoni alimcheka. Hii ni taswira ambayo mwanamke alitumia kama silaha ya kujigomboa kutoka kwa mume wake. Kitendo hiki kilimtia aibu mume wake na kumuacha. Hadithi inaifunza jamii kuwa ni vyema watu wajue kusoma na kuandika. Pili, wakichukua mkoba au kuvaa nguo zenye majina ni vyema kuelewa maana ya majina hayo ili yasije kuwaletea aibu. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa wanajamii kuwa wawe wastahamilivu katika ndoa zao na wajuwe kusoma na kuandika.

#### **5.6.44 Hadithi ya Bibi Mjamzito**

Hadithi ya bibi Mjamzito inaifunza jamii kuwa wanawake wanapokuwa waja wazito wasiwe waroho na waishi na majirani zao vizuri. Hadithi inaelezea kuwa bibi mjamzito alipika ugali wake lakini kabla ya kula alisikia hodi na kuanza kuficha sahani yake ya ugali. Mgeni aliingia ndani na alibaini kilichomo ndani lakini hakukaribishwa, aliondoka na kurudi tena. Alimuona bibi mjamzito anakula na yeye akakaa pale pale. Baada ya kuondoka bibi mjamzito akaanza kulia kwa sababu ugali wake umeliwa. Kitendo cha kuficha ugali ni dalili ya uchoyo, na si maadili mazuri kwa jamii Pia, mgeni kula chakula bila ya kukaribishwa si vizuri. Hivyo, hadithi inawafunza wanajamii waishi maisha mazuri na majirani zao. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa wanajamii kuwa waishi vizuri na majirani zao, wasiwe waroho katika kula na wageni wapige hodi kabla ya kuingia katika nyumba.



#### **5.6.45 Hadithi ya Mzee Mpacho na Wajukuu Wake**

Hadithi ya mzee Mpacho na wajukuu wake inawafunza wanajamii kuwa watoto wanapooona mambo mapya katika mazingira yao wanashtuka kwa hivyo, wazee wanaposikia mayowe, waharakishe kwenda kuwasaidia. Hadithi inaelezea kuwa mzee Mpacho alisikia mayowe kutoka kwa wajukuu wake. Alipoambiwa kuwa ni nyoka, akauona mkia tu, naye alikimbia huku akipiga kelele kama wajukuu wake. Hata hivyo, mjukuu wake mmoja alibaini kuwa ni mjesi. Hadithi inafunza jamii kuwa wanaposikia watoto wao wanapiga kelele sehemu wanazochesha, ni vyema kutoka na kuchunguza kwa makini kilichosababisha mshituko kwa watoto. Kwa jumla hadithi inaifunza jamii kuwa mtu mzima hachekwi na watoto. Pili, watoto wasiwacheke watu waliowazidi kiumri wanapowaona wazee wao wamefikwa na shida au matatizo mitaani.

#### **5.6.46 Hadithi ya Kijana Aliyejifanya Msomi**

Hadithi ya kijana aliyejifanya msomi inaifunza jamii kuwa wasichukuwe vitabu na kalamu na kupita mitaani ili waonekane wasomi hali ya kuwa hawajui kusoma wala kuandika. Hadithi inaelezea kuwa siku moja, wazee wa kijiji walipata barua lakini hawajui kusoma, hivyo walimtafuta kijana anayepita mitaani na vitabu vyake, msomi. Alipopewa barua aliifungua na kuanza kulia, watu wote walianza kulia wakifikiria kuwa ndani ya barua hiyo muna habari za kifo. Hadithi inaifunza jamii kuwa watahadhari na wasomi bandia wanaopitapita mitaani. Taswira ya kijana na vitabu vyake mitaani, ni ishara kuwa wazee wa kijiji wawe na tahadhari na wasomi wa bandia ambao wanaleta matatizo katika jamii husika wanazoishi na kutia hasara bila ya kujua.

#### **5.6.47 Hadithi ya Babu na Jiwe**

Hadithi ya babu na jiwe inaifunza jamii kuwa wazee wasikae uchi mbele ya watoto, ni aibu mtu mzima kuonekana na watoto. Hadithi inaelezea kuwa Babu alikunja shuka yake na kukaa utupu, wajukuu wakamuuliza kitu kilichokuwa kinaning'inia baina ya miguu miwili. Babu aliwajibu kuwa ni jiwe. Hadithi inaifunza jamii ya kuwa wazee wavae nguo vizuri na kuacha kukaa uchi mbele ya watoto. Pili, wazee wanatakiwa wasiwafundishe watoto wao kusema uongo. Watoto wanaweza kumuliza wazazi wao kwenye mkusanyiko wa watu mambo yasiyostahili kulizwa hadharani. Kwa jumla hadithi ya babu na jiwe inawafunza wanajamii kuvaa nguo zenye stara mbele ya watoto au jamii na kuwafundisha watoto wao kusema ukweli

#### **5.6.48 Hadithi ya Kijana Anaomba Starehe kwa Ndugu yake Bila ya Kujua**

Hadithi ya kijana aliyeomba starehe kwa ndugu yake bila ya kujua, inatoa elimu kwa wanajamii kuwa waache vitendo vya ngono wakiwa vijiwani ikiwa ni mchana au usiku. Hadithi inaeleza kuwa ni saa tatu, usiku wakiza, mvulana huyo alipomuona kijana wa kike aliyekuwa amatembea kidogo kidogo, alianza kumuomba starehe. Ulipotokezea muangaza wa gari na kumpiga usoni, aligundua kuwa ni dada yake na kuomba radhi. Pia, jamii ya wanawake wanatakiwa waepukane na tabia ya kutembea ovyo usiku wakiwa na mavazi yasiyo na heshima barabarani. Hadithi inatoa taswira ya “mwanamke amepita akiwa kachoka na kutembea kwa maringo”. Hii ni taswira ya mwanamke katika jamii aliyekuwa hana maadili mazuri. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa wanajamii kuwa waache tabia ya kukaa vijiwani na kuomba starehe kwa wapita njia kwa sababu inaweza kuleta madhara katika jamii wanazoishi.

Ngano ni hadithi fupi zisimuliwazo kuwaasa watoto kwenye maadili ya jamii fulani, mara nyingi ngano huanza kwa Paukwa.....Pakawa na kuishia “Kwa....raha mustarehe” wakati mwengine ngano huambatana na nyimbo, wahusika wake hujitokeza katika aina nyingi, kama vile, wadudu, wanyama, binadamu, mzimu na miungu. Pia vitu visivyo na uhai kama vile mawe, milima nakadhalika. Ngano huambatana na maadili mbalimbali katika jamii husika.

Mgawanyo wa hadithi za ngano katika mikabala ifuatayo:

1. Hadithi zenye kufunza maadili ya sheria na malezi
2. Hadithi zenye kufunza maadili ya itikadi za kijamii
3. Hadithi zenye kufunza maadili ya usaliti, wivu na choyo

**Jedwali Na. 5.7: Hadithi zenye kufunza maadili ya Sheria na malezi**

| Namba | Jina la hadithi                    |
|-------|------------------------------------|
| 49.   | Mfalme na maradhi                  |
| 50.   | Sungura na Fisi                    |
| 51.   | Mama na watoto wa kambu            |
| 52.   | Mtoto aliyeomuomba radhi mama yake |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Kizimbani na Mitiulaya (2011)**

**5.7.49 Hadithi ya Mfalme na Maradhi**

Hadithi ya Mfalme na maradhi inaifunza jamii kuwa ni vyema kwa kiongozi wa nchi akaweka sheria ambazo hazitaleta madhara kwa mtu, watu au jamii fulani. Anapotunga sheria ni vyema ikachunguzwa na wasaidizi wake kabla ya kutumika. Hadithi inaelezea kuwa Mfalme alitangaza kuwa kuna maradhi ya kipindupindu kwa hivyo, nzi anapoonekana pahala popote auliwe. Siku zikapita na nzi wakauliwa.

Siku moja, mfalme akaitisha mkutano wake, huku akiwa amenyoa kipara wakati wa mkutano. Nzi alitua katika kichwa cha mfalme.

Mtu mmoja akapiga rungu kichwa cha mfalme na hatimaye, mfalme akafariki pale pale. Mtu huyo alishitakiwa lakini akaachiwa kwa sababu alikuwa anatekeleza amri ya mfalme. Pili, hadithi ya Mfalme na maradhi inawafunza wanajamii kuwa maradhi ya kipindupindu ni adui mkubwa kwa wanajamii. Maradhi haya yanauwa watu wengi kwa haraka kama hapana dawa. Ni vyema wanajamii wakaweka mazingira yao katika hali ya usafi. Hadithi inaelezea kuwa mfalme aliona kuwa jamii inapata maradhi yanayosambazwa na nzi, akatoa amri kila anapoonekana nzi auliwe. Hii ilikuwa ni amri nzuri lakini haikuwa halali kusema kuwa “kila anapoonekana nzi auliwe”. Ingekuwa vizuri kutaja maeneo ambayo yanatakiwa inzi kupigwa. Sheria iliyotungwa vibaya. Watu walipata matatizo na mfalme alipoteza maisha. Ni vizuri kuichunguza sheria kabla ya kuitangaza matumizi yake kwa jamii.

Hadithi inaifunza jamii kuwa sio kila analolisema kiongozi likatekelezwa, ni vizuri kupatiwa ufafanuzi utekelezaji wake. Mfalme amepigwa rungu la kichwa na akafariki hapo hapo. Taswira inafunza maadili kuwa sheria ni msumeno, kwa wadogo na wakubwa. Kiongozi, leo yuko kwenye madaraka lakini kesho akimaliza muda wake. Sheria ile aliyoitunga inaweza kumbana na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria na kushitakiwa. Kwa hivyo wafalme wawe makini wanapotunga au kupisha sheria. Kwa jumla hadithi ya mfalme na maradhi inasisitiza kuwa jamii itunge sheria ambazo zina misingi mizuri ambayo haitaleta matatizo kwa watu na mali zao.

#### **5.7.50 Hadithi ya Sungura na Fisi**

Hadithi inasisitiza kutatua migogoro inapotokezea katika jamii. Pili, hadithi inatoa elimu kuwa adhabu ikitolewa isizidi mipaka na kuleta hasara katika jamii. Hadithi inaelezea kuwa baada ya wanyama kukutana, walikubali fisi asiuliwe na wengine walitaka wampofuwe macho lakini tatizo likawa ni jinsi ya kumkamata. Hii ni taswira ambayo inaonyesha kuwa adhabu aliyotakiwa apewe fisi ni kubwa. Kumtoa macho ni kumuharibia maisha. Fisi atakuwa haoni tena linalofanyika katika jamii. Tatu, hadithi inawafunza wanajamii kuwa kwenye jamii yenye mashirikiano ni rahisi kutatua matatizo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Hadithi inaelezea kuwa sungura alitumia hekima na busara na kufika nyumbani kwa Fisi. Sungura aliweza kumlainisha fisi na matumaini ya kula nyama. Fisi alihadaiwa kwanza atiliwe kwenye kinywa chake. Mwisho, fisi alitiliwa jiwe lilokuwa la moto katika mdomo wake na akafariki dunia. Kwa ujumla hadithi ya Fisi na Sungura inaelimisha jamii kuwa wanadamu wanatakiwa wasiwe na tamaa kupita mpaka, wanaweza kupata matatizo. Wanajamii wawe na umoja na mshikamano.

#### **5.7.51 Hadithi ya Mama na Mtoto wa Kambu**

Hadithi ya Mama na mtoto wa kambu inawafunza wanajamii kuwa baadhi ya mama wa kambu wanakuwa na tabia mbaya kwa watoto wanaowalea. Kwa hivyo ni vyema baba akawa muangalifu sana katika malezi. Hadithi inaelezea kuwa mama Asha alikuwa hampendi Fatma, mtoto wake wa kambu. Baba yake alipoondoka, mama Asha alimchukua Fatma, akampeleka porini, akamchimbua shimo na akamfukia ili baba yake asimuone atakaporejea safari yake.

Baba Asha aliporejea safari yake alimuuliza mkewe na alitaka kujua Fatma alipo. Mama Asha alikataa kusema lakini Asha alimpeleka baba yake porini, akaimba wimbo ambao ulimuwezesha Fatma kuitambua sauti ya Asha. Baba na mtoto wake walimfukuwa Fatma na wakamuona ameshaharibika sehemu moja. Walirejea nyumbani wakiwa na hasira. Baba alitaka kumuacha mkewe lakini Fatma alimuomba. Taswira hii inafunza maadili jamii ya Wazanzibari kuwa baadhi ya walezi wana tabia mbaya. Wazee wanapoondoka kwenda kazini au safari ni vyema kuchunguza malezi ya watoto wao. Pili, wazee wasiwe na hasira katika kutatua matatizo ya kifamilia wanapoyaona. Taswira ya Baba Asha kuamua kutaka kumuacha mke wake inafunza jamii kuwa si vizuri kumfukuza mtu aliyefanya makosa ila ni vyema kuelimishwa makosa yake ili asiyarudiye tena. Tatu, hadithi inaifunza jamii kuwa watoto wanalelewa na mama, baba na jamii. Mama Asha alikuwa hampendi Fatma kwa sababu alikuwa mtoto wa kambu. Hadithi inaelezea kuwa wanakijiji walikuwa hawakupenda tabia ya mama Asha kutokana na vitendo alivyokuwa akimfanyia. Mtoto wake.

“mama Asha alikuwa hampendi sana Fatma kwasababu alikuwa ni mtoto wake wa kambu alikuwa anamtesa mtoto huyo kitendo ambacho kilikuwa kinawaumiza sana watu waliokuwa wanaishi kijijini hapo”

Maelezo haya yanathibitisha kuwa mama Asha alikuwa hampendi mtoto wake wa kambu. Hadithi inafunza maadili kuwa mtoto, katika mazingira ya kizanzibari, hulelewa na jamii. Nne, hadithi inaifunza jamii kuwa wanapoondoka kwenda safari, watu wenye tabia mbaya wanapata nafasi ya kutenda mambo maovu. Ni vyema kuyafuatilia. Mama Asha alipoona baba Asha ameshaondoka, alipopata nafasi

ya kwenda porini na kuchimba shimo alilomfukia Fatma. Hivyo, jamii ya Wazanzibari wanatakiwa wawe na tahadhari wanapoondoka katika majumba yao. Viongozi katika nchi waelewe kuwa wanapoondoa katika nchi, baadhi watu wanaweza kusababisha uharibifu katika familia au jamii. Wimbo anaoimba Asha na Fatma unathibitisha hali hiyo:

Asha akaanza kuimba:

“Fatma ee, baba yetu kesharudi, Fatma ee

Fatma katuletea zawadi, Fatma ee Fatma

Fatma akajibu:

Asha ee Asha ee, mama ako hanipendi Asha

kanichimbia handaki Asha ee Asha.

Kanitia mumo Asha ee Asha .....

Wimbo huu unathibitisha kuwa Asha alikuwa ametiwa ndani ya shimo baada ya baba yake kwenda safari. Kwa jumla hadithi ya mama na watoto wake wa kambu inaifunza jamii kuwa baadhi ya mama wa kambu wanawafanyia vitendo viovu watoto wao wa kambu.

#### **5.7.52 Hadithi ya Mtoto Aliyeomba Radhi kwa Mama yake**

Hadithi ya mtoto aliyeomba radhi kwa mama yake inawafunza wanajamii kuwa wasiwadharau wazazi wao. Wazee ndiyo dira ya maendeleo ya mtoto au watoto katika maisha yake ya dunia na akhera. Hadithi inaelezea kuwa mama alimwita mtoto wake ili amtume dukani lakini, mtoto aliweza kusema kwa mama yake kuwa “kila wakati anatumwa yeye tu”. Jambo hilo lilimkera mama yake na akajaribu

kumueleza kuwa faida na hasara zake. Baadaye mtoto alifahamu na aliweza kuomba radhi kwa mama yake.

“Ewe mwanangu leo uko hapa kesho uko kwengine aibu inaweza kukufika”

“Mama Sitorejea tena baada ya hapo niliposema nitatunza heshima na nasaha zako”

Maelezo haya yanatoa taswira kuwa mtoto anapokosea hana budi kuomba radhi. Pili, hadithi inasisitiza kuwa mtoto anapokosea na kuomba radhi kwa wazazi wake ni vyema wazazi kumkubalia. Kwa sababu dua ya mama au mlezi inaweza kuleta madhara kwa mtoto. Hadithi inaeleza kuwa baada ya mtoto kuomba radhi kwa wazazi wake aliweza kuishi na kupata mafanikio mema. Kwa jumla hadithi inaelimisha wanajamii kuwa mtoto anavyomlelewa katika maisha ndivyo anavyokuwa. Wazazi wajitahidi kuwafunza maadili mema watoto wao ili waishi maisha mazuri, hapa dunia na mbele ya Mola wao.

**Jedwali Na. 5.8: Hadithi zenye kufunza maadili ya itikadi za kijamii**

| Namba | Jina la hadithi                |
|-------|--------------------------------|
| 53.   | Makame wa Makame atafuta mtoto |
| 54.   | Makumbi yageuka fedha          |

**Chanzo: Shule ya Sekondari ya Mitiulaya (2011)**

**5.8.53 Hadithi ya Makame wa Makame Atafuta Mtoto**

Hadithi ya Makame wa Makame atafuta mtoto inaifunza jamii kuwa kila mtu amshukuru MwenyeziMungu alivyomjalia katika ndoa yake. Mwenyezi Mungu,



akimpa mtoto ashukuru na asipompa pia amshukuru. Hadithi inaelezea kuwa Makame wa Makame na Mkewe walikaa muda mrefu na mkewe hawajapata mtoto katika ndoa yao. Waliamua kwenda kwa mganga wakapewa masharti ya kwenda porini na kutafuta ua jekundu. Wakishapata walifunike chungu. Walipewa masharti kuwa wasije wakamwambia mtoto asili yake. Mtoto alipokuwa mkubwa alikuwa mtundu na mkaidi. Siku moja mama yake alikasirika na kumwambia mtoto asili yake. Mtoto alikasirika na kukimbia huku akielekea porini, mwisho aligeuka ua.

Taswira ya mtoto kukasirika na kuelekea porini ni kuwa mtoto huyo hakuwa mweye kuleta manufaa katika familia au jamii. Kwa hivyo, hadithi inafunza maadili kuwa jambo alilokukosesha Mwenyezi Mungu ni vyema mwanadamu akafanya subira, kwani mwenye kusubiri hajuti. Pili, hadithi ya makame wa Makame anatafuta mtoto inaifunza jamii kuwa na umuhimu wa mganga au mtabibu katika jamii za kiafrika. Kila maradhi yana matibabu yake. Mganga alijua matibabu ya Makame wa Makame na Mkewe lakini watu hawa walishindwa kufuata masharti. Hili lililokuwa tatizo la kukosa mtoto. “Mtizame Yule mtoto wamauwa tu” basi mtoto aliamaki na kuanza kurudi kwao ambako ni mtini, sharti lilitenguka na mtoto alikwenda zake huku akilia njiani na kuimba nyimbo ifuatayo:

“Mama kanambia mtoto wa maua, kwaheri mwana maua

Kwa heri mwana maua, kwa heri mwana maua...

Wimbo unathibitisha kuwa mtoto mkaidi alikimbia porini huku akilia.

Kwa jumla hadithi ya Makame wa Makame atafuta mtoto inaifunza jamii kuwa ni vyema kumshukuru Mwenyezi Mungu alivyokujalia katika ndoa. Pia ni vizuri kufuata ushauri wa waganga.

#### 5.8.54 Hadithi ya Makumbi Yageuka Fedha

Hadithi ya makumbi yaliyogeuka fedha inaifunza jamii kuwa watoto waheshimu wazazi wao wakiwa ni matajiri au maskini. Radhi za wazee kwa mtoto zinaweza zikampelekea kuwa na maisha mazuri au mabaya katika dunia na akhera yake. Hadithi inaelezea kuwa mama alifunga safari ya kuwatembelea wajukuu wake na aliamua kuwachukulia zawadi ya makumbi. Kila mjukuu alipopewa makumbi alitakiwa ayafiche. Siku moja mtoto alipoanza kwenda kuvipunguza vifurushi alivyoletewa, ghafla alizona noti katika vifurushi. Alipiga kelele na kumwita mumewe kwa mshangao. Kitendo hicho kiliwazidishia utajiri yeye na mama yake. Taswira ya mkumbi yaliyoletwa na bibi ni kuwa radhi za wazee kwa watoto au wajukuu ni baraka katika ndowa na familia nzima. Hadithi inaifunza jamii kuwa radhi za wazee ni muhimu katika maisha ya watoto au wana ndoa. Pili, hadithi inafunza maadili kwa jamii kuwa mapenzi ya kweli ya mume na mke huleta baraka na Mwenyezi Mungu. Kitendo cha mjukuu kupokea zawadi ya kifurushi asichokijua na kufuata maelekezo ya bibi yake, mwisho alibaini kuwa ni fehda zilizowaengezea utajiri yeye na familia yao. Kwa jumla hadithi inawafunza watoto kuwaheshimu wazazi wao ili waishi vizuri na familia zao.

#### Jedwali Na. 5. 9: Hadithi zenye kufunza maadili ya usaliti, wivu na choyo

| Namba | Jina la hadithi                    |
|-------|------------------------------------|
| 55.   | Sungura,tembo na kobe              |
| 56.   | Simba Mzee na Sungura              |
| 57.   | Mwanamke aliyeolewa na Zimwi       |
| 58.   | Simba na sungura                   |
| 59.   | Wazee wakulima                     |
| 60.   | Nguruwe na Komba                   |
| 61.   | Simba na mkewe na Sungura na mkewe |

**Chanzo: Shule ya Sekondari Bembella, Bububu na Hailesallassie (2011)**

### **5.9.55 Hadithi ya Sungura, Tembo na Kobe**

Hadithi ya Sungura, Tembo na Kobe inaifunza jamii kuwa kiumbe yeyote anayejikubalisha kuingia katika mashindano ni lazima kujiandaa. Kwenye mashindano kila mtu hujiandaa kupata ushindi. Hadithi inaelezea kuwa Sungura, Tembo na Kobe wote walikuwa katika mashindano. Sungura alijiona mjanja, mwepesi na anauwezo wakushinda kuliko tembo. Tembo alijiona mkubwa na mwenye nguvu, anaweza kufanya au kutenda lolote akamshinda sungura na kobe.

Kobe alijiona hana mwendo mbele ya sungura na tembo lakini ni vyema akawalika ndugu zake kwa vile wamefanana. Mashindano yalipoanza, kila kichaka cha mashindano alikaa kobe mmoja, tembo na sungura hawakujua. Mwisho wa mashindano hayo, kobe alishinda. Sungura na tembo waliduwa na wakamchukia kobe. Taswira hii inaifunza jamii kuwa kila penye mashindano, ni vyema kujiandaa ili kuhakikisha kuwa hakuna udanganyifu wa kuwakosesha ushindi. Pili, hadithi inaifunza jamii kuwa akushindaye kwa tonge mshinde kwa kutowea. Hadithi ya Sungura, tembo na kobe inaelezea kuwa sungura alijiona kuwa yeye ndiye mjanja katika jamii kuwashinda wenzake wote.

Kwa hivyo, ataweza kushinda katika shindano hilo. Kobe alikwisha kujua ujanja wa Sungura wa kumuona hana mbio. Kwa hivyo, aliwakukusanya ndugu na jamaa zake bila kujulikana na kupata ushindi. Taswira hii inaifunza jamii kuwa penye kutafuta ushidi ni lazima ndugu na marafiki washiriki. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa wanajamii kuwa katika mashindano hawanabudi kujiandaana kujua mbinu za watu wengine ili kupata ushindi.

### **5.9.56 Hadithi ya Simba Mzee na Sungura**

Hadithi ya Simba na Sungura inaifunza jamii kuwa katika maisha kuna wasaliti, wanapokuwa mbele ya watu huonekana kuwa ni watu wema sana lakini wanapokuwa peke yao, hubadilika na kuwasaliti watu. Hadithi inaelezea kuwa simba mzee, hawezi kuwinda. Kwa hivyo, wanyama wengine walimsaidia kumpelekea chakula. Wanyama wote walikubali kumpelekea chakula lakini waligundua kuwa wanapungua. Kila anayepoleka chakula kwa simba mzee, harudi. Sungura alimshutumu kuwa simba mzee kuwa anakula wanyama wanompelekea chakula. Sungura alimtengeneza sanamu. Siku yake ya kupeleka chakula ilipofika, alilipeleka sanamu na simba akalirukia na kutaka kulila. Wanaynma wote walisikia kelele zile na wakaona kuwa simba mzee ndiye anayekula wanyama, wakamuacha mpaka kufa kwake. Taswira ya simba mzee anayekula chakula anachopelekewa na yule anayepolekea inafunza maadili kuwa kuna mashujaa waliozeeka na wanahitaji msaada. Wanapopelekewa, wanasababisha matatizo kwao na kwa wale wanaowapelekea.

Hadithi inafunza maadili kwa jamii kuwa mwanadamu aridhike na kile anachokipata kuliko kutumaini kitu kilicho nnje ye uwezo wake au chenye kuleta hasara. Hadithi inaelezea kuwa simba mzee hakuridhika na chakula alichokuwa anapelekewa ila alithubutu kumla na yule aliyempelekea chakula. Hii si tabia njema kwa wanajamii kupewa kitu cha msaada na baadaye kuleta matatizo kwa yule aliyekuletea msaada. Kwa hivyo, ni vyema kuepukana tabia hiyo. Tatu, hadithi inaifunza maadili kwa jamii kuwa panapotokezea tatizo katika jamii ikiwa ni zuri au baya ni vyema kukutana na kushauriana ili kutafuta ufumbuzi. Wanyama waliamua kumsaidia

simba mzee kwa kumpelekea chakula lakini walijiona wanapungua. Sungura na wanyama wengine walikutana na kujadiliana, mwisho sungura alitegeneza sanamu na kumpelekea simba siku yake ilipofika ya kumpelekea chakula. Simba alilirukia sanamu na wanyama waliokuwa nnje walisikia vishindo na kujua kuwa simba ndiye anayekula wanyama wanapokwenda kupeleka chakula. Kwa jumla hadithi ya simba na Sungura inaifunza jamii kuwa baadhi ya watu ni wasaliti. Jamii iwe na tahadhari na wasaliti. Panapotokezea jambo lolote katika jamii ni vyema kukaa pamoja na kutatua matatizo.

#### **5.9.57 Hadithi ya Mwanamke Aliyeolewa na Zimwi**

Hadithi ya mwanamke aliyeolewa na zimwi inaifunza jamii kuwa mtu anapofika umri wa kuolewa ni vyema kuchunguza tabia za mchumba atakayemuoa kabla ya kufunga ndoa. Hadithi inaelezea kuwa mtoto wa kike aliyekuwa akiishi na mama na baba yake. Kila mchumba aliyekuja kumposa alimkataa na mwisho alipata mwanamme mzuri lakini hakumjua kuwa alikuwa zimwi. Alikaa siku nyingi bila ya kumjua kama mume wake ni zimwi ingawa watu walikuwa wakimwelezea. Ni kweli mwenye mapenzi haoni ijapokuwa macho anayo. Siku moja usiku alipolala, alisikia sauti ikisema, “njoo tule nyama “hapo alibaini kuwa ni mume wake, zimwi. Hadithi inatoa taswira ya zimwi na binadamu. Hii inafunza jamii kuwa ikiwa binadamu mwezako, atukuja na atakakuelezea jambo zuri lakini akalikataa, Mwennyezi Mungu atamletea kiumbe mwengine, kinyume na alivyotarajia. Wakati mwengine huwa ni adhabu. Kijana wa kike, mwisho alibaini kuwa mume wake hakuwa binadamu, ni zimwi. Pili, hadithi inaifunza jamii kuwa wasivutiwe na sura nzuri katika kuchagua mchumba. Tabia njema na maelewano huimarisha ndoa.

Kijana wa kike alitoroka kwa zimwi, mumewe, na kurejea kwao. Sura nzuri ya zimwi inatoa taswira kuwa kuna vijana wengine wanapokwenda kuposa huwa na hadaa za aina mbalimbali. Baada ya ndoa, hadaa zao hujulikana na ndoa huvunjika. Ndoa ni masikilizano mazuri baina ya mume na mke. Tabia zikilingana wawili hudumu milele na milele katika ndoa yao. Tatu, hadithi inafunza maadili kwa jamii kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Wazee wanapokushauri si vizuri akawawapuza.

Kijana anayeyapuza mzee anaweza akaharibikiwa katika maisha yake Kijana wa kike akiishi na wazazi wake, kabla ya kuolewa na Zimwi, majirani walimueleza kuwa mchumba atakayemuowa ni zimwi lakini hakukubali. Aliolewa, akayaona yaliyokuwa yakisemwa na hatimaye akatoroka kwa Zimwi. Kwa hivyo, ni vyema kusikiliza wazazi na majirani zako kabla yakuolewa. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa jamii kuwa si vyema kwa mwanamwari kuchagua mchumba kupita kiasi. Vijana wafuate ushauri wa wazee wao au majirani zao kabla ya ndoa, na wasihadaiwe na sura, ndoa hujengwa na tabia njema na maadili mazuri ya Dini.

#### **5.9.58 Hadithi ya Simba na Sungura**

Hadithi ya sungura na simba inaifunza jamii kuwa ni vyema kuwa kila baada ya muda kufanya tathmini katika maisha yake. Hadithi inaelezea kuwa Sungura na wanyama wengine walikuwa wengi katika msitu lakini walijiona kila siku wanapungua mmoja mmoja. Jambo hilo liliwafanya wawaite wanyama wengine na kufanaya mkutano. Wanyama waligundua kuwa simba anawala wanyama wengine kidogo kidogo. Pili hadithi inawafunza wanajamii kuwa ni lazima wawe wajasiri

katika kutekeleza majukumu mazito katika jamii. Kitendo cha sungura kuelewa kuwa simba ndiye anayewala wanyama wengine kilisababisha kujitolea muhanga ili kutekeleza uamuzi mzito.

Wanyama wengine walishirikiana kumuondosha simba katika msitu. Sungura alikwenda kwa simba na kumuelezea kuwa kwenye kisima kuna mnyama mbaya, na wao wameshindwa. Simba akajiona ana nguvu na akatoka kwenda kisimani. Kila anapomtisha mnyama huyo kisimani na yeye simba anatishwa. Mwisho simba akijitosa kisimani na kuona kuwa hakuna mnyama yoyote. Na alifariki. Huu ulikuwa ni ujasiri wa sungura. Hadithi inafunza maadili kuwa kiongozi anayeogopwa na watu katika jamii, huondoshwa kwa hekima na kupelekwa pahala asipoweza kurudi tena kwao. Kwa jumla hadithi ya Simba na Sungura ina nafasi ya kuifunza jamii kuwa ukubwa wa umbo sio wingi wa maarifa, ujasiri na umoja ni ngao katika jamii, na utengano ni udhaifu.

#### **5.9.59 Hadithi ya Wazee Wakulima**

Hadithi ya wazee wakulima inafunza maadili kwa jamii kuwa kilimo na ufugaji ni muhimu katika maisha. Wazee wawili waliishi kwa kuaminiana. Mmoja ni mkulima na mwingine ni mfugaji. Mfugaji alipoona mazao ya mkulima, aliwapelekea ng'ombe wake usiku na kula mahindi. Mkulima alipeleleza na mwisho akaikamata mifugo iliyokuwa ikila mahindi. Palitokezea ugomvi baina ya mkulima na mfugaji kwa muda mrefu. Hata hivyo, jirani zao, waliwapatanisha na wakasameheya. Pili, hadithi ya wakulima wawili inaifunza jamii ya kuwa wafungaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine ni vyema wakapata eneo la kutosha kwa ajili ya mifugo yao, si hivyo mifugo hiyo inaweza kula mazao ya wakulima na kusababisha

ugomvi mitaani. Kwa jumla hadithi ya wakulima wawili inaifunza jamii kuwa na umoja na ushirikiano, kuepuka usaliti katika jamii. Subira na uvumilivu huleta upendo. Chuki baina ya watu ni adui kwa maendeleo yao.

#### **5.9.60 Hadithi ya Nguruwe na Komba**

Hadithi ya nguruwe na komba inaifunza jamii kuwa Mwenyezi Mungu kawaumba viumbe wake hali tafauti, waridhike na maumbile waliyonayo bila ya kuoneana wivu, choyo na uhasidi. Hadithi inaelezea kuwa nguruwe alimuoneya wivu komba kupanda miti na kuweza kuurukia mti mmoja hadi mwengine. Nguruwe alitamani na yeye apande miti na kurukia mti mmoja hadi mwengine. Mwili wa nguruwe ulivyo, si rahisi kwake kupanda mti au kurukia mti mmoja hadi mwengine. Nguruwe alimwambia komba amfundishe. Akafundishwa kupanda na kurukia miti midogo midogo. Baada ya muda nguruwe bila ya kuambiwa akaaza kupanda miti mikubwa na kutaka kuirukia miti mengine mikubwa. Alipojaribu, alianguka na kuharibika uso, ukapondekapondeka hadi leo. Taswira ya kuwa kila myama anaubo lake inafunza maadili kuwa kazi ya Mwenyezi Mungu haina makosa.

Hadithi inafunza maadili kwa jamii kuwa mtu akitaka kujifunza jambo hutafuta mwalimu akamfundisha. Jambo ambalo hukufunzwa na mwalimu wako. Akilifanya, anaweza akakosea na kupata hasara. Ni vyema kabla ya kufanya ukauliza. Nguruwe alipotaka kujua kupanda miti na kurukia mti mmoja hadi mwengine alikwenda kwa komba. Komba alimfundisha nguruwe kupanda na kurukia miti midogo midogo. Baada ya muda nguruwe akajiona ameshakuwa na uwezo wa kupanda miti mikubwa na kurukia bila ya amri ya mwalimu wake. Alipojaribu akaanguka kifudifudi akapondeka uso.



Hadithi inaifunza jamii kuwa mtu anapojifunza jambo anatakiwa awe makini na asiwe na pupa. Akihitimu jambo dogo, mwalimu wake atamfundisha kubwa. Hadithi inaelezea kuwa nguruwe alipoona tayari keshajua kupanda na kurukia miti midogo midogo, hakungojea kufundishwa kupanda na kurukia miti mikubwa. Nguruwe alipopanda akaanguka kufudufudi pua ikapondeka na mifupa ya uso wake ikavunjika, akawa na mfano wa bonde ambalo kila nguruwe analo mpaka leo. Kwa jumla hadithi ya nguruwe na komba inawafunza wanajamii kuwa waridhike na maumbile ya mwili aliyowaumba Mwenyezi Mungu, wasiwe na wivu wala pupa, katika kujifunza. Mwenye pupa hukosa kila kitu.

#### **5.9.61 Hadithi ya Simba na Mkewe na Sungura na Mkewe**

Hadithi ya Simba na mkewe na Sungura na mkewe inaifunza jamii kuwa unapoona kitu kizuri ujuwe kuwa na wanajamii wengine huwa wameshakiona. Anayetaka jambo ni lazima afanye jitihada ili alipate au anaweza akalikosa. Hadithi inaelezea kuwa Sungura alitafuta sehemu akafyeka ili apate kiwanja cha kujenga nyumba. Baada ya kufyeka kiwanja. Simba alitokezea na akakiona kizuri na kuanza kujenga. Sungura alipokuja akaona maajabu na kuamua kukandika. Simba alipokuja alisema kuwa ni nyumba ya ajabu akaanza kuezeka. Siku iliyofuata sungura na mkewe wakaja wakahamia. Baada ya siku chache, Simba na mkewe akaingia. Wakaelezana na sungura na mkewe. Wote wakahamia pamoja. Kwa hivyo simba na mkewe na sungura na mkewe wakawa wanaishi katika nyumba moja.

Hadithi inaifunza jamii kuwa ni vyema wanapoingia katika maisha ya ndoa wakawa na pahala pa kuishi. Sungura alitafuta pahala akafyeka ili aweze kujenga nyumba na akaishi na mkewe. Simba naye alifanya hivyo hivyo lakini kila mmoja alikuwa

anapojenga hamkutii mwenziwe, walikutana wakati wa kuhamia. Hadithi inaifunza maadili kwa jamii kuwa mafahali wawili hawakai zizi moja. Sungura aliona kuwa simba na mkewe wanasifika porini kwa ukali, kwa hivyo alifanya mbinu ili wahame katika nyumba wanayoishi. Hadithi inaelezea kuwa sungura na mkewe walipanga ujanja. Siku ya kwanza, sungura alimwambia mumewe kuwa anatamani maini ya kifaruru, Simba na mkewe waliyasikia maneno ya sungura na mkewe. Sungura alimletea mkewe maini ya kifaruru ambaye alikuwa amekufa porini. Siku iliyofuata, mke wa Sungura aliagizia maini ya nyati. Sungura alikwenda kutafuta maini ya nyati aliyekufa na kuyaleta. Hali ikaendelea hivyo hivyo, kwa muda. Simba na mkewe wakaona si vyema kukaa na Sungura na mkewe kwani wanaweza kuuliwa. Wakaamua kutafuta pahala pengine pa kuishi.

Hadithi inaifunza jamii kuwa katika ndoa kunahitajika ustahamilivu na umakini. Bibi na bwana lazima washirikiane, wawe kitu kimoja ili waweze kuishi vizuri katika jamii. Sungura na mkewe walijua kuwa hawana nguvu za kumshinda simba na mkewe. Kila mnyama anajua kuwa Simba ana nguvu zaidi kuliko mnyama mwengine. Ushirikiano mzuri na umakini wa Sungura na mkewe uliweza kumuondosha simba na mkewe katika nyumba ya ushirika. Hadithi inafunza kuwa jambo la ushirika huwa halifiki mahala pa zuri. Iko siku, mtu mmoja anaweza kuhama au kudai chake. Inaweza kuwa kwa siri au kwa dhahiri. Hadithi inaelezea kuwa sungura alipoona anataka nyumba iwe yake peke yake, alimfukuza simba na mkewe kwa kisaikolojia. Mbinu ambazo zilimtisha simba na mkewe na kuhama kwa hiari yao. Kwa jumla hadithi inatoa elimu kwa wanajamii kuwa wawe wastahamilivu, umoja na ushirikiano. Kujua kuwa jambo lolote lile bila ushirikiano

linaweza kuharibika na kuleta ugomvi na watu watafute pahala pa kuishi kabla ya kufunga ndoa.

#### **5.10 Maoni ya Wanafunzi**

Wanafunzi 154 kati ya 162 ambao ni sawa na asilimia 95% wamekubali kuwa mwalimu anapowasimulia hadithi simulizi darasani huwa anakusudia dhamira aliokusudia kwa wanafunzi wake ingawa wanafunzi 8 kati ya 162 wamekataa, sawa na asilimia 5%. Wanafunzi 146 kati ya 162 ambao ni sawa na asilimia 90.12% wamekubali kuwa mwalimu anapofundisha hadithi simulizi huwa anazingatia maadili mema ya Kizanzibari hata hivyo wanafunzi 16 kati yao wamekataa, sawa na asilimia 9.8%. Wanafunzi wengi wametaja kuwa mbinu wanazotumia walimu kufundishia ni masimulizi ya mdomo, mbinu ya kuteua mwanafunzi na kuwasimulia wenzake, mbinu ya kutumia picha, redio, kusoma vitabu, kuangalia patananga, mbinu ya kuwalika wazee kutoka mitaani na kusoma kutoka magazetini. Faida ambazo wanafunzi wanazipata wanapofundishwa hadithi simulizi katika kujifunza maadili mema ni kwamba mwanafunzi anakuwa mweledi katika kujua maadili mema na mabaya, huwa na heshima kwa wazee, walimu na wanafunzi wengine katika jamii, pia hukuza vipaji vyao vya akili ili kutatua matatizo mbalimbali katika jamii, huwasaidia kujua historia ya jamii hivyo hufungamana na maadili yaliyomo katika utamaduni wao.

Matatizo ambayo wanafunzi wanaweza kuyapata ikiwa hawafundishwi hadithi simulizi katika kufunza maadili mema ni kwamba wanafunzi watakosa kufahamu vyema historia na utamaduni wa jamii yao na itakuwa rahisi kwao kufuata utamaduni

wa kigeni. Wanafunzi watakosa mapenzi bora kwa wazazi, kwa wanafunzi wengine wanaojifunza darasani na hata katika jamii anayoishi kwa sababu watakuwa na tabia mbaya. Hadithi simulizi zinazofundishwa shuleni ni visasili, vigano, ngano, tarihi, sogu na hekaya. Kiasi cha wanafunzi 116 kati ya wanafunzi 162, sawa na asilimia 71 % wanakubali kuwa mwalimu anapowasimulia hadithi darasani huwa anazingatia vianzio. Vianzio wenyewe ni hivi vifuatavyo:

Hapo kale, palikuwa na ntu na vijitu na watu ndiyo siye,

au

Hapo zamani za kale kulikuwa na .....

au

Hadithi, Hadithi.....

(Hadhira).....Hadithi njoo, ukweli njoo, utamu kolea.

Fanani huendelea:

“ Paliondokea chanjagaa

Kajenga nyumba kakaa

Mwanangu mwana siti

Vijino kama chikichi

Vya kujengea ukuta

Na milango ya kupita

Jiwe zama kupwa eleya.”

au

Paukwa.....Pakawa

au

Paukwa.....Pakawa

Msimuliaji

Nitoe.....nisitoe?

Nianze.....nisianze?

Nisimulie.....nisisimulie?

Asilimia 80.86% ya wanafunzi ambao ni sawa na wanafunzi 131 kati ya 162, wanakubali kuwa mwanafunzi anapowasimulia wanafunzi wengine hadithi simulizi darasani huwa anazingatia maadili mema, hata hivyo, wanafunzi 31 kati ya 162, sawa na asilimia 19% wanakataa hoja hii. Wanafunzi 131 kati ya 162, sawa na asilimia 80.86 % wanasema kuwa muda uliopangwa kwa ajili ya hadithi simulizi hautoshi ingawa wanafunzi 31 kati ya 162 sawa na asilimia 19% wamekubali kuwa, kwa wiki somo la Kiswahili lina vipindi 4 na vinatosha.

### **5.11 Maoni ya Walimu**

Walimu 18 kati ya 18 sawa na asilimia 100 % wamesema kuwa wanapowasimulia wanafunzi hadithi simulizi huwa na dhamira maalumu wanayoikusudia na huzingatia maadili mema ya Kizanzibari kama vile kuheshimu wazee, walimu na wanafunzi wengine, kushirikiana na kusaidiana katika masomo, wakati wa furaha au msiba, kuwa na matumizi mazuri ya lugha katika mazingira ya shule au nyumbani, kujenga uzalendo na kufanya kazi kwa bidii. Kwa kiasi kikubwa maoni haya yanakubaliana na yale yaliyotolewa na wanafunzi. Mbinu anazotumia mwalimu katika kufundisha hadithi simulizi na maadili mema ni mbinu ya masimulizi ya mdomo ya fanani na hadhira, mbinu ya kuteua mwanafunzi na kusimulia, kusoma vitabu au magazetini, kusikiliza redio, kuangalia na kusikiliza

patananga, runinga, mbinu ya matumizi ya picha na mbinu ya kutumia methali kama msisitizo. Maelezo haya yanakubaliana na yale yaliyoainishwa na walengwa wanafunzi.

Faida anayoipata mwanafunzi katika kufunzwa maadili mema ni kujengeka kwa tabia njema na kuwafunza wanafunzi wengine maadili mema, kuwa mdadisi na kukuza kipawa chake cha akili, kuwa na ufasaha na matumizi mazuri ya lugha fasaha na lahaja anayoitumia katika jamii, kuelewa historia ya jamii na kuwa mwepesi katika kutatua matatizo yanayomkabili. Faida hizi zinalingana na zile zizoonyeshwa na walengwa wanafunzi. Matatizo ambayo mwanafunzi anaweza kupata ikwa hatafundishwa hadithi simulizi katika shule za Sekondari ni kuwa anaweza kujiingiza katika tabia na vitendo visivyokuwa vya maadili mema na kutengwa na jamii, atakosa kujua historia ya jamii yake na utamaduni, na nirahisi kujiingiza katika utamaduni wa kigeni, mawazo ambayo yanakubaliana na yale yalitolewa na walengwa wanafunzi.

Hadithi simulizi zinazofundishwa shule za sekondari ni soga, tarihi, hekaya, vigano, ngano na visasili. Hadithi pia zimetajwa na walengwa wanafunzi. Asilimia 88% ambayo ni sawa na walimu 16 kati ya 18 wamekubali kuwa wanapofundisha hadithi simulizi huzingatia vianzio vya hadithi. Maelezo haya yanakubaliana kwa kiasi kikubwa na yaliyotolewa na walengwa wanafunzi. Asilimia 94% ambayo ni sawa na walimu 17 kati ya 18 wanaunga mkono hoja kuwa mwanafunzi anaposimulia hadithi simulizi wanafunzi wengine huwa wanazingatia maadili mema ya Kizanzibari. Hata hivyo asilimia 6% ambayo ni sawa na mwalimu 1 kati ya 18

anakataa hoja hii. Maelezo haya pia yanathibitishwa na walengwa wanafunzi kwa kiasi kiubwa. Walimu 14 kati ya 18 ambao sawa na asilimia 77.7% wamesema kuwa muda wanaotumia kufundishia hautoshi. Wazo hili pia linakubalika na walengwa wanafunzi kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo asilimia 22.3% wameona kuwa muda huo unatosha. Kwa wiki ni vindi 4, kila kipindi kinachukua muda wa dakika 45 au 35. Vipindi hivyo 4 ni kwa somo zima la Kiswahili.

### **5.12 Maoni ya Wazee**

Asilimia 97% ya wazee ambao ni sawa na wazee 65 kati ya 67 wamekubali kuwa wanapowasimulia hadithi simulizi watoto/wajukuu wao nyumbani huwa wanazingatia maadili maalumu. Maelezo haya, kwa kiasi kiubwa yanakubaliana na mawazo ya walengwa walimu na wanafunzi. Hata hivyo asilimia 3% sawa na wazee 2 kati ya 67 wanakataa hoja hii. Lengo ni kuwafunza maadili mema na kuzingatia mila na desturi za jamii. Wazee huwa na madhumuni ya kuwaweka watoto wao pamoja, kuwaelimisha umuhimu wa kuishi pamoja, kushirikiana na kuhifadhi historia ya jamii. Mbinu wanzotumia wazee katika kusimulia hadithi simulizi na maadili mema ni masimulizi ya mdomo, kuchagua mtoto mwenye kujua hadithi na kuwasimulia wengine na mbinu ya kusoma kitabu. Mbinu hizi ni kidogo sana ulinganisha na mbinu tisa zilizotajwa na walengwa walimu na wanafunzi. Matatizo ambayo mtoto anayapata anaposimuliwa hadithi isiyokuwa na maadili mema ya kizanzibari ni kuwa hupoteza asili na utamaduni wake, huwa mkaidi kufuata ushauri wa wazee na hutengwa na baadhi ya watu katika jamii. Mawazo haya yanakubalina na ya walengwa wanafunzi na walimu. Mtoto anapowasimulia hadithi watoto wengine nyumbani huwa anazingatia maaadili ya Kizanzibari kwa sababu huwa

anasimulia hadithi ambazo amesimuliwa na wazee, walimu au wanajamii ambazo huwa na mafunzo maalumu. Maelezo haya yanalinga na yale yaliyotolewa na walengwa walimu na wanafunzi. Hata hivyo, mtoto anaweza kuengeza lake. Wazee wengi wameeleza kuwa kuna hadithi za aina nyingi. Hadithi ambazo wamezitaja ni hekaya, ngano, sogu na visakale. Hadithi hizi ni kidogo, ukilinganishana zile zilizotajwa na walengwa walimu na wanafunzi.

Kwa jumla utafiti huu ulikuwa na lengo la kujadili nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za sekondari, Visiwani Zanzibar. Utafiti umetumia mbinu ya kiwango na ujumla. Maswali ya utafiti yamegawika katika makundi makuu matatu, walimu, wanafunzi na wazee. Kwa upande wa walimu kulikuwa na maswali manne. Kwanza, utafiti ulitaka kujua kuwa mwalimu anapowasimulia hadithi simulizi wanafunzi darasani huwa anafuata dhamira maalumu anayokusudia kwa wanafunzi wake. Pili, kujua ni mbinu gani anazotumia katika kufundisha hadithi simulizi na maadili mema. Tatu, kujua kuwa anaposimulia hadithi simulizi darasani huwa anazingatia vianzio vya hadithi. Nne, muda aliopangiwa kufundisha unatosha au hautoshi. Kwa upande wa mwanafunzi, utafiti ulitaka kujua mambo manne. Kwanza utafiti ulitaka kujua kuwa wanapofundishwa hadithi simulizi zinazingatia maadili mema ya Kizanzibari. Pili, ni faida gani wanazozipata wanapofundishwa hadithi simulizi katika kufunza maadili mema visiwani Zanzibar. Tatu, ni matatizo gani ambayo wanayapata ikiwa hawafundishwi hadithi simulizi zenye kufunza maadili mema. Nne, ni aina gani ya hadithi simulizi na maadili mema zinazofundishwa shule za sekondari. Kwa upande wa wazee, utafiti ulitaka kujua mambo manne. Kwanza, wazee wanapowasimulia hadithi simulizi watoto/wajukuu



wao nyumbani wanafuata maadili maalumu wanayokusudia kwa watoto au wajukuu wao. Pili, ni mbinu gani wanazotumia wazee wanapowasimulia hadithi simulizi na maadili mema Visiwani Zanzibar. Tatu, ni matatizo gani wanayoyapata watoto wanaposimuliwa hadithi isiyokuwa na maadili mema ya Kizanzibari. Nne, watoto wanapowasimuliwa hadithi simulizi na watoto wengine nyumbani kwao huwa wanazingatia maadili mema ya Kizanzibari.

### **5.13 Uchambuzi wa Vianzio vya Hadithi Simulizi**

5.13.1 Tasnifu ya Sengo, imeelezea maana ya “Paukwa.....Pakawa” kuwa “paondokwapo.....hukaliwa”. Utafiti umebaini kuwa katika hadithi simulizi za Visiwani Zanzibar kuna kianzio ambacho kimejitokeza kubeba dhima na maadili mema kwa wazee, walimu na wanafunzi kama ifutavyo:

Paukwa.....Pakawa

Hadithi, Hadithi.....

(Hadhira).....Hadithi njoo, ukweli njoo, utamu kolea.

Fanani huendelea:

“Paliondokea chanjagaa

Kajenga nyumba kakaa

Mwanangu mwana siti

Vijino kama chikichi

Vya kujengea ukuta

Na milango ya kupita

Jiwe zama kupwa eleya.”

Katika kianzio hiki kilichojikita kama ushairi, kina lugha teule ya mnato, mguso, mvuto na kulisimua hisia za hadhira kimebeba dhima na maadili mema. Kuna taswira zilizojitokeza ambazo zinatoa dhima na maadili mema kwa hadhira inayosikiliza hadithi simulizi. Kwanza ni “Palitokezea chanjagaa”, hawa ni wanyama mfano wa kaa wenye vilemba vyeupe, wanakaa baharini lakini huja ufukweni na kuvamia ufukwe kwa makundi. Huvamia pahala pasipokuwa pao na kufanya makaazi yao, hujenga nyumba na kuizungushia ukuta kwenye ufukwe. Katika nyumba zao hutoboa vishimo katikati, akitokezea kiumbe yoyote ni rahisi kujiingiza ndani ya nyumba yake. Maji yakijaa ufukweni, ukuta aliojenga hubomoka na nyumba huingia maji. Chanjagaa huzama ndani ya maji na kuendelea kuishi bila ya matatizo. Maji yanapotoka ufukweni, chanjagaa hucheza karibu na nyumba yake. Anapotokezea mtu, chanjagaa hukimbia na kujificha katika vishimo. Ujanja wa chanjagaa huwasaidia kuishi pahala pasipokuwa pao kwa muda wa miaka mingi. Pili, dhima na maadili mema yanayojitokeza katika mistari minne inayofutatia:

“ Mwanangu mwana siti

Vijino kama chikichi

Vya kujengea ukuta

Na milango ya kupita”

Taswira inayojitokeza hapa kwanza ni “mwana siti”, msimuliaji anawataka hadhira yake wasikate tamaa kwa kile kilichowapotea au kuchukuliwa na chanjagaa kwa sababu kila chenye mwanzo hakikosi kuwa na mwisho. Mwana siti ni mchikichi ambao hukua na kuzaa, baada ya kuzaa umbile lake hubadilika kutokana na uzazi. “Vijino kama chikichi” hii ni taswira ambayo iko katika chikichi, ukiibanja

huvunjika vunjika, vipande vyake hukaa kama vijino vya mtoto. Chikichi iliyozeeka na kuwa kavu. Hizi huwa ndani hazina nyama imeshaliwa na wadudu, huwa kama ukuta uliotobolewa mlango, hausaidii kuzuia kitu kinachoingia ndani au kutoka nje. Chikichi mbovu haziwezi kuwa mbegu za kuotesha mmea mwengine, kilichobakia huwa mlango wa kupita. Kwa hivyo msanii huwa amekusudia kuwaambia hadhira kuwa ni vyema kuutumia umri wa ujana vizuri kabla ya kufika uzeeni. Uzee ukiigia mwilini unahitaji msaada wa vijana au wajukuu. “Na huu ndio ukweli unaojitokeza katika kiitikio” (ukweli njoo). Taswira ya ” jiwe zama kupwa eleya”, kawaida ya jiwe huzama kwenye maji lakini maji yakitoka ufukweni mwa bahari, jiwe hueleya au kuonekana kwa hivyo na chajagaa anapewa ujumbe kuwa ataonekana ufukweni kama jiwe linavyooneka wakati wa maji kupwa.

Kwa jumla fanani huwa anawaelimisha hadhira maadili mema kuwa walikuja watu katika kiambo wakaa, wakajenga, wakazaa, na walipokuja wenyeji walikuta wahamiaji. Pili, wasiwe na tabia ya kukata tama kwa kitu kilichwapotea au kuchukulliwa. Tatu, watumie ujana wao katika kufanya mambo mema yatakayowasaidia watapokuwa wazee. Mwisho msimuliaji anaitaka hadhira waelewe kuwa kila lenye mwanzo lina mwisho.

## SURA YA SITA

### 6.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.1 Hitimisho

Utafiti huu umefanyika katika Mkoa wa Mjini-Unguja, Wilaya ya Kaskazini A-Unguja. Utafiti pia umejumuisha katika Wilaya ya Wete na Kusini-Pemba. Kwa jumla utafiti umefanyika katika Wilaya nne, Unguja na Pemba. Matokeo na mapendekezo ya utafiti ni kama ifutavyo:

#### 6.2 Madhumuni ya Utafiti

##### 6.2.1 Madhumuni ya Kwanza ya Utafiti

Kwanza ni Kuzikusanya hadithi simulizi mbalimbali kutoka kwa wanafunzi, wazee na walimu wa Kizanzibari na kuzichambua ili kutafiti dhima zilizomo na jinsi zinavyoweza kuathiri malezi ya kimaadili mema shule za Sekondari visiwani Zanzibar. Madhumuni haya yaliongozwa na swali la kwanza, Je, hadithi ni nini na zina nafasi gani katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar?

Katika kuzikusanya hadithi simulizi za vigano, sogu na ngano (zimo katika kiambatanishi cha iv), dhima zilizomo zinaweza kuathiri malezi ya maadili mema katika shule za Sekondari za Zanzibar hasa pale zinaposimuliwa na msimuliaji, ikawa wasikilizaji wanasikiliza kwa makini dhima na maadili mema yanayojitokeza. Pia utafiti umeweza kujibu swali la hadithi kuwa ni usanii wa masimulizi ambao husimuliwa kwa njia ya mdomo na kuhifadhiwa kwa kichwa kutoka mtu mmoja hadi

mtu mwengine. Hadithi hizi zina nafasi kubwa katika kufunza maadili mema shule za Sekondari kisiasa, kiuchumi, kijamii na kifamilia. Hadithi inaposimuliwa na msimuliaji akiwa ni mzee, mwalimu au mwanafunzi hufutana na hisia na matendo ya msimuliaji, mafunzo na maadili mema yaliyomo huwaathiri wasilizaji katika shule au jamii yao.

### **6.2.2 Madhumuni ya Pili ya Utafiti**

Ni kuainisha maadili mema mbalimbali ya hadithi simulizi yenye mafunzo mema kwa wanafunzi wa shule za Sekondari za Zanzibar ambayo ni makuzi ya mtoto, wema na ubaya, elimu, umoja na ushirikiano, ndoa na starehe, uongozi, kilimo na biashara, urafiki, dini na imani, mapenzi na tabia njema, sheria na malezi, itikadi za kijamii, usaliti, wivu na choyo. Madhumuni haya yaliongozwa na swali la pili. “Je, kuna mikabala ya aina ngapi ya maadili mema katika hadithi simulizi inayoweza kutolewa na wazee, walimu, na wanafunzi wa shule za Sekondari, Zanzibar?” Jibu ni kwamba kuna mikabala tisa ambayo imeainishwa katika majedwali (angalia uk. xi).

### **6.2.3 Madhumuni ya Tatu ya Utafiti**

Ni kutafiti mbinu mpya na muda wa kufundishia hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar ili kuwashawishi wanafunzi wengi wa shule za Sekondari kupenda kujifunza hadithi Simulizi kwa urahisi. Madhumuni haya yaliongozwa na swali tatu “Ni mbinu gani za hadithi simulizi zinazotumika katika kufunza maadili mema kwa wanafunzi wa shule za Sekondari, Visiwani Zanzibar?” Utafiti umebaini kuwa mbinu zinazotumika ni masimulizi ya mdomo baina ya msimuliaji na msikilizaji. Fanani na hadhira wanaonana uso kwa

uso, mbinu ya kuchagua mwanafunzi, mbinu ya kutumia mchoro na maelezo, patananga, runinga na video, redio, vitabu, magazeti na mbinu ya kutumia methali kama msisitizo. Na hakuna muda uliopangwa kwa ajili ya kufundisha hadithi simulizi. Muda ulioko katika shule ni vipindi sita kwa kufundishia somo zima la Kiswahili Sarufi na Fasihi.

#### **6.2.4 Madhumuni ya Nne ya Utafiti**

Ni kuwashauri walimu wa shule za Sekondari kutumia mbinu za kisayansi na teknolojia katika ufundishaji wa hadithi simulizi ili kukuza kiwango cha elimu shule za Sekondari. Madhumuni haya yaliongozwa na swali. “Ni ugumu upi wa kutumia hadithi simulizi katika kuwafunza maadili mema wanafunzi wa shule za Sekondari Visiwani Zanzibar?.” Utafiti umebaini kuwa hadithi simulizi zinakabiliwa na athari za utandawazi na kudharaulika kutokana na vyombo vya habari kama T.V, wavupepe na patananga katika jamii ambazo huonyesha fasihi simulizi za kigeni zaidi kuliko za wenyeji. Wanafunzi ambao wamo katika jamii huchotwa na akili za kukubali kuwa fasihi simulizi za kigeni ni kigezo cha usasa, maendeleo na mafanikio. Pili, wanafunzi wanaposoma hadithi simulizi ziliyoandikwa kwenye kitabu au maadishi wanayakosa mambo yafuatayo:

- (i) Hawapati kumuona fanani akitumia viungo vyake vya mwili akisimulia, kwa hivyo hukosa kuona msisitizo wa maadili yanayotakiwa kama mema au mabaya.
- (ii) Panapotokezea hisia za huzuni au furaha ni vigumu kwa wanafunzi wanaosoma hadithi simulizi kwenye kitabu kuziona. Hisia hizi huonekana zaidi kwa macho au uso kwa uso baina ya fanani na hadhira.

- (iii) Msimuliaji wa tokeo anapochukua nafasi ya muhusika ndani ya hadithi simulizi, maigizo na vitendo hubeba dhima na maadili. Hali hii si rahisi kuiona kwenye maandishi kama inavyojitokeza katika masimulizi ya ana kwa ana.
- (iv) Wasikilizaji hukosa nafasi ya kutenda au kushiriki wanaposoma hadithi simulizi iliyoandikwa.

### **6.3 Lengo Kuu la Utafiti**

Ni kujadili nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Katika kufanikisha lengo hilo, utafiti umetumia mbinu ya Maktabani, shirikishi, mahojiano ya ana kwa ana, na mbinu ya kutumia mtafiti msaidizi. Mbinu hizi zimemsaidia mtafiti kufikia lengo.

### **6.4 Nadharia Mbalimbali Zimetumika Kufanikisha Utafiti Huu**

Nadharia hizo zimegawika katika mikabala miwili. Kwanza, mtafiti ametumia nadharia ya Ndani-Nnje, ya mkabala wa kiislamu, ya fasihi na jamii, ya dhanna ya muundo na ya hisia katika uchambuzi wa data. Pili, kuna nadharia ambazo zimemuongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data na kufikia lengo, hizi ni nadharia ya saikolojia ya tiba, umithilishaji, ushunuzi-chambuzi, ya ubadilikaji, ya utamaduni, ya kijamii, ya kimaendeleo, ya msambao, ya uhalisia, ya uamilifu, ya maneno, ya ubunifu na ya tajriba ya maisha. Mwisho, kumbainika kuwa hadithi simulizi zina nafasi kubwa katika kufunza madili mema Shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Hadithi hurithishwa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine, kwa hivyo maadili mema yanakwenda sambamba na jamii na mahitajio yake. Utanzu wa hadithi simulizi hutumika kuifunza jamii maadili mema kwa watoto na watu wazima.

## 6.5 Mapendekezo ya Utafiti

- (a) Hadithi simulizi zina nafasi kubwa katika kufunza maadili mema, Shule za Sekondari nchini. Zitumike katika kutatua matatizo ya kielimu, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni Visiwani Zanzibar. Kutumika kwake kutasaidia jamii ya Wazanzibari kuishi vyema.
- (b) Hadithi simulizi zina mvuto kwa watoto na watu wazima. Ni vyema ziendelezwe kufundishwa na wazee ili ziendele kutunza maadili mema kwa jamii ya Wazanzibari.
- (c) Wazazi hawana mbinu za kutosha za kitaalamu za kuwasimulia watoto wao kwa hivyo ni vyema kujenga ushirikiano imara na walimu ili wanafunzi wafundishwe hadithi simulizi kwa kutumia mbinu tafauti za kitaalamu katika Shule za Sekondari.
- (d) Hadithi za ngano ni chache katika jamii na hakuna vitabu vya kutosha vya kufundishia hadithi simulizi na maadili mema, Visiwani Zanzibar. Ni vyema wataalamu wa fasihi kuzihifadhi katika kanda za ( c.d ) na kuandika vitabu mbalimbali vya kufundishia hadithi simulizi katika Shule za Sekondari.
- (e) Somo la Kiswahili lina muda mchache wa kufundishia Shule za Sekondari, kwa hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iengeze muda na ifikie vipindi vinane kwa wiki. Vinne vya fasihi na vinne vya sarufi ili walimu wa somo la fasihi wawe na muda wa kutosha wa kuwafundisha hadithi simulizi na maadili mema. Katika kufundisha fasihi, wawepo walimu maalumu wa kufundisha hadithi simulizi.
- (f) Walimu wanaofundisha madarasa ya elimu mjumuisho katika shule za Sekondari washauriwe kutumia mbinu ya kuteua msimuliaji au kusikiliza



hadithi zilizohifadhiwa katika kanda za (c.d) ili kuwahamasisha wanafunzi walemavu wa macho na wale wasiokuwa walemavu darasani.

- (g) Walimu wa shule za Sekondari wawafafanuliye wanafunzi wao dhima na maadili mema yanayojitokeza katika vianzio vya hadithi simulizi.
- (h) Wazee waandae utratibu maalumu wa kusimulia hadithi simulizi katika shule za Sekondari Visiwani Zanzibar kwa kupitia kamati za shule.
- (i) Wataalamu wengine waendeleo kufanya utafiti wa hadithi simulizi za hekaya, visasili n.k.

## MAREJELEO

- Alex, N. (2005). *Fasihi simulizi kwa shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Ali, K. B. (2007). “Tasnifu ndogo, Baadhi ya maneno ya Kiswahili Sanifu na athari katika kuandikwa yasivyotamkwa”. Zanzibar: SUZA
- Ali, Z. H. (2005). “Tasnifu ndogo, Athari za nyimbo za kale za harusi katika ndowa za Wazanzibari”. Zanzibar: SUZA
- Ali, S. K. (2007). “Tasnifu ndogo, Athari za usasa katika lahaja ya Kitumbatu asiliya”. Zanzibar: SUZA,
- Ali, H. B. (2008). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya mwanamke katika hadithi simulizi za Fasihi simulizi za lugha ya Kiswahili”. Zanzibar: SUZA.
- Ali, H. A. (2008). “Tasnifu ndogo. Nafasi ya mwanamke katika hadithi za Fasihi Simulizi za lugha ya Kiswahili”. Zanzibar: SUZA
- Al-Barwan, A. (1996). *Conflict and Harmony in Zanzibar*. Zanzibar.
- Al-Ismaily, I. (1999). *ZANZIBAR, Kinyanganyiro Na Utumwa*. Muscut: Ruwi.
- AI-Ismaily, M. (h.t). *Malezi Mema, Sultanate of Oman*. Muscut: Ruwi
- Adam, H. (2001). *Masimulizi kamilifu ya Alfulela Ulela*, Toleo nambari 1. DSM: Mkuki na Nyota Publishers
- Adam, H. (2004). *Masimulizi kamilifu ya AlfuLela Ulela*, Toleo nambari 3. DSM: Mkuki na Nyota Publishers.
- Afro, S. P. (1973). *Historia fupi ya Zanzbar*. Kimeandikwa na Idara Kuu ya A. S. P, Elimu: Zanzibar.
- Ayany, G (1983). *A history of Zanzibar* : Nairobi, Kenya literature Bureau.

- Balisidiya, M. L. (1987). Tanzu za Fasihi Simulizi, *Mulika 19*, DSM: TUKI.
- Balisidya, M. L. (1977). “Mabadiliko katika Fashi Simulizi ya Wagogo”. Tasnifu, DSM: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Bakari, K. (2007). *Kiswahili Cha Asili Cha Kina Mama Wa Visiwani Zanzibar*
- Ben, A. D. (1975). Folklore in African Society. *Research in African Literature*, Vol.6 na 2 p. 167
- Dhilali, D. A. (2005). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya Tamthiliya katika jamii ya leo ya Kiunguja”. Zanzibar: SUZA
- Farsy, M. (h.t). *Seyyid Said Bin Sultan*. Mongozi Printing Press
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Afrika*. Nairobi: Oxford University Press.
- Finnegan, R. (1989). *Oral Traditions and the Verbal Arts: Aguide to Research Practices*. London and New York: Routledge.
- Haji, N. M. (2007). “Tasnifu ndogo, Matatizo ya ufundishaji wa fasihi andishi katika Shule za wilaya ya Mjini Unguja”. Zanzibar: SUZA.
- Haji, A. I. na Wenzake (1983). *Fasihi simulizi*. DSM: Publishing House
- Haji, H. G. (2004). *Ujanja wa Sungura*. DSM: Oxford University Press.
- Haji, H. G. (2004). *Nahodha Chui*. DSM: Oxford University Press Ltd
- Haji, M. M. (2007). “Tasnifu ndogo, Sababu zinazopelekea utatanishi katika matamshi katika lugha ya Kiswahili”. Zanzibar: SUZA.
- Hamad, F. A. M. (2005). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya visasili katika jamii ya leo ya Wazanzibari”. Zanzibar: SUZA.
- Hassan, H. H. (2005). “Tasnifu ndogo, Matatizo ya tahajiya ya Kiswahili na mtazamo wa Waswahili wasiojua kusoma na Kuandika”. Zanzibar: SUZA.
- Hassan, F. A. (2007). “Tasnifu ndogo, Nyimbo za msanja na athari zake katika mashairi ya mke na mume katika kijiji cha Jambiyani”. Zanzibar: SUZA.

<http://www.augustana.edu/users/sontarawangwi/uhakiki>.

<Http://www.ajol.info./index./php/kcl/article/viewFile/61390/49476> –

<http://ResearchKenya.org.html?search=Folklore&P=20>

<http://www.kiswahili.gskool.com/simulizi.htm>.

<http://www.kiswahili.gafkosoft.com/fasihi-simulizi/hadithi>

<http://www.bing.com/search?q=skinner+learning>.

<http://alleeshadowtradition.com/realism.html>.

<http://www.britainunlimited.com/Biogs/Darwii>

<http://www.ping.com/search?q=john+Locke+big>.

<http://lectureguru.net/courses/theory/struct>.

<http://www.big.com/seach?q=Boris+Tomashev>.

<http://en.wikipedia.org/wiki/EverettRogers#Er>

<http://www.ifeas.un-main.de/swaFo/SF-14-11%20...>

Iddi, R. M. (2007). “Tasnifu ndogo, Mafundisho ya kiislamu yanayojitokeza katika baadhi ya methali za Kiswahili”. Zanzibar: SUZA.

Iddi, Z. A. (2005). Tasnifu ndogo, Utani katika jamii ya Wazanzibari, Zanzibar: SUZA

Issa, H. na wenzake (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi Simulizi*. Zanzibar: TAKILUKI

Juma, N. H. (2008). “Tasnifu ndogo, Kiini cha matumizi madogo ya istilahi za Kiswahili katika TVZ”. Zanzibar: SUZA

Juma, R. P. (2008). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya nyimbo za unyango katika jamii ya Wazanzibari”. Zanzibar: SUZA.

- Juma, H. K. (2007). "Tasnifu ndogo, Matatizo yanayomkakabili mfasiri wa lugha ya Kiingereza kwa Kiswahili". Zanzibar: SUZA.
- Kaloris, S. (1992). *Mgeni wa Bundi*. Tanzania: Kagera Writers and Publishers Cooperative Society Ltd.
- Kamera, W. D. (1978). *Hadithi za Wairaqw wa Tanzania*. Arusha, Tanzania: EALB
- Kiango na Wenzake, (2007) *Kamusi ya shule za Msingi*: Kenya, Exford University Press
- Kimani, N na Rocha, C (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Kirumbi, P. (1977). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungway
- Khamis, S. A. M. (1983). "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania", *MULIKA* 15:3-15, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Khamis, M. M. (2007). "Tasnifu ndogo, Ukungwi katika harusi za Wazanzibari". Zanzibar: SUZA
- Kothari, C. R (1985) *Research Methodology*. Wiley Eastern Limited: New Delhi
- Koul, L. (1984), *Methodology of Educational Research*: Vokas Publishing House, PUT Ltd: New Delhi.
- Krain, E. (1998) *Agrarian Constitution of Zanzibar and its impact on Agricultural Development*, Germany: Born, Wehi.
- Masebo, J. A na Nyangwine, N (2002) *Kiswahili kidato cha tatu na cha nne*. Afroplus Industries Ltd, DSM
- Masoud, F. A. (2005). "Tasnifu ndogo. Nafasi ya Visasili katika jamii ya leo". SUZA: Zanzibar.
- Makame, A. A. (2007). "Tasnifu ndogo, Matumizi ya Kiswahili Sanifu kwa watangazaji wa sauti ya Tanzania Zanzibar". Zanzibar: SUZA.

- Makame, K. O. (2005). “Tasnifu ndogo, Uhusiano wa vitendawili na masomo mengine yanayofundishwa katika Shule za Zanzibar”. Zanzibar: SUZA
- Mwansoko, D. na Mdee, J. (2003). *Mulika* na. 15. Dar es Salaam: Taasisi Ya Uchunguzi Wa Kiswahili.
- Mbarouk, A. (1983). *Fasihi Simulizi ya Zanzibar, Nyimbo na Michezo ya Watoto*. Dar es Saalam: Tanzania Publishing House.
- Mbarouk, S. S. (2007). “Tasnifu ndogo, Mbinu mchanganiko za ufundishaji wa uhakiki fasihi kwa ufahamu wa wanafunzi”. Zanzibar: SUZA.
- Mbarouk, S. S. (2005). Tasnifu ndogo, Nafasi ya Methali za Kiswahili katika maisha ya kila siku ya Wazanzibari, Zanzibar, SUZA.
- Mbunda, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi Fupi*. DSM: Dar es Salaam Univesity Press
- Mbunda, F. L. (1996). *Mbinu za kufundishia lugha ya Kiswahili*. DSM: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania
- Mdungu, A. M. (2007). “Tasnifu ndogo, Mafunzo ya nyimbo za Singarimbwa katika jamii ya Watumbatu”. Zanzibar: SUZA.
- Mlacha S. na Hurskainen, A. (1995). *Lugha Utamaduni na Fasihi simulizi ya Kiswahili*. DSM: TUKI.
- Mulokozi, M. (1989). *Mulika* na. 21:5, DSM: TUKI
- Mussa, S. T. (2008). “Tasnifu ndogo, Hadhi ya nyimbo ya michezo ya watoto katika wilaya Mjini katika zama za utandawazi”. Zanzibar: SUZA
- Mussa, F. K. (2007). “Tasnifu ndogo, Mchango wa suala la ukombozi katika riwaya ya Shafi Adam Shafi”. Zanzibar: SUZA.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. DSM: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. (1991). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI

- Mulokozi, M. M. (1989). *Mulika na 21.DSM* ; TUKI
- Mvungi, T. A. (2010). *Kiswahili Kidato cha Kwanza na cha pili*. DSM: Ben and Company Ltd.
- Mzee, A. F. (2007). “Tasnifu ndogo, Ufanisi katika usomesaji na usomaji wa somo la Kiswahili kwa walimu na wanafunzi wa kitado cha nne shule za Mchipuo”. Zanzibar: SUZA.
- Ndere, A. (2003). *Fasihi Simulizi*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Ndungo, C. M (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Universiy of Nairobi
- Neuman, W. L. (2000). *Social Research Methods Qualitative and Quntitative Approaches*. Beston: Allyn and Backon.
- Ngure, A. (2004). *Fasihi Simulizi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Njogu, K. na Chimera (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Ltd.
- Ramadhan, S. K (2007). “Tasnifu ndogo, Uhakiki wa nafasi ya mwanamke kataka vitabu vya mashairi ya Shaban Robert na Muhamed Seif Khatib”. Zanzibar: SUZA
- Salim M. Z (2007),”Tasnifu ndogo, Hali halisi ya matumizi ya mbinu za kufundishia sarufi ya Kiwsahili katika shule za Sekondari.’ Zanzibar: SUZA
- Salim, S. R (2007). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya kasida za Kiswahili kwa jamii ya Wazanzibari”.Zanzibar: SUZA
- Salim, Z. A (2007). “Tasnifu ndogo, Changamoto juu ya ufundishaji wa Fasihi Simulizi katika Shule za Sekondari”.Zanzibar: SUZA
- Said, A. A (2007). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya mwanmke katika hadithi fupi za mwandishi Said Ahmed Mohd ukilinganisha na jamii ya Kizanzibari”.Zanzibar: SUZA
- Said, A. S ((2005). “Tasnifu ndogo, Nafasi ya methali kwa vijana kwa vijana wa Kizanzibari wasiosoma shule wala madrasa”. Zanzibar: SUZA

- Said, D. A (2005). "Tasnifu ndogo, Mafunzo ya ngano katika jamii ya Wazanzibari". Zanzibar: SUZA
- Sengo, T. S. Y (1985). "The Indian Ocean Complex and the Folklore The case of Zanzibar Tale Performance Khartom, UN. Published PHD Dissertation Department of Folk lore", IAAS: University of Khartom.
- Sengo, T na Njole, S (1996). Fasihi simulizi ya Mtazania.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI
- Sengo, T na Njole, S (1993). Fasihi simulizi ya Mtazania.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI
- Sengo, T (1981). *Kiklio cha haki*. Nairobi: Longman
- Sengo, T.S. Y (1998) *Kitambulisho cha Uprofesa*, Copytex: Mbale
- Senkoro, F. E. M.K. (1997). "The Significance of the Journery Motif in Forktales, Tasnifu ya Udaktari wa Falsafa" Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Shaaban, M. S (2007) "Tasnifu ndogo, Nafasi ya mwanamke katika tamthilia za mwandishi Penina Muhando".Zanzibar: SUZA
- Songonyi, E. M (1997). *Oral Literature*. Dar es Salaam:The Open University of Dar es Salaam
- Suleiman, S. A (2005). "Tasnifu ndogo, Nafasi ya Maudhui ya nyimbo za Taraab katika jamii ya Zanzibar ya leo"Zanzibar: SUZA
- Taasisi ya Elimu Tanzania (1996). *Kiswahili kidato cha kwanza, kitabu cha mwanafunzi*.Dar es Salaam:Oxford University Press
- TAKILUKI (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Sweden: Artov
- TAKILUKI (1982). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*.Sweden: Artov



- TAKILUKI (1983). *Fasihi Simulizi* . Dar es Salaam:Tanzania Publishing House
- Temu, C. W na Mbogo, E (1987). *Mulika*, na. 19. DSM: TUKI
- Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publication Ltd
- Wamitila, W (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*: Nairobi; Focus Publication Ltd
- Wamitila, W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focu Publications Ltd.
- Wayne, K. hoy and Cecil T. Miskel (1991) Educational Administration, Theory, Research and Practice Fouth Education U.S. A. Mc Graw – Hill
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (2011). “Table namba (25a), (25b), (25c) Drop-out by Standard, sex and Distric in Basic Schools- October, 2004” Zanzibar
- Zanzibar Leo* (11/5/2011). “Kuchoma moto vibanda Pwani Mchangani”, Zanzibar
- Zanzibar Leo* (15/5/2011), “Utalii Zanzibar unachangia mapato”, Zanzibar
- Zanzibar Leo* (17/5/2011), “Kupotea kwa kiasi cha maadili, Kusini Unguja”, Zanzibar.
- Zanzibar Leo* (21/5/2011), “Kuporomoka kwa maadili katika shule na taasisi za elimu”, Zanzibar
- Zanzibar Leo* (24/5/2011). “Matemwe haiko salama kimaadili”, Zanzibar.
- Zanzibar Leo* (24/5/2011). “Kupata ujauzito na kuacha masomo”, Zazibar.
- Zanzibar Leo* (29/5/2011) “Kuondolewa kwa vipindi vichafu vyenye maadili machafu kwa wanafunzi”, Zanzibar.
- Zanzibar Leo* (12/6/2011), “Utandawazi”, Zanzibar.
- Zanzibar Leo* (15/6/2011), “Wafanyakazi mahotelini Paje”, Zanzibar.

*Zanzibar Leo* (19/6/2011) “Utalii”, Zanzibar

*Zanzibar Leo* (21/6/2011), “Ulinzi shirikishi wapunguza dawa za kulevya Mlandege”.Zanzibar

*Zanzibar Leo* (22/6/2011), “ Polisi wayabana magunia ya bangi”, Zanzibar

*Zanzibar Leo* (24/6/2011). “Talaka za ndoa zimeengezeka sana katika jamii”, Zanzibar.

*Zanzibar Leo* (27/6/2011), “Jamii lazima zikae vizuri kukabiliana na mamba wa utotoni”, Zanzibar.

## VIAMBATANISHI

### Kiambatanishi I: Maswali ya ana kwa ana na walimu

**1. Mwalimu**

Jina lako.....

Shule unayosoma/unayosomesha.....

Umri wako.....

Unapoishi.....

Tarehe ya kuelezea hadithi.....

**2. Mwalimu anapowasimulia hadithi simulizi wanafunzi darasani huwa anafuata dhamira maalumu anayokusudia kwa wanafunzi wake?**

Ndiyo----- hapana -----

**3. Mwanafunzi anapofundishwa hadithi simulizi huwa zinazingatia maadili mema ya Kizanzibari? Ndiyo -----Hapana-----**

Yataje.....

.....

.....

**4. Ni mbinu gani anazotumia mwalimu katika kufundisha hadithi simulizi na maadili mema, Visiwani Zanzibar?**

Zitaje.....

.....

.....

5. Ni faida gani anayoipata mwanafunzi anayefundishwa hadithi simulizi katika kufunza maadili mema, Visiwani vya Zanzibar?

Elezea.....  
 .....  
 .....  
 .....

6. Ni shida gani ambazo mwanafunzi atazipata ikiwa hafundishwi hadithi simulizi katika kufunza maadili mema, Visiwani Zanzibar?

Elezea.....  
 .....  
 .....  
 .....

7. Ni aina gani ya hadithi simulizi na maadili mema zinazosimuliwa shule za sekondari?

Zitaje.....  
 .....  
 .....  
 .....

8. Mwalimu anapowasimulia hadithi simulizi darasani huwa anazingatia vianzio vya hadithi ? -----Ndiyo.....Hapana.....

Vitaje vianzio unavyovijua

- (i) .....
- (ii) .....
- (iii) .....
- (iv) .....
- (v) .....
- (vi) .....
- (vii) .....
- (viii) .....

9. Mwanafunzi anapowasimulia hadithi simulizi wanafunzi wenzake darasani huwa anazingatia maadili mema ya Kizanzibari?

Ndiyo----- Hapana.-----

10. Unadhani muda uliopangiwa kwa ajili ya kujifunza hadithi simulizi kwa siku Unatosha?. Ndiyo..... Hapana.....

11. Kwa wiki ni vipindi vingapi?.....  
Vinatosha?.....Ndiyo.....Hapana.....

12. Taja aina za hadithi unazozijua

13. Toa maoni /mapendekezo yako kuhusu nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema Visiwani Zanzibar.

**ASANTE SANA**

## Kiambatanishi II: Maswali ya ana kwa ana na wanafunzi

### 1. Wanafunzi

Jina lako.....

Shule unayosoma/unayosomesha.....

Umri wako.....

Unapoishi.....

Tarehe ya kuelezea hadithi.....

2. Mwalimu anapowasimulia hadithi simulizi wanafunzi darasani huwa anafuata dhamira maalumu anayokusudia kwa wanafunzi wake?

Ndiyo----- hapana -----

3. Mwanafunzi anapofundishwa hadithi simulizi huwa zinazingatia maadili mema ya Kizanzibari? Ndiyo ----- Hapana-----

Yataje.....

.....

.....

.....

4. Ni mbinu gani anazotumia mwalimu katika kufundisha hadithi simulizi na maadili mema, Visiwani Zanzibar?

Zitaje.....

.....

.....

5. Ni faida gani anayoipata mwanafunzi anayefundishwa hadithi simulizi katika kufunza maadili mema, Visiwani Zanzibar?

Elezea.....  
 .....  
 .....  
 .....  
 .....

6. Ni shida gani ambazo mwanafunzi atazipata ikiwa hafundishwi hadithi simulizi katika kufunza maadili mema, Visiwani Zanzibar?

Elezea.....  
 .....  
 .....  
 .....

7. Ni aina gani ya hadithi simulizi na maadili mema zinazosimuliwa shule za sekondari?

Zitaje.....  
 .....  
 .....  
 .....

8. Mwalimu anapowasimulia hadithi simulizi darasani huwa anazingatia vianzio vya hadithi ? Ndiyo----- Hapana.....

Vitaje vianzio unavyovijua

- (i) .....
- (ii) .....
- (iii) .....
- (iv) .....
- (v) .....
- (vi) .....
- (vii) .....
- (viii) .....

9. Mwanafunzi anapowasimulia hadithi simulizi wanafunzi wenzake darasani huwa anazingatia maadili mema ya Kizanzibari?

Ndiyo----- Hapana.-----

10. Unadhani muda uliopangiwa kwa ajili ya kujifunza hadithi simulizi kwa siku Unatosha?. Ndiyo.....Hapana.....

11. Kwa wiki ni vipindi vingapi?.....  
Vinatosha?.....Ndiyo.....Hapana.....

12. Taja aina za hadithi unazozijua.

13. Toa maoni /mapendekezo yako kuhusu nafasi ya hadithi simulizi katika

**ASANTE SANA**



### Kiambatanishi III: Maswali ya ana kwa ana na wazazi/wazee

#### 1. Wazee

Jina lako.....

Umri wako.....

Unapoishi.....

Tarehe ya kuelezea hadithi.....

#### 2. Mzee anapowasimulia hadithi simulizi watoto/wajukuu wake nyumbani huwa anafuata maadili maalumu anayokusudiwa kwa watoto/wajukuu wake?

Ndiyo.....Hapana.....

Elezea.....

.....

.....

#### 3. Ni mbinu gani anazotumia mzee katika kuwasimulia hadithi simulizi na maadili mema Visiwani?

(i).....

(ii).....

(iii).....

(iv).....

#### 4. Taja madhara anayopata mtoto anaposimuliwa hadithi isiyokuwa na maadili mema ya kizanzibari?

.....

.....

.....

- 4 Mtoto anapowasimulia hadithi watoto wenzake nyumbani huwa anazingatia maadili mema ya Kizanzibari?

.....  
 .....

6. Je, kuna aina ngapi za hadithi simulizi unazozijua?

Zitaje.....  
 .....  
 .....  
 .....

7. Toa maoni yako kuhusu nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili

mema, visiwani Zanzibar? .....

ASANTE SANA

#### **Kiambatanishi IV: Mahojiano**

Mahojiano na Juma Simai (Mnungwi, 2011). Maandamano ya wanawake wa Nugwi kutoka Nungwi hadi Mkokotoni kwa Mkuu wa Mkoa na kudai wanawake wa Tanga waondoke mahotelini-wanafanya biashara ya ngono, Zanzibar.

Mahojiano na Bwana Kassim Suleima Dadi (2011), Kilimahewa-Unguja. Maendeleo ya Ulimbe na utunduizi yameiwezesha fasihi simulizi ya kigeni kuonekana bora kuliko ya wenyenji, Zanzibar.

Mahojiano na Mwalimu Ali Bakari (S.O.S 2011), Matumizi mabaya ya wavupepe na runinga kwa wanafunzi wa shule za Sekondari, Zanzibar.

Mahojiano na Bi Asha Muhene Rashid (2011), Maadili kwa watoto wa kizanzibari, Zanzibar.

Mahojiano na Bwana Silima, Khamisi Ngwali na Walimu wa Tumbatu Jongowe, (2011), Asili na maana ya chanjagaa, Visiwani Zanzibar.

Mahojiano na Bwana Shaaban Saadat (2011), kitego Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mnazi mmoja, Zanzibar.

Mahojiano na Bwana Abdalla Omar Fundi, (2011), TAKILUKI, Dhima na Maadili ya Vianzio vya Hadithi za ngano, vigano, ngoma ya umundi na msewe. Zanzibar.

Mahojiano na Bwana Omar Othman, (2011), Mbuzini-Unguja, Dhima na Maadili ya vianzio vya Hadihi simulizi za Unguja na Pemba, Zanzibar.

### **Kiambatanishi V: Hadithi Simulizi za Vigano, Soga na Ngano**

#### **1. Mtu na mwanawe**

Paukwa.....Pakawa

Usipouanika utaula mbichi.

Hapo zamani za kale alikuwepo mtu na mwanawe, sasa mamangwa akamwambia mwanawe kipindi cha mvua kinakaribia sasa mwanangu mpunga uanike. Mtoto akasema mama tutaotoa kesho mpunga, siku ya pili ilipofika bongela la mvua, hivyo kikanyesha, kwa hivyo mzee na mtoto wakakosa chakula kwa wiki nzima. Usipouanika utaula mbichi.

#### **2. Mize, Mboje na wazazi wake**

Paukwa .....Pakawa.

Hapo zamani za kale palikuwepo na familia moja ambayo ilikuwa na watu watatu mama baba na mtoto wao mmoja aitwaye Miza. Kadiri siku zilivyokuwa zikiendelea usoni mama wa familia hiyo alipata maradhi hadi kufariki dunia. Baada ya kufariki dunia, baba wa familia hiyo akaoa mke mwingine na kupata mtoto mmoja wa kike aitwaye Mboja

Siku moja baba yao akasafiri, aliposafiri Miza akawa anakaa na mama wa kambu. Mama huyo akawa anamtesa sana hatimaye wakenda kutafuta kuni, akamchimbua shimo na kumfukia mzima mzima. Asiyekujua hakuthamini.

Aliporudi baba yao Mboja akamwambia baba yake na wakenda porini akaimba nyimbo.

Miza eee Miza,  
 Baba yetu kesha rudi Miza eee Miza,  
 Katuletea zawadi Miza eeee Miza,  
 Moja yako moja yangu eee Miza,  
 Mboja eee Mboja  
 Mama yako ni mbaya eee Mboja  
 Kanichimbia handaki eee Mboja,  
 Njoo hapa unione eee Mboja,

Baba yake Miza na Mboja akaisikia ile sauti hatimaye Miza akaokolewa na baba yake. Baba yao akahamaki na akataka kumuuwa mkewe lakini Miza na mboja wakamwambia baba yao amsamehe mama yao. Halafu wakaishi raha mustarehe.

### 3. Furaha

Paukwa.....Pakawa

Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

Katika kijiji cha tumaini kilikuwa na watu wengi sana, walikuwa wanapendana sana watu wa kijiji hicho, walikuwa wanaishi wazee, watoto na vijana. Furaha alikuwa ni mmoja ya watoto waliokuwa wakiishi katika kijiji hicho alikuwa ni mwanafunzi lakini alikuwa akijishughuisha na mapenzi, watu wa kijijini hapo walikuwa wakisema na kumuasa sana aachane na tabia hiyo lakini hakisikia, alikuwa kama anapaliliwa. Mwisho Furaha alipata ujauzito, skuli akafukuzwa na nyumbani kwao pia alifukuzwa, akenda kwa mwanamme aliyempa ujauzito naye pia akamfukuza hatimaye akawa mtu wa kutangatanga. Mwisho akajifungua mtoto wa kike lakini hakupata huduma muhimu, alifariki yeye pamoja na mtoto wake. Ama kweli “asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.”

#### 4. BI KIZEE NA MJUKUU WAKE

Paukwa.....Pakawa.

#### BI KIZEE NA MJUKUU WAKE

Hapo zamani za kale alikuwepo bibi kizee na mjukuu wake. Sasa yule bibi akawa anakaa na mjukuu wake lakini mjukuu huyu kila analolifanya hana kosa, mjukuu huyu akawa hatumwi na anachokitaka ndicho anachofanyiwa mtoto akamlea malezi mabaya mwanzoni, baadaye akakulia madhehebu yaleyale aliyolelewa kwao hata ukitaka kumrekebisha haiwezekani tena kubadilika kwa hivyo hata ukimweka sawa utashindwa. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

#### 5. Fisi adhibiwa

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani katika mbuga za Rijeni wanyama wadogo walikutana kwa siri kujadili uovu wa fisi. Walikutana kwa siri kwa sababu walijua wanyama kama simba, chui na fisi walikuwa na hamu kubwa ya kuwashambulia na kuwala.

Swala alikuwa kiongozi wa mkutano na akawambia wenzake,” jamani uonevu umezidi” juma lililopita watoto wawili wa Kongoni waliliwa na chui, tena chui alisema hakushiba. Alitaka sana amshike Kongoni amle, lakini Kongoni aliwahi kukimbia. Juzi mwanangu aliliwa na Fisi, nilimpiga teke jichoni lakini alitaka kunitauna, nikakimbia, sasa tufanyeje?

Basi wanyama walijadili kwa uchungu na kwa muda mrefu. Wote walitaka chui na fisi wauwawe haraka. Tatizo lao kubwa lilikuwa jinsi ya kuwauwa. Wengine walishauri waovu wale wategewe mitego ya kamba baadaye wapofuliwe. Hata hivyo ilionekana ni hatari bado.

Hatimaye sungura akatikisa masikio yake na akasema, “kuwauwa niachieni mimi. Nipeni siku saba nitawaeleza na kuwaonyesha nitakachofanya.”

Basi mkutano ukafungwa kwa kumkubalia sungura afanye kazi hiyo. Usiku ulipoingia sungura alikoka mota nje ya nyumba yake. Moto ulipokolea vizuri akatia jiwe moja ndani ya ule moto. Jiwe hilo lilikuwa na ukubwa na mpira wa tenisi, sungura akaongeza kuni mekoni halafu akaenda kumtafuta fisi pangoni mwake.

Fisi alipofika mlangoni mwa pango akasema, “hodi kwa mzee fisi” fisi alifurahi moyoni, kwa sababu alijua ile sauti ya sungura na alijua kuwa sungura angeweza kuwa chakula chake, fisi hakujibu haraka. Kwa hiyo sungura akasogea mlangoni na kupiga tena hodi. Hapo ndipo sungura alipojikuta makuchani mwa fisi! Sungura akaona kifo waziwazi. Sungura akamwambia rafiki yangu, mzee fisi vipi leo? Nakuletea habari nzuri halafu unanikamata! Fisi akasema,” mimi nina nja ya siku nne halafu uniletee habari nzuri gani?, wewe niriziki yangu” sungura akampoza, “hata kama utanila hutashiba, mimi nimekuja nikukaribishe kwangu. Huko ni nyama ni tele”. Kumbe kikulacho kinguoni mwako.

Fisi alitoka na kucheka huku akimwachia sungura. “Haya ongoza njia, tena uongeze mwendo, sio ule mwendo wake wa sisimizi” sungura na fisi waliika kwa sungura huku mate yakimtoka fisi mdomoni kwa hamu ya nyama. Hapo sungura akapanga vitimbi na akasema, mzee fisi nyama ziko nyingi lakini hizi ni nyama za tambiko. Kwa desturi za kwetu mnofu wa kwanza nitakulisha mimi mwenyewe, mradi ulale chali na ufumbe macho. Baada ya hapo nyama nyingine utakula mwenyewe kwa mikono yako” kabla sungura hajamaliza kusema fisi alikwishalala chali na kufumbaua mdomo na pia kuumba macho.

Sungura alicheka kimomoyo akatoa kibanio, akabana lile jiwe la moto na kulitubwikiza mdomoni mwa fisi, kwa kuwa fisi alikuwa amejandaa kumeza nyama, alilimeza jiwe haraka sana. Looo! Fisi aliungua koo, kifua na tumbo. Fisi alibiringia akilia sana na kujitupa huku na huku hadi akakata roho.

6 . Tajiri na Masikini

Paukwa.....Pakawa.

(Hadhira).....Hadithi njoo, ukweli njoo, na utamu kolea.

Msimuliaji

“ Paliondokeya chanjagaa

Kajenga nyumba kakaa

Mwanangu mwana siti

Vijino kama chikichi

Vya kujengea ukuta

Na milango ya kupita

Jiwe zama kupwa eleya.”

Alikuwepo tajiri mmoja mkubwa sana na maskini ambaye chakula chake ilikuwa ni mikate, kutokana na umaskini aliokuwanao, yule maskini alikula mkate kila siku na kitoeyo chake kilikuwa ni harufu ya nyama na mchuzi itokayo kwa tajiri, tajiri ilikuwa ni kawaida yake kwenda kazini na akirudi. Siku moja alichelewa kurudi kazini na aliporudi alimkuta yule maskini anakula mkate kwa harufu itokayo kwa tajiri, baada ya kusalimiana wawili hao, maskini alianza kwa kumshukuru tajiri kwa kumwambia” asante sana bwana mkubwa, Mwenyezi Mungu akupe moyo huo huo wa ukarimu na ubinaadamu wako kwasababu nimekuwa nikila mikate yangu, kitoweyo changu ni hii harufu ya mchuzi wa nyama na samaki vitokavyo humu mwako “Baada ya maneno hayo tajiri alianza kutoka na kusema “kumbe wewe ndiye unaekula harufu ya vyakula vyangu na nduiyo maana huwa havina ladha “basi utanitambua” tajiri alikwenda kumshitaki kwa mjumbe na alidai alipwe fidia ya shilling 20, maskini alikosa pesa hizo na yule jaji alimsaidia kwa kumpa shilingi ishirini kwa masharti ya kwamba akifika kwa tajiri aidondoshe ile pesa. Maskini alitaka kugoma kwani atamvunjia heshima tajiri lakini hakuwa na namna ila kufanya kama aliyotakiwa. Maskini alikwenda mpaka kwa tajiri alipofika ile pesa aliitoa na ilitoa kelele, kwa bahati nzuri jaji alikuwepo na alimuamuru yule tajiri achukue zile



kelele za shillingi na kama alivyo mshitaki maskini kwa kunusa harufu ya vyakula vyake. Tajiri akaambiwa kitu anachotumia kukandamiza watu ndio hicho kinachoweza kumzalilisha katika maisha yake. Kalamu ya Mungu haifutiki.

#### 4. Paukwa.....Pakawa.

Watoto wa tajiri na maskini.

Hapo kale alikuwepo tajiri na mkewe na walibahatika kupata watoto wawili wanawake. Kando ya nyumba ya tajiri alikuwepo bwana mmoja masikini ambaye alikuwa na kazi ya useremala akiitwa babu tenda watoto wa tajiri walikuwa wanapenda kucheza na babu tenda ambaye ni jirani yao naye alipenda sana watoto na alicheza nao wakati akiwa na harakati zake za useremala.

Kila siku waliokwenda watoto kwa babu Tenda, walimuita kwa kusema Babu Tendaa ..... naye alijibu “naam babu kila mtenda wema hujitendea nafsi yake na mtenda mabaya huitendea nafsi yake.”

Kitendo cha watoto wa tajiri kucheza na babu Tenda kilimchukiza sana mke wa tajiri na kilijenga chuki na uhasidi ndani yake.

Babu tenda alikuwa na kawaida ya kuwapa zawadi watoto mara wanapoondoka na kuelekea nyumbani kwao kama vile njugu, kashata ndizi n.k. watoto walifurahia na kujenga upendo na babu yao.

Siku moja mama yao aliandaa keki nzuri na kumpa mtumishi kama ni zawadi aipeleke kwa babu tenda. Keki hiyo alikuwa ameitia sumu kwa lengo la kumuwa babu tenda. Babu tenda aliipokea keki ile bila ya wasiwasi na kuiweka na aliendelea na kazi zake za useremala. Kama kawaida watoto waliingia kwa babu yao na kuanza kumuita “babu tenda” naye alijibu naam “babu mtenda wema hutenda nafsi yake na mtenda ubaya hutendea nasi yake”.

Watoto waliendelea kucheza kwa furaha na babu yao na ilipofika wakati wa kuondoka alikuwa siku hiyo hana kitu isipokuwa keki ambayo ililetwa kutoka kwa

mama yao. Babu tenda alichukua vipande vya keki na kuwapa watoto walikula na kuondoka kuelekea nyumbani kwao.

Mama mtu alikaa akisubiri kifo cha babu tenda ghafla watoto wake waliingia wakilalama matumbo yanauma kwa maumizu makali, alishtuka na kumuita muumewe na kumueleza kuwa watoto wanaumwa.

Walikimbizwa hospitali na daktari alithibitisha kuwa wamekula sumu. Baba watoto alistuka na kushangaa alimueleza mkewe na alimhoji kwa ghadhabu huku mwana mama yule akiwa na hofu na tahayuri. Daktari aliwaita na kuwaeleza kuwa watoto waumwa sana na tajiri alimtaka mwanamke aseme watoto wamekula wapi sumu.

Bila ya kusita mama watoto alisingizia waliondoka kwenda kucheza kwa babu tenda wakiwa wazima, walitumwa askari wakamchukue babu tenda na alipohojiwa alisema ukweli kwamba aliwapa keki iliyoletwa na mama yao kama zawadi ambayo yeye hakuwahi kuitumia na aliwapa wao na nyingine iko labda ikachukuliwe ifanyiwe uchunguzi.

Uchunguzi ulibaini kuwa ni kweli na kwa kuwa ni mama yao na alitiwa hatiani.

## 5. Fisi, chui na sungura

Paukwa..... pakawa.

Hapo zamani katika mbuga za rijeni wanyama wadogo wadogo walikutana kwa siri kujadili uovu wa fisi. Wanyama kama simba, chui na fisi walikuwa na hamu kubwa ya kuwashambulia na kuwala. Swala alikuwa kiongozi wa mkutano na akawaambia wenzake. “Jamani uonevu umezidi. Juma lililopita watoto wawili wa Kongoni kasoro kidogo waliwe na chui, lakini Kongoni waliwahi kukimbia. Juzi mwanangu aliliwa na fisi nilimpiga jichoni, fisi akataka kunitafuna nikakimbia sasa tufanyeje?

Basi wanyama walijadili kwa uchungu na kwa muda mrefu. Wote walitaka simba, chui na fisi wauwawe haraka. Tatizo ni jinsi ya kuwauwa, wengine walishauri

wategewe mitego ya kamba baadaye wapofuliwe. Hata hivyo ilionekana ni hatari bado.

Hatimaye sungura akatikisa masikio yake na kusema. ‘‘Kuwauwa niachieni mimi, nipeni siku saba nitawaeleza na kuwaonyesha nitakachokifanya.’’

Basi mkutano ukafungwa kwa kumkubalia sungura afanye kazi hiyo. Usiku ulipoingia sungura alikoka moto nnje ya nyumba yake. Moto ulipokuwa vizuri akatia jiwe moja ndani ya ule moto. Jiwe hilo lilikuwa na ukubwa wa mpira wa tenisi. Sungura akaongeza kuni mekoni halafu akaenda kumtafuta fisi pangoni mwake.

Sungura alipofika mlangoni mwa pango akasema ‘‘Hodi kwa mzee fisi’’ fisi alifurahi moyoni, kwa sababu alijuwa ile ni sauti ya sungura na alijua kuwa sungura angeweza kuwa chakula chake. Fisi hakujibu haraka. Kwa hiyo sungura akasogea mlangoni na kubisha tena hodi. Hapo ndipo sungura alipojikuta makuchani mwa Fisi, sungura akaona kifo wazi wazi. Sungura akamwambia ‘‘Rafiki yangu mzee fisi vipi leo’’? Nakuletea habari nzuri halafu unanikamata. Fisi akasema mimi nina njaa ya siku nne halafu uniletee habari nzuri gani? ‘‘wewe leo ni riziki yangu’’ sungura akampoza ‘‘Hata ukinila hutashiba’’ mimi nimekuja nikukaribishe kwangu huko nyama ni tele’’.

Fisi alifurahi na kucheka huku akimwachia sungura ‘‘Haya ongoza njia, tena uongeze mwendo, sio ule mwendo wako wa sisimizi’’. Sungura na fisi walifika kwa sungura, fisi mate yakimtoka mdomoni kwa hamu ya nyama. Hapo sungura akapnga vitimbi vyake akamwambia fisi nyama ziko nyingi lakini ni nyama za tambiko, kwa hivyo ufuate miko, akamwambia mnofu wa kwanza atalishwa lakini alale chali mdomo ukiwa wazi na macho afumbe, baada ya kusema tu, amemkuta fisi kashalala chali na kufumbua mdomo na macho kufumba.

Sungura alicheka kimoyomoyo akatoa kibanio, akatoa like jiwe la moto na kulitumbikiza mdomoni mwa fisi, kwa kuwa fisi amejandaa kumeza nyama, alimeza jiwe haraka sana. Looo! Fisi aliungua koo, kifua na tumbo. Fisi alibiringika akilia sana na kujitupa huku na huku hadi akakata roho. ‘‘Ama kweli tamaa mbele mauti nyuma.’’

## 9. Sikudhani na Majaaliwa.

Paukwa ..... Pakawa

Mwenye kutafuta elimu lazima akeshe usiku.

Walikuwepo wanafunzi wawili Sukuzani na Majaaliwa, walikuwa ni wanafunzi wenye kushirikiana katika masomo yao na walipofikia darasa la 12 mwalimu wao aliwambia washughulikie masomo yao wakati wote bila ya kujali kuwa ni usiku au mchana ili wafaulu katika masomo yao, waliendelea kushirikiana siku hadi siku lakini mwisho Sikudhani alijishughulisha na mambo mengine na badala yake hakuyajali tena masomo lakini Majaaliwa aliendelea kuufanyia kazi ushauri wa mwalimu wake na badala yake alifaulu kuingia darasa la 13, na Sukuzani hakufaulu hapo ndipo Sukuzani aliposema “ama kweli kutafuta elimu lazima akeshe usiku”.

.

## 10. Asma abeba ujauzito wa Hassan

Paukwa.....Pakawa

Mtaka yote hukosa yote,

Hapo zamani za kale alikuwepo mwanafunzi mmoja aliyejulikana kwa jina la Asma. Mwanafunzi huyu alikuwa akiishi na wazazi wake, wazazi wake walifanya kila njia kuhakikisha mtoto wao anasoma ili aje kuwasaidia huko mbele. Asma alipewa kila nasaha na wazazi wake ili ashughulikie masomo na asijishughulishe na mambo mengine. Lakini wapi nasaha zote hizo hakuzijali, asma alipata mvulana mmoja aliyejulikana kwa jina la Hassan, Asma alipewa kila alichokuwa akihitaji, hivyo aliacha kabisa kushughulikia masomo na akajiingiza kwenye dimbwi la mapenzi. Baada ya miezi kadhaa Asma alibeba ujauzito na skuli akafukuzwa kabisa, ndipo alipoamua kwenda kumuelezea Hassan ili apate msaada, lakini kwa bahati mbaya Hassan alimkataa na kumwambia asimfate fate, baadaye mama yake Asma kusikia

habari zile, alipandwa na presha na kufariki dunia, na baba yake Asma alimfukuza nyumbani mwake akamwambia hataki kumuona, akabaki Asma hana mbele wa nyuma wala hajui ni afanye. Ama kweli! Wahenga walisema Mtaka yote hukosa yote.

#### 11. Mwanampate na Nyangoro

Paukwa .....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo Mwampate na Nyangoro wote walikuwa ni wanafunzi wa kidatu cha sita katika skuli ya Nzisiwe. Waliweza kusaidiana katika masomoyao kwa hali na mali hadi wakawa ni marafiki na kuahidiana kuowana. Baada ya kumaliza muhula wa kwanza walipewa mapumziko ya mwezi mmoja. Siku moja, Mwampate alikutana na mvulana mzuri ambaye ni tajiri ukilinganisha na mpenzi wake Nyangoro, na Mwampate akamkubalia na kuweza kufanya mapenzi na yule mvulana. Udhaniaye ndiye, kumbe siye.

Baada ya muda kidogo Nyangoro akaanza kuona mabadiliko na kufikia kujua kama hatakiwi na kuweza kutengana kimazungumzo na kimasomo. Baada ya kufikia karibu na mtihani wa mwisho, Mwampate aligundulikana na ujauzito na kupelekea kufukuzwa shule na hakuruhusiwa kufanya mtihani wake wa mwisho. Basi Mwampate alimwendea yule mpenzi wake aliyembebesha mamba, kufika akamuhadithia na akamjibu mimi sikutaki kinyago kama wewe badala ya kusoma unaendekeza mapenzi na usije kwangu. Na hadithi yangu ikaishia hapo.

#### 12. Kurwa na Doto

Paukwa.....Pakawa.

“Mgaa na upwa hali wali mkavu”

Hapo zamani za kale, alikuwepo Kurwa na Doto, ndugu hawa walipenda sana, pia ni wanafunzi wa shule ya ya sekondari ya Njoo nawe.

Kurwa alijitahidi sana katika masomo yake, Doto hakupenda kujishughulisha na masomo shuleni, Kurwa alimshauri sana dada yake asome, lakini Doto alimfumbua macho na kumzibia masikio dada yake kwa ushauri wake.

Baadaye Kurwa alimsikiliza dada yake na kushirikiana naye na kuhangaika huku na kule kutafuta elimu. Kurwa na Doto walifanikiwa kwani Doto akawa daktari na Kurwa akawa mwalimu, wote kwa pamoja wakisema “Mgaagaa na upwa, hali wali mkavu”

### 13. Adili na Amali

Paukwa ..... Pakawa

Umoja ni nguvu na utengano ni dhaifu

Hapo zamani za kale walitokea ndugu wawili, waliojulikana kama Adili na nduguye alieitwa Amali. Watoto hawa walikuwa wakiishi na babu yao mpenzi mzee Mjuma. Mzee Juma aliwapenda sana wajukuu zake, na alikuwa akiwafundisha maadili yanayotakiwa kuwa nayo mtoto.

Siku moja Adili na Amali walikwenda mwituni kutafuta embe. Walipofika huko mwituni walianza kuchokozana, haikuchukua muda kila mmoja aliamua kushika njia yake bila kujali kama wao ni ndugu, kila mmoja alianza kutafuta embe bila kumuuliza mwenzake chochote, baada ya dakika kadhaa lilikuja kundi jengine la watoto nao walikuwa wanataka embe, walijiunga na kina Adilki kutafuta embe huku utafutaji wa embe unaendelea, ghafla mtoto mmoja kutoka kundi lile akamchokoza Amali, Amali hakukubali mara wakaaza kupigana, hatimaye Amali akavunjika mkono katika mapigano hayo, Adili hakumtazama Amali wala hakumsaidia. Waliporudi nyumbani babu yao aliuliza kuhusiana na mkasa huo, na ndipo babu alipoamua kuwapa kila mmoja kijiti chake na kumuamuru kila mtu akivunje na

hatimaye walifanikiwa na baadaye akawapa kila mtu vijiti viwili akaamuru vivunjwe, wakashindwa hapo babu yao ndipo alipowaambia kuwa “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu”.

14. Mtoto aliyetumwa kwa mfalme.

Paukwa .....Pakawa.

Mjumbe hauwawi.

Alikuwepo Mfalme, baba mtu na mwanawe, yule baba mtu alimtuma mwanawe akamwambiye mfalme kuwa baba anaumwa. Yule mwanawe akaenda kwa mfalme akagonga na akajibiwa toka kila siku unaomba wewe” akamwambia aaa miye nimekuja na shida nyengine” yule mfalme akasema “huna jipya ndio hilohilo kila siku” shida tu ndio ilokuleta” mtoto akakataa sio baba anaumwa tena akamwambia toka haraka yule mtoto akashusha pumzi na akaondoka.

Akarudi kwao akamwambia baba leo mfalme hakunifungulia mlango kakataa, na anasema kila siku tunakwenda kuomba. Yule baba yake mtoto akawa anaumwa na akaenda kumtafuta dawa ana akapoa. Akasema yule mtoto Mwenyezi Mungu hamtupi mja wake. Baba mtu na mwanawe wakawa hawaendi kwa mfalme kuomba nawao wakawa na maisha mazuri. Sasa siku moja mtoto alimwambia baba yake twende tukamtembelee mfalme yule baba mtu akasema “kweli mwanangu halahala jirani kama ndugu aliyembali “wakaenda lakini walifukuzwa sasa siku moja mfalme alipatwa na tatizo haoni naakaamua aende kwa yule jirani yake aliyekuwa akienda akakaribishwa kwa raha na akamhudumiwa kwa kila kitu, mara yule baba akaanza kulia, mwanawe akamwambia baba usilie mwanangu nakumbuka mengi “wakamjaamazisha na yule mfalme akaomba radhi na hadithi ikaishia hapo.

15. Viungo vilivyokataa kufanya kazi

Paukwa.....Pakawa

“Fikiri ndipo utende”,

Siku moja viungo vilikataa kufanya kazi. Viligoma kwa sababu ya kuchoka kulitumikia tumbo. Punde ukafika wakati wa chakula. Kwa vishindo pupa la kutaka kutangulia katika ngomo, mguu ulitangaza, “mimi sitakwenda kuleta chakula”.

Lo! Kusikia vile na meno yalidai huku yakiumana kwa hasira na ukali, “sisi kabisa hatutakitafuna licha ya kukichukua na kukisaga kikalainika chakula hicho. Bila ya subira ulimi nao ukatamka, “sitaki lainisha kwa mate yangu na wala sitoviringa tonge na sitosukuma tumboni”.

Mradi kila kiungo kilisema kwake katika kuunga mkono dai la mgomo. Kwa wingi wa busara na werevu wa kuchukua mambo, tumbo tulijiuzuia kujibu lolote.

Muda si muda uongo ulijitenga! Viungo vyote vikadhofika kwa kugoma kwao. Hapo ndipo tumbo lilipopata nafasi ya kususuka je mnaniona! Mbona mnaregea hamuwezi kufanya kazi? Tunaposhirikiana, faida si ya mmoja bali ni ya wote. Huo ndio ushirikiano. Lakini nyinyi hamkufikiri, mmetenda tu.

#### 16. Nyuki aliyetoroka wenzake

Paukwa .....Pakawa.

Ummoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Hapo kale palikuwa na Nyuki na jamaa zake. Wakaamua kutengeneza asali, wakafanya kazi kwa jitihada kubwa katika kutengeneza sega la asali. Zilipita siku nyingi sana na kufanya kazi bila ya kukorofishana lakini nyuki mmoja aliona kwamba anategewa na hapati manufaa yoyote isipokuwa kidogo, Hivyo akaona awahame Nyuki wenzake, alipowahama yalimpitikia mashaka mengi bila ya kupata afueni, Hivyo alirejea kwa nyuki wenzake. Lakini aliporejea aliona kazi anaendelea kama ilivyokuwa awali. Akasema ni kweli haiwezekani jambo la watu likaharibika kwa mtu mmoja mmoja. Nyuki alirejea na kufanyakazi na wenzake kama kawaida.



## 17. Simba, Chui, Chura na Kiwaviwavi

Paukwa.....Pakawa

Ukubwa si hoja

Hapo zamani alitokea simba, chui, chura na kiwavi. Siku moja chui aliondoka na kuuwacha wazi mlango wake, kuona vile kiwavi akaingia ndani na akaufunga mlango, mara chui aliporudi akaukuta mlango wake unefungwa, akaaza kuhodisha na kusema. “wewe nani ulifunga mlango na kuingia ndani”. Kiwavi wavi akasema “sitoki mimi ni jini wa bahari ya saba nitakutekeza sasahivi, kuona vile chui akaaza kulia. Mara akatokea simba na kuanza kumuhadithia akajaribu kumtoa lakini hakutoka, akatokea chura na kuanza kumwambia “wewe nani toka kwenye nyumba ya hii” kiwawavi akasema “sitoki mim ni jini wa bahari ya saba nitawaangamiza nyote”. Chura akamwambia mimi ni jini wa bahari ya ishirini na saba nitakuangamiza hata jivu lako lisibakie” kuona vile kiwaviwavi akatoka na wote walipomuona walishangaa. Nahadithi yangu imeishia hapo.

## 18. Mtoto Mzuri Kushinda Wenzake

Paukwa..... Paukwa

Mtaka nyingi na saba hupata mwingi msiba.”

Hapo zamani za kale walikuwepo watu na familia zao, humo ndani kukawepo na mtu mmoja na mkewe mmoja na watoto wake miongoni mwa watoto hao alikuwepo mmoja ni mzuri sana kushinda wenzake, mtoto huyo alipofikia umri wa utu uzima alitokezea mchumba na kuja kumposa, baba yake hakumtaka mchumba huyo kwa sababu alikuwa masikini, akaja wa pili pia hakumkubali na watatu pia hakumkubali. Baba yake alikuwa anataka mwanawe aolewe na tajiri, basi yule mtoto wa kike akafanya mambo mabaya ambayo yalimpelekea kupata ujauzito .

Baada ya kupata ujauzito huo na hakuonekana kwao, basi aliamua kutafuta dawa mbali mbali kwa ajili ya kiotoa ila mimba yake. Kwa bahati mbaya zile dawa zilimpelekea kufariki dunia .

Hapo wazazi wake wakabakia na majonzi kwa kufa kwake. Sababu zote hizo alisababisha baba yake kwani wangali muozesha mume yasingali wafika hayo.

#### 19. Uvumilivu wa Bi Asha

Paukwa..... Pakawa

Mvumilivu hula mbivu,

Hapo zamani za kale alikuwepo Bi Asha aliyekuwa akiishi na mumewe pamoja na mtoto wake Fatma, mara tu baada ya mumewe kuongeza wake wawili alimnyanyasa sana mkewe na kumuona hana maana lakini Bi Asha alivumilia mateso yale.

Mara tu baada ya mwaka mmoja kupita mumewe alimuacha mke mmoja baada ya mwengine kutokana na ugomvi na matatizo ya hapa na pale. Kwa vile mwenda tenzi na omo hurejea ngamani mumewe Bi Asha alimrejea mkewe na kumlea mtoto wao wa pekee, Fatma.

#### 20. Sungura na Chura

Paukwa.....Pakawa

Hapo zamani za kale palitokea marafiki wawili waliopendana sana, yaani walikuwa chanda na pete. Marafiki hao walikuwa wakiitwa Sungura na Chura, mara nyingi walifuatana sanjari kila mahali ijapokuwa walikuwa na dosari ndogo ndogo baina yao lakini walipendana sana. Sungura alikuwa na sifa ya kubuni mambo kwa haraka lakini bwana Chura alikuwa mwingi wa kufikiri kwa kina.

Siku moja Sungura alipewa kazi ya ushenga. Ilitakiwa siku inayofuata apelize barua ya madai ya wanyama kwa ukoo wa binadamu. Kwa vile Sungura ni mbunifu alipewa kazi hiyo ili kufikisha malalamiko ya kuliwa kwa wanyama na Ukoo wa

binadamu. Hata hivyo Sungura alipendeza afuatane na Chura maana wawili dawa. Sungura alimwambia Chura, “Rafiki yangu tuna safari” “Chura akajibu,” ya kwenda wapi na inahusu nini?” Sungura akafikiri kidogo kisha akasema, “Sio hao nguru mbili!” “Ngurumbili ndio nani?” “Chura aliuliza” Ni binadamu wala wanyama, Mfalme wetu Tembo amenipa barua ya kwenda kuwaona.

“Usiwe na hofu tutakwenda sote, hii ndiyo komesha yao” alimaliza Chura. Tena mfalme kasema kuwa “wakikaidi tu, Chui na Simba wapewa amri ya kuwararuwa hao binadamu” Sungura alimaliza. Asubuhi kulipopambazuka, Sungura na Chura walianza safari ya kupeleka barua. Njiani walikuta ndizi wakala na nyengine wakaficha ili wakati wa kurudi wamalizie. Lakini walikubaliana kuficha siri ya kuiba hizo ndizi. Kumbe kahakuna siri ya watu wawili.

Walipokuwa njiani wakirejea Sungura akaanza kumlaumu Chura kuwa ana wasiwasi na hofu, unataka tujuulikane kuwa tumeiba ndizi “naona utasema tu hii siri” Chura kwa unyonge akajibu, “Rafiki yangu mimi ndio nilivyo, siwezi kusema labda utasema wewe” waliendelea na safari yao ya kurudi. Vijiji vile walivyokula ndizi za wizi, binadamu wakaanza kuwatafuta hao wezi bila ya mafanikio. Hatimae wakaanza kukata tama. Wakiwa umbali wa vijiji viwili kufika maskani kwao, Sungura na Chura walianza tena kubishana. Sungura ndiye alianza maneno tena ya dharau dhidi ya Chura. Alimwambia kuwa Chura ni mwanamke hawezi kuficha siri tena siri yenyewe ni ndogo mno. Chura aliamaki na kukataa kuendelea na safari. Loo! Sungura akaanza kumbembeleza ili warudi kwao si vyema kubaki pale. Wakati wanaendelea na mazungumzo yao ghafla akatokea mtoto wa binadamu. Akawauliza “kwani kulikoni ndugu zangu mbona mwagombana?” Chura akamuangalia usoni rafikiye na kumpiga ukope. Afanaleki! Sungura akapayuka, “Sii! Unaona, mimi nilikwambia wewe Chura huna kifua, ona unavyopumua kwa woga “mbona mwanifumba kwani kifua cha nini hasa?” Aliuliza mtoto wa binadamu. Aaa! Si tuliiba ndizi huko njiani. “Basi yeye ndio wasiwasi mtindo mmoja” Alimaliza Sungura. Chura akasema, “si unaona wewe ndio unasema” Hapo hapo mtoto wa binadamu aliwakamata na kuwapeleka nyumbani kwa mzee wa ukoo wa binadamu. Na huu ndio mwisho wa hadithi!

Bwana Masoud alitafuta mke mwengine akaowa na kuwalea watoto na wote waliishi raha mustarehe.

## 22. Bwana Ali kapanda cheo.

Paukwa.....Pakawa.

Alikuweko Bwana Ali alifanyakazi kwa siku nyingi tu, mwaka juzi akapandishwa cheo katika ofisi ya kipima joto, akawa na wahudumu kabakaba na gari la mneso lemye dereva kijana, Bwana Ali akawa anapita mitaani na kila sehemu kutangaza cheo chake, kila anapopita anagawa pesa na vitu mbalimbali, na huku tayari kasha lewa, kiingereza kinamtoka “rememba I am Boss”, Mashabiki wanamuitikia kwa shangwe, kwa kuwa anawapa vitu. Boss bichwa likavimba kama boga. Januari mwaka huu wakamtema maana shirika linadidimia na yeye anainukia. Basi wamemtoa pale bosi yuko kijijini analima mahindi.

## 23. Kiongozi aliyefungua kisima

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alitokezea kiongozi mmoja akenda kufungua kisima katika sherehe za wanakijiji. Yule kiongozi akachungulia kwenye kisima, ndani ya kisima kile na akauliza humu kwenye kisima wanafuga mamba? Msimamizi wake akamjibu, hapana muheshimiwa ni sura yako hiyo.

## 24. Bunuasi na Mfalme

Paukwa.....Pakawa

Hapo zamani za kale palikuwepo na mfalme na bunuwasi, siku moja Mfalme alimwambia Bunuasi kuorodhesha majina ya watu wasioona katika kijiji chao, mara Bunuasi akanyanyuka akachukua tawi la mti na kuaza kuliburura. Mfalme akamuuliza “Wee Bunuasi unafanya nini?” Bunuasi akamuangalia mfalme na

akamuorezesha kwenye daftari la watu wasioona kwa vile hakuweza kumuona yeye anafanya nini ndiyo maana akamuuliza.

25. Hadithi ya Mzee Majaliwa.

Paukwa .....Pakawa.

Hapo zamani za kale kulikuwepo na kikundi kilichoitwa “mtu lake haliwezi”, kiongozi wa kikundi hicho alikuwa anaitwa Majaaliwa .Mzee huyo hakuwa mtu mwenye kujithamini, alipendelea sana kuvaa nguo mbovu, jambo ambalo halikupendezwa na wanakikundi. Siku moja katika harakati zao za chama, alitokezea mwanachama mmoja aitwaye Majungu Ndo Pao. Mzee huyo ni mtu mweye mas-hara sana. Wakati wanapanga shughuli zao za kazi alimsogelea mzee Majaaliwa na kumchoma ujiti wa ubavu, watu walipomuona walicheka sana na hata yeye alicheka sana kwa tahayari, aliondoka kwenda kubadili suruali nyengine ilio nzima.

26. Hadithi ya Majuha wanne wasiojuana.

Paukwa .....Pakawa.

Hapo zamani za kale walikuwepo majuha wanne ambao walikuwa hawajuani kama wote ni majuha. Siku moja majuha watatu walikutana barazani, hawakuchukuwa muda na baadaye Juha wa nne akatokea na kuwasalimia” ASSALAMU ALAIKUM MAJUHA” wale majuha wote watatu wakatazamana na kuanza kuulizana maswali “inabidi sote tulokuwepo hapa ni majuha ?”Mmoja aliuliza. Na kwa nini akatusalimia kwa kututambua? Itabidi kila mmoja aeleze kwa nini akawa ni Juha?

Juha wa kwanza akajieleza. Mimi nilikuwa na tajiri wangu ambaye alikuwa ana kawaida ya kunituma. Siku moja alinituma nikakate kigogo cha kuni ili nipeleke kwake, nilipokwenda kukata kile kigogo, kilipotaka kuanguka kutoka juu ya mti nikainamisha mgongo wangu ili kisianguke chini kikaingia tope, hivyo kiliniangukia mgongoni na kuchuruzika damu nyingi, JEE WENZANGU HUU SI UJUHA? Wenzake wakajibu huu ni ujuha.

Juha wa pili na yeye akajieleza, mimi nilikuwa na jino nikenda hospitali kilingoa niliporudi numbani mke wangu akaniuliza “mume wangu umengoa jino shilingi ngapi?” Nikamjibu shilingi hamsini, mke wangu kusikia vile akakasirika sana kusema “pesa zote hizo mume wangu umengoa jino moja, huoni ni pesa nyingi, basi nenda kamwambiye akurejeshee pesa zako au akuwachiye uyangowe na meno mengine “Niliposikia hivyo nilirudi spitali na kuyangoa meno yote, jee wenzangu huu si ujuha? Wenzake wakajibu ni ujuha.

Juha wa tatu na yeye akaendelea kusema “mimi niliajiriwa kazi ya ulinzi wa duka nikapewa bunduki ili akija mwizi nimuuwe lakini kabla ya kuondoka yule tajiri wangu aliniambia “nakupa bunduki lakini atakaye kuja hapa kwanza umuulize wewe nani? Akiwa hakukujibu basi mpige bunduki. Baada ya masaa kupita, usiku nao ukazidi kuwa mkubwa na watu nawo wakawa wanataka kuingia dukani, kila anayetaka kuingia dukani, ikawa namuuliza wewe nani? Ananijibu “mimi mtu, “namuachia anapita, mpaka ikafikia karibu na alfajiri sijapata mtu, nikazunguka nyuma ya duka, nilipofika Yuma ya duka, nikamuona punda wa mizigo nikamuuliza “wewe nani?” Yule punda hakunijibu kitu, mara tatu nikaendelea kumuuliza hakunijibu kitu, ikabidi nimpige bunduki. Asubuhi yule mweye duka alipofika

akaniuliza “Enhe leo umepata wizi angapi?” Nikamwambia kuwa nimepata mwizi mmoja yuko nyuma huko kamtazame, yule tajiri alipofika akamkuta punda wake keshakufa na alipotazama dukani hakukuta chochote mali zote zimeibiwa .Jee huu si ujuha? Wenzake wakajibu ni ujuha.

Juha wa nne akajitambulisha kuwa yeye pia ni juha kwa kusema kuwa “siku moja nyumbani kwangu kulipikwa nyama, wakati nyama iko jikoni inatokota mke wangu alikwenda kuteka maji,nilipomuona mke wangu katoka tu, nikakiendea chungu cha nyama nikaaza kuchota na kuikamata mkononi,niliposikia mke wangu anakuja niliitumbukiza mdomoni, shavu likaanza kuvimba, mke wangu akaniita siitiki kwa kuamini kuwa nyama mdomoni itakuja nitoka na ataiyona, mke wangu akawa hana raha tena, anahangaika huku na kule akisema “mume wangu una nini mbona husemi leo?” Mpaka akapata fikra ya kuchukua kinga cha moto na kunipiga nacho mdomoni, ndipo ile nyama ikanguka na kudondoka chini huku akinita na kuanza kunilaumu. Jee huu si ujuha ? Majuha wenzake wakamjibu wewe ndiye juha zaidi. Na hadithi ikamalizikia hapo.

27. Dereva wa gari

Paukwa.....Pakawa.

Alikuwepo dereva wa gari, dereva huyo aliendesha gari aina ya mbavu za mbwa alikuwa ni dereva mzuri sana.

Siku moja alipokuwa kazini kwake akitokea shamba na kuelekea mjini, njiani alisimamishwa na polisi ili kuangalia usalama wa gari ile pamoja na usalama wa abiria. Polisi akamuuliza dereva “Umepakia watu wangapi?” dereva akajibu “mna watu ishirini na tatu na mmakonde mmoja”. Basi yule mmakonde aliyekuwemo



ndani ya gari ile alichukiwa na lile jibu la dereva na hakufurahia hata kidogo kauli ile. Yule polisi alipomaliza kuikagua ile akairuhusu iondoke.

Gari iliendelea na safari na dereva akaanza kudai nauli kwa abiria wake, alipofika kwa Mmakonde, Mmakonde aligoma kutoa nauli na kusema “kwani Mmakonde mtu, Mmakonde chi mtu, wewe umemwambia polichi humu mna watu ishirini na tatu kwa iyo mimi chitoi nauli maana mimi chi mtu umechikia?”

Kwa hiyo dereva aliishiwa nguvu na akawahana la kusema na kwendelea na safari yake, hadithi yangu imeishia hapa.

## 28. Sungura na fisi.

Paukwa.....Pakawa.

Alikuwepo sungura na fisi, sungura akenda hotelini akaagiza chakula, akala, kushiba tu akamchukua panya ambaye alikuwa kishakufa alimficha hapo mwanzo akamtia katikati ya chakula akamwita muhudumu na kuanza kumshambulia akamwambia nitamwambia tajiri wenu, wale wahudumu wakajitolea kwa kumpa pesa kibao na yule sungura akazichukua zile pesa ili asitowe siri ile.

Fisi naye akaenda kulekule hotelini akaagiza chakula, akaletewa na kuanza kula, kushiba tu naye akatoa mende na kumtia kwenye chakula, naye akaanza fujo kujitetea kwa wahudumu, fisi akapewa elfu tano. Kuona pesa aliyopewa ni ndogo akaanza kuwashambulia wahudumu nyinyi vipi mwenzangu kaja kutia panya mmempa pesa kibao, miye nimetia mende mmenipa elfu tano sikubali. Wale wahudumu wakamvamia na kumpiga fisi kichapo cha nguvu.

## 29. Mla matonge.

Paukwa.....Pakawa.

Siku moja tulikaa barazani katika mazungumzo akaja mmoja wetu akasimulia kuwa fulani alikuwa shughulini anakula matonge makubwa halafu hatafuni mara akatokea mwenyewe tukasema “mwambile mwenyewe ikisha akamwambia kwa utani tukacheka”.

### 30. Mtepe uliosheheni.

Paukwa.....Pakawa.

Siku moja watu walikuwa baharini wakaona mtepe unashehena nyingi ukawa hauwezi kwenda nahodha akasema “yule mwarabu amepakia nini? Hebu tizameni katika makanda”. Wakakata gunia moja akaona tende wakadhani ukwaju akasema “anawazimu mwarabu yule katupa kwaju kupakia katika mtepe wetu hata mtepe unataka kuzama, yatoseni makanda. Wakayatosa.

Wakasema, moja liacheni tuunge mchuzi wakaliacha moja na mle ndani ya mtepe mna mtu mmoja jina lake Mchendewa, hajiwezi ana vidonda miguuni na anaona baridi sana. Akasema ndani ya moyo wake “ni heri nende ni kachukuwe ukwaju nile”, akaenda mpaka akatoa kisu chake akakata banda akatoa, akaona tamu sana, akakaa pale pale, anakula lakini watu mtepeni hawamuoni.

Baadaye masarahangi wakamuona na wakapiga makelele, wakitana wakala tende zote na wakampelekea nahodha wao kidogo. Akala nahodha akawambia “Huu si ukwaju ni tende, rudisheni mtepe” wakapindua matanga. Wakarudi wakafika waliokotosa makanda. Nahoda akasema “zizamieni” akazamia wa kwanza, akafa wakadhani labda amekaa kitako ndani ya maji anakula, akaenda wapili, watatu wanne wote wakafa.

Hawa wamefanya shauri wote wanakula tende chini ndani ya maji. Akabaki ndani ya mtepe yule Mchendewe peke yake naye kujitosa hawezi ana kidonda miguuni anaogopa maji ya chumvi. Akageuza mtepe akatweka peke yake hata akafika lamu. Ukimwambia mgunya “si ukwaju ni mtende” akasirika sana.

### 31. Sungura na Membe

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani palikuwa na sungura na Membe walikuwa ni marafiki wenye kupendana kama pete na kidole. Siku moja walialikwa harusi na rafiki yao.

Walipanga safari ya kwenda harusini, walipitia mtoni kwenda kukoga. Alianza kukoga Sungura alipomaliza akatoka akakaa juu, alipoingia Membe alimpa sungura nguo yake aikamate, aliingia majini na kuanza kukoga. Kule harusini kulikuwa na ngoma ya tarabu imeacha maji yume Membe alitoka chini kwa chini hadi ng'ambo ya pili na kuelekea harusini. Alipofika akakaribishwa na akapewa ngoma alipiinga na kuimba, alimuimba rafiki yake sungura kama hivi:-

“Kashiki bamba kashiki bamba kisungura nimwacha mtoni  
kashiki bamba kashiki bamba kisungura nimwacha mtoni”

Yule sungura baada ya kuona amekaa sana hajatoka akaamua aende zake alipofika njiani alisikia ngoma ikilia kwa mbali na alisikia akiimbwa yeye, alikazana kuharakia alipofikia harusi imemaliza na ngoma imeshivunjwa.

### 32. Jogoo na Nyoka

Paukwa.....Pakawa.

Alikuwepo jogoo na nyoka, jogoo alikuwa na macho lakini hana miguu na nyoka alikuwa na miguu lakini hana macho. Siku moja nyoka alialikwa harusi, kwa vile hana macho alikwenda kwa rafiki yake jogoo ili amuazime macho na aende harusini ili apate kuona. Bila ya mashaka jogoo alikubali lakini walikubaliana kuwa ikimaliza harusi tu amrejeshee macho yake. Lakini zimepita siku nyingi bila ya nyoka kuonekana. Tokea siku hiyo nyoka akimuona jogoo anamkimbia.

### 33. Marafiki watatu.

Paukwa..... pakawa

Palikuwepo na marafiki watatu, nao ni Kingiro, Karne na Miliso. Kati yao Kizingiro alimtuma rafiki yake Miliso dukani akamnunulie zungusho. Miliso alianza kwenda kila duka na kuanza kuzunguushwa na kila mtu anaejua maana ya zungusho humcheka na kumfahamisha duka jengine. Alipoona watu wanamcheka sana akauliza mbona mnanicheka, akajibiwa kuwa kidume wewe unazungushwa. Hapo

alikutuka akarudi kwa rafiki yake na wao walianza kumcheka na kusema basi haina noma.

#### 34. Marafiki Wanne

Hadithi ya Marafiki wanne

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale walikuwepo marafiki wanne ambao walikuwa wanapenda sana kufanyiana utani. Siku moja walikuwa wameka katika kibaraza na wakanza kumtania mwezao mmoja, wakamwambia kuwa jana mkewe alimuaga, jee alijua kuwa alikwenda wapi? Akamjibu kuwa alimuaga anakwenda harusini. Yule rafiki yake akamwambia, mkewe jana hakwenda harusini tumemkuta hoteli anatoka na jamaa. Bwana wenyewe ni huyo anayepita hapo njiani. Watu wote waliokuwa wamekaa pale barazani wakamtazama yule bwana alinayepita kwa mshangao. Pale pale yule mume mtu akaanguka na kuzimia na kupelekwa hospitali. Watu akaja wakaesema jamani utani mwengine siyo, mutakuja kuuwana bila ya kukusudia.

#### 35. Kipofu aliyeomba duwa

Paukwa.....Pakawa

Hapo zamani za kale alikuwepo mtu mmoja kipofu ambaye aliishi kwa muda mrefu bila ya kuona, siku moja kijijini hapo alitokea mcha mungu mmoja anaombeya watu duwa, kila mtu/ kitu anachokitaka, anamuomba duwa na anapata. Yule kipofu aliposikia na yeye alikwenda na akataka aombewe duwa aone japo mara moja. Yule mtu akamuomba duwa, akaona kwa muda mfupi sana, kufumbua macho tu, akaona jongoo, hapo hapo akarudia upofu aliokuwanao. Kutokana na kuwa alipofumbua macho alimuona jongoo, alikuwa kila kitu anachokisikia kwa watu wanasema yeye huuliza, kuliko jongoo, mfano ipite gari nzuri, yeye atauliza kuliko jongoo.

36. Kichwa kidogo aliomba duwa.

Paukwa.....Pakawa.

Alikuwepo jamaa mmoja ambaye alikuwa na kichwa kidogo sana. Siku moja aliamka usiku akafanya ibada kisha akamuomba Mwenyezi Mungu ampe kichwa kikubwa kama weziwe, kabla hajarejea kulala akataka kutoka nje kwa ajili ya kuomba zaidi, lakini aliogopa akapitisha kichwa chake kwenye matundu ya madirisha na akaomba zaidi, ghafla kichwa kikawa kikubwa anataka kurudi hakirudi akapiga kelele usiku ulele watu wakaja kukata nondo za madiridha kichwa kikatoka.

37. Bibi aliyekuwa hajazaa

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo bibi aliyekuwa hajazaa mtoto hata mmoja. Siku moja alikiona kijoka sindano katika matembezi yake na alisema. Ewe Mwenyezi Mungu nipe na mimi mtoto kama kijoka sindano”. Basi bibi huyo alibeba ujauzito na akakizaa kijoka sindano kama kile kijoka sindano alichokiona na alikilea.

38. Binti wa shamba kaingia mjini.

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo binti mmoja aliyeolewa kutoka kijijini na wqkenda kuishi mjini, makaazi yao yakawa ya mjini. Binti yule alikuwa hajawahi kuona mambo mengi ya mjini, katika chumba chake aliekewa vitu mbali mbali kama vile kioo. Ilikuwa ni mara yake ya mwanzo kuona kioo.

Siku moja wakati mumewe yuko kazini alipoangalia kioo na kuona mwanamke, hapo akasema “kumbe huyu mume wangu anamwanamke” alikipiga kioo hadi kikavunjika. Aliporudi mumewe akamkasirikia sana na yule mumewe alimfahamisha mkewe kuhusu kioo na sio mwanamke wa mjini.

## 39. Tupa, Shida na Asha

Paukwa.....Pakawa.

Kulikuwepo na watoto wawili wanaishi na baba yao mzazi, mkubwa anaitwa Shida na mdogo anaitwa Asha na baba yao anaitwa Tupa. Siku moja Shida akasema anataka mke, akenda kuposewa ikafika harusi yao, bwana na bibi hawajuani wala hawajaonana. Siku hiyo ikawa inatakiwa idhini ya mwanamke lakini haikupatikana kwasababu aliamini kuwa hakuna mtu ni shida tupu ila alilazimishwa na kupelekwa kwa mume asiyemtaka lakini baadaye, kufika nyumbani kwa mumewe, alikimbia kwa mumewe na akaenda kwa mwanamme anayemtaka mwenyewe, watu wa pande zote wakaaza kuhangaika kwa kumtafuta bi harusi veli lake lakini hawakumuona tena.

## 40. Sultani na Suria

Paukwa..... pakawa.

Hapo zamani za kale palitokea bibi mmoja ambaye aliishi na mjukuu wake aitwaye Suria, waliishi katika maisha ya shida na umasikini wa hali ya juu katika kijiji chao, walitengwa kutokana na hali waliyokuwanayo lakini bibi huyo alijua kupika sana vyakula mbalimbali na kumfundisha mjukuu wake naye akapata ujuzi huo.

Katika kijiji hicho aliishi mfalme na mkewe na mtoto wao mmoja aitwae Sultani alikuwa ni mtoto pekee kwa mfalme na mkewe kwani alikaa miaka mingi mfalme bila kupata mtoto na mwisho wakampata sultani wakiwa ni watu wazima, walimpenda sana na kumsikiliza kila asemalo.

Siku moja sultan akawaambia wazazi wake kwamba yeye anataka kuowa. Wazazi wake walifurahi sana kusikia maneno ya mtoto wao, lakini akatoa masharti ya kuchaguliwa au kuchagua mke huyo, Sultani alisema kuwa anapenda mkewe awe anajua kupika. Ikapigwa mbiu ya mgambo, siku ikafika watu wakafahamu kuwa

mtoto wa mfalme anataka mke, wanawari wakakusanywa wote katika kijiji na wakapewa chakula cha aina moja wapike, kwa kila mmoja apike chakula chake wakishamaliza kila mmoja akaye katika chakula chake sehemu iliyoandaliwa, mtoto wa mfalme akaaza kupita na kuangalia kila chakula. Suria alikuwa mwisho na chakula chake kikawa ni cha mwisho kuonjwa na mtoto wa mfalme, alifanyiwa hivyo kutokana na hali aliyokuwanayo, alikuwa mchafu kuliko wenziwe. Mtoto wa mfalme ambaye ni Sultani alifanya kama alivyofanya kwa wengine, alionja, akala hadi akakimaliza.

Kwa hiyo Sultan na Suria walioana na kuishi katika maisha ya raha mustarehe yeye na bibi yake.

41. Mtu na mkewe.

Paukwa.....Pakawa

Palitokea mtu na mkewe ambao walikuwa wakiishi maisha duni, yule mke alimwambia mumewe waanzishe biashara ili maisha yao yawe mazuri, lakini mumewe kwa kutaka utajiri wa haraka haraka alikataa wazo hilo na kuamua kujiingiza katika wizi.

Siku moja alikwenda kuiba katika nyumba ya tajiri mmoja, tajiri huyo alimfuata mwizi wake na alipomuona, alimkata kiganja chake cha mkono wa kulia na kumsababishia mkono wake huo usifanye kazi na kuwa na ulemavu hadi leo.

42. Jogoo na Mkewe

Paukwa ..... Paukwa

Hapo zamani za kale, alikuwepo jogoo na mkewe. Siku moja jogoo alimwambia mkewe, “Mke wangu, akajibu;” “mume wangu, hata mimi napenda sana tuzaye ila ninahofia watoto wetu wataliwa na mwewe” Jogoo akamwambia mkewe:” hilo usihofu mimi nitajitolea kuwalinda watoto wetu zidi ya mwewe”. Wakakubaliana wazae. Siku ya kutaga ilipofika mke wa jogoo akaanza kutetea kwa kusema “Ntaka

ntakazaa,ntakazaaa” Jogoo akamsindikiza kwenda kutaga. Tembe akataga, akalia na hatimae akaangua.ilipofika siku ya kutoa watoto wao nje, wakawatoa

Ghafla akatokeya mwewe, Jogoo akakimbia mbio nyingi sana na akajifisha kachakani. Koo naye akawaita watoto wake haraka ili awafiche katika mabawa yake ila Mwewe akawahi kuchukua mtoto mmoja. Alipoondoka mwewe, Jogoo alirudi kwa mkewe na mke akamuuliza mumewe sababu ya kujificha, Jogoo akajibu kuwa ilikuwa ni kitendo cha ghafla kilichotokea hivyo alichanganyikiwa. Watoto wakaendelea kuchukuliwa na mwewe mpaka wakabakia watatu ndipo Koo naye akazidi kukasirika na kuanza kumshambulia mumewe kwa maneno na kumwambia “huna uume taa, huna uume taa, waacha watoto waliwa” Jogoo naye akajibu” sinchezele, sinchezele, angenikamata miye”. Hadi leo hii akitokea mwewe Jogoo na Koo hugombana katika kulinda watoto wao.

43. Bwana aliyepewa mkoba wa sokoni

Paukwa .....Pakawa.

Alikuwepo bibi na bwana, wakaishi kwa muda mrefu katika hali ya unyonge na umasikini. Bibi aliweza kustahmili muda mrefu, siku moja mumewe akenda sokoni kwenda kununua chakula, bahati nzuri alikuta muhogo, akanunua na kumpelekea mkewe, mke alipoumenya, akauonja na kuuona mchungu kama shubiri, akampikia mumewe hivyo hivyo, siku ya pili akanunua tena muhogo mchungu na siku ya tatu akanunua ule ule, bibi sasa akahamaki na kuamua kushona mkoba mzuri kwa ajili ya mumewe, mkoba ule akauandika MAPUA NIACHA HUNA UCHUMI, kwa kweli mkoba ulikuwa mzuri sana wakuvutia bibi yule akampa mumewe kwa ajili ya kununulia chakula sokoni, bwana akafurahia lakini hakujua kimeandikwa nini katika mkoba, kwani hajui kusoma wala kuandika.

Siku ya pili akachukua mkoba wake kwenda sokoni huku akijinabi kwa wenziwe kupata mke bora, alipofika sokoni kila anayemona anacheka kwa ule mkoba wake,



wakaendelea kumcheka mpaka soko zima linamcheka, akaamua kuwauliza, “hivi nyinyi mnacheka nini?” walizidi kumcheka, mmoja wao akamwambia unaambiwa umepata jiko bora mbona mkoba wako kaandika mapua niacha huna uchumi? Hakuamini na kuelekea kwa rafiki yake akamwambia hivyo hivyo akaanza na alipofika kwake akamuacha mkewe kumpa talaka moja tu.

Hadithi imeishia hapo

#### 44. Bibi Mjamzito

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikwepo bibi mmoja ambaye alikuwa ni mjamzito, sasa siku moja akapika ugali, alipomaliza kuupika akautia katika chombo kwa ajili ya kula. Hafla akasikia hodi hakitikia ile hodi akauficha ule ugali, nyuma ya mgongo wake na baadae akaitikia ile hodi. Baada ya hapo wakaulizana hali na baadae yule mgeni akaaga akaondoka. Baada tu ya kuaga yule bibi akaivuta sahani ya ugali na kuanza kula, hafla yule mgeni akaingia ndani bila ya kupiga hodi na kumkuta yule bibi anakula na yule mgeni akakaa bila ya kukaribishwa akaanza kula, mara tu baada ya yule mgeni kuondoka yule bibi mjamzito akaanza kuli kwa yule mgeni alikula ugali wake. Na hadithi yangu ikaishia hapo.

#### 45. Mzee Mpacho na wajukuu zake

Paukwa .....Pakawa.

Siku moja mzee Mpacho alisikia kelele za watoto. Aliacha kuchanja kuni, alitupa shoka na kukamata panga,mbio alikimbilia kule sauti inakotoka. Alikutana na watoto watatu wakikimbia mbio, huku wakipiga mayowe, aliwasimamisha huku akiwauliza kinachowakimbiza, wakasema “nyoka”. Mzee mpacho aliwacheka sana mpaka akakaribia kuanguka.

Ghafla mtoto mmoja alipiga tena kelele na kuruka huku akisema “huyu hapa amekwisha fika”, akiruka na kupiga kelele. Aliwataka na wale watoto wengine wakimbiye, mzee Mpacho naye akaomba msaada, “Jamani tuokoeni tunakufa”, mzee Mpaco alikumbuka ujana wake kwa mbio alizokwenda na panga lake mkononi.

Mtoto mwengine aliwazuia wenzake wasikimbie. Aliwaonesha mjusi aliyekuwa akitikisa tikisa majani makavu ya pale karibu yao.

Sasa ilikuwa zamu yao kumcheka mzee Mpacho, walicheka mpaka wakaanguka chini, mzee Mpacho alielewa kuwa hapakuwa na kitu bali mzaha wa kitoto. Hivyo aliamaki sana na kurudi huku akiwakamatia bakora na kutishia kuwapiga.

#### 46. Kijana aliyejifanya msomi

Paukwa.....Pakawa.

Alikuwepo kijana mmoja katika kijiji kimoja kilichokuwa hakina wasomi sana, kijana huyo alikuwa akipita kwenye vikundi vya watu akiwa na mabuku yake kwapani. Wanavijiji walipomuona walisema kijana yule ni msomi sana kumbe kijana yule hajui kusoma na anajionesha tu mbele za watu.

Siku moja wanakijiji hao walipokea barua kutoka kwa mkuu wa wilaya lakini hawajui kusoma. Mmoja kati yao alisema kuwambia wenzake tumpelekeni yule kijana anaepita na mabuku kila siku kijana yule alipopelekewa barua ile aliikamata na kuifungua ndani lakini kwa vile hajui kusoma alijikuta anaadhirika mbele za watu hao tena akiwa analia.

Kwa hivyo wanakijiji wale walipomuona kijana yule anaanza kulia nao walianza kutazamana na kuanza kulizana huku wakifikiria kuwa barua ile ndani yake ina habari ya msiba, baada ya muda vilio viliengezeka mtaani na msomaji wao.

## 47. Babu na Jiwe

Paukwa.....Pakawa

Hapo zamani za kale alikuwepo mzee na wajukuu zake, sasa siku moja mzee alikaa na wajukuu zake akawa anawatolea hadithi mbalimbali, kikafika kipindi cha swala akaenda kutia udhu. Wakati anatawadha miguuni alikunja nguo zake akawa yuko uchi sasa wale wajukuu wakamuuliza “babu nini hicho?” Akwaambia jiwe.

Na hadithi ikaisha hapo.

## 48. Kijana aliyeomba penzi kwa ndugu yake bila kujua

Paukwa.....Pakawa.

Katika miaka ya hivi karibu, palikuwepo na vijana waliokuwa wakiishi maeneo ya kwa alimsha. Wanapenda kukaa barazani na kunyawa juisi na vileja huku wakizungumza. Siku moja wakiwa barazani kati ya wale vijana, walikuwa na tabia ya kutoipisha kanga (wanawake). Katika kibara chao ipite peke yake.

Siku moja alipita mwanamke akiwa kachoka na kutembea kwa maringo, kijana mmoja wa kijiweni(kibaraza)alimananisha na mwanamke wake. Yule kijana akamfuata kwa pozi akimkamata mabega na kusema halo mpenzi kadogodogo. Yule dada aliitikia bila kuangalia, jamaa akamuuliza mbona hujasalimia pale kijiweni? Aah! Nimechoka. Jamaa akajipa moyo na kusema usijali nikubeba, kadogodogo wangu! Au? Yule dada akasema we acha tu.

Ilikuwa muda wa saa tatu usiku, mwangaza ulikuwa hautoshi. Kwa bahati ikapita gari kutoka jangombe ikienda mjini. Mwangaza wa taa za gari ulitoa aibu. Yule jamaa wa kiume alimuona vizuri yule mwanamke kumbe ni dada yake wa mama mmoja na baba mmoja, du!!! Mwanamke akaanza kujibu kaka yake, na kumwambia we pumbavu, we kumbe muhuni sana, wewe nilikuwa nasikia tu ukishakaa

kibarazani kazi yake kufuata wash-kaji tu,kila kikanga wakifuta wewe, utakoma naenda kusemae nyumbani.

Hadithi yangu imeishia hapo.

#### 49. Mfalme na Maradhi

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo Mfalme na kijiji chake, sasa pakawa na tatizo kubwa la kipindupindu. Mfalme akatoa amri kuwa nzi atakapotua popote auliwe. Siku mmoja Mfalme akaitisha mkutano wake huku alikuwa amenyoa para safi, wakati wa mkutano ulipofika nzi akatua juu ya kichwa cha Mfalme. Mtu mmojoa akampiga rungu la kichwa Mfalme na akafa, hapo hapompigaji akachukuliwa lakini hapakuwa na hukumu yoyote kwa kuwa Mfalme alitoa amri kuwa nzi atakapokutiwa popote auliwe.

Na hadithi ikamalizika hapo.

#### 50. Sungura na Fisi

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale walikuwepo wanyama wakubwa na wadogo lakini wale wanyama wakubwa walikuwa wanawaonea sana wanyama wadogo na kuwashambulia. Siku moja wanyama wadogo wakaamua kuweka kikao na Swala akawa kiongozi wa mkutano huo na kusema kua uonevu umezidi. Juma lilipopita watoto wawili wa Kongoni waliliwa na Fisi na hakushiba na juzi mwanangu ameliwa tena Fisi jee tutafanyaje? Ndipo wote wanakubaliana Fisi ni lazima auwawe haraka, wengine wakasema wampofue macho lakini tatizo ni jinsi ya kuwauwa. Nahatimae Sungura alitikisa kichwa na kusema kuwauwa niachieni mimi na nipeni siku saba tu.

Usiku ulipofika, alikoka moto nje ya nyumba yake na moto ulivyokolea alichukua jiwe kwenye moto nakuzidi kuongeza kuni na baadae alikwenda nyumbani kwa Fisi kumwita. Bwana Fisi alifurahi sana na kupata chakula usiku ule lakini Sungura alimlainisha kwa maneno matamu kwa kumwambia nimekuja kuchukua kwani kuna nyama nyingi nyumbani kwangu twende ukale, kwa vile Fisi ana tamaa akamfuata na walipofika akamwambia hizi ni nyama za Tambiko kwa hiyo zina masharti, ni lazima mnofu wa kwanza nikulishe mimi na ni lazima ulale chali na mdomo uwepo wazi huku sungura akicheka kimoyo moyo, ilikuwa tayari Fisi alishatekeleza masharti ndipo Sungura akachukua kibanio na kuchukua jiwe na kulitia kwenye mdomo wa Fisi, hapo hapo Fisi aligagaa na kufa na wanyama wadogo wakaishi raha mustarehe.

#### 51. Mama na mtoto wake wa kambu

Paukwa .....Pakawa.

Hapo zamani za kale palikuwepo na familia moja ambayo ilikuwa na watu watatu ,mama, baba na mtoto wao mmoja aitwaye Miza. Kadiri siku zilivyokuwa zikiendelea usoni, mama wa familia hiyo alipata maradhi hadi kufariki dunia. Baada ya kufariki dunia, baba wa familia hiyo akaowa mke mwengine na kupata mtoto mmoja wa kike aitwaye Mboja.

Siku moja baba yao akasafiri, aliposafiri, Miza akawa anakaa na mama wa kambu. Mama huyo akawa anamtesa sana hatimaye wakenda kutafuta kuni, mama akamchimbua Mize shimo na kumfukia mzima mzima.

Aliporudi baba yao, Mboja akamwambia baba yake na wakenda porini, akaimba nyimbo.

Miza ee Miza,

Baba yetu kesho rudi Miza ee Miza,

Katuletea zawadi Miza ee Miza,

Moja yako moja yangu ee Miza,

Mboja ee Mboja

Mama yako ni mbaya ee Mboja

Kanichimbia handaki ee Mboja,  
Njoo hapa unione ee Mboja,

Baba yake Miza na Mboja akaisikia ile sauti hatimaye Miza akaokolewa na baba yake kwenye shimo. Baba yao akahamaki na akataka kumuuwa mkewe lakini Miza na mboja wakamwambia baba yao amsamehe mama yao. Halafu wakaishi raha mustarehe.

52. Mtoto aliyeomba radhi kwa wazee wake

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo mtu mmoja na mwanawe, sasa wakakaa siku moja, yule mama akamwambia mwanawe “njoo nikutume”. Yule mtoto akawa anamjibu mama yake huku akipiga miguu chini kuwa kila siku unanituma miye tu, kwa hivyo miye sendi. Yule mama akamwambia mwanawe kwa kumfuza “ewe mwanangu leo uko hapa kesho uko kwengine aibu itakayokufika itakupta wewe na mimi mamayo.” Yule mtoto akafikiri pale pale akaona kuwa kweli amekosea na aliyoambiwa na mama yake ni ushauri mzuri kuhusu maisha yake na mama yake “Ewe mwanangu leo uko hapa kesho uko kwengine aibu inaweza kukufika”

“Mama Sitorejea tena baada ya hapo niliposema, nitatunza heshima na nasaha zako”. Mtoto akamuomba radhi mama yake na kamwambia hatafanya tena kosa kama lile. Mtoto huyu baadaye akaishi na mama yake katika maisha ya raha mustarehe.

53. Makame wa Makame atafuta mtoto

Paukwa ..... Pakukwa

Hapo zamani za kale alitokea Makame wa Makame na mkewe ambao waliishi vizuri katika maisha yao, lakini walikaa muda mrefu bila ya kupata mtoto, hivyo waliamua

kwenda kwa mpanga ili kutatuliwa tatizo lao, mganga bila ya kusita aliwapatia tiba ambayo aliwataka waende msitu na nyika kutafuta ua jekundu na wakisha pata walifunike chungu.

Makame wa Makame na mkewe walibahatika kupata hilo ua na walitekeleza masharti yote na hatimaye walibahatika kupata mtoto. Siku zilipita na mtoto alikuwa mkubwa na kwa bahati alikuwa mkaidi, vile vile mganga aliwaambia, wasije wakamwambia asili yake yule mtoto, basi ilitokea siku moja ambayo vituko vilizidi, sasa kutokana na vituko vya yule mtoto mama yake alisahau lile sharti katika kumgomba mtoto wake na alimwambia “mtizame yule mtoto wa maua tu” basi mtoto aliamaki na kuanza kurudi kwao ambapo ni mtini kwa hivyo lile sharti lilitenguka na mtoto alikwendazake huku akilia njiani na kuimba nyimbo isemayo”.

“mama kanambia mtoto wa maua, kwaheri mwana maua,

“Kwaheri mwana mauwa, kwaheri mama mtoto wa mauwa

Aliimba mpaka akafika msituni na kugeuka ua na likakaa mtini hatimaye Makame wa Makame wakaishi raha mustarehe kwani vitendo vya yule mtoto vilikuwa vikubwa na walijuta kutafuta mtoto.

#### 54. Makumbi yageuka fedha

Paukwa .....pakawa.

Hapo zamani alitokea mtu na mumewe ambao walibahatika kupata mtoto mmoja wa kike, mume akafariki, mtoto yule aliendelea kuishi na mama yake hadi alipofikia kuolewa, aliolewa na mume mwenye maisha mazuri, na waliishi mjini katika ndoa yao walipendana sana.

Huko kijijini mama wa mwanamke alikuwa akiishi maisha ya kawaida na alikuwa akipenda kuwapelekea watoto wake zawadi mjini na kuwajuliya hali zao.

Siku moja alipanga kuwaona wajukuu zake na ndipo alipokwenda porini kutafuta makumbi ya zawadi kwa watoto wake, aliyafunga vizuri na kwenda nayo mjini. Anapofika hakumueleza mwanawe juu ya mzigo huo, mtoto yule aliyachukua kuyahifadhi bila ya mumewe kujua.

Siku moja aliamua kwenda kuipunguza mizigo ile aliyokuwa aliletewa na mama yake mara alipatwa na mshangao alipofunua vifurushi vile na kukuta pesa kwa wingi, alimuita mumewe wazichukuwe na pia wampe habari mama yao, mama yao na yeye alishangaa sana na aliwaeleza hali halisi iliyokuwanayo hapo kabla, ndipo watoto wale walizidi kuwa matajiri pamoja na mama yao, waliishi raha mustarehe.

Na hadithi yangu imemalizia hapo.

#### 55. Sungura, Tembo na Kobe

Paukwa ..... pakawa

Walikuwepo Sungura, Tembo na Kobe, siku moja walipanga washindane mashindano ya mbio za miguu. Siku ilipofika harakati zilianza na walijipanga kwa ajili ya mashindano.

Walianza kwenda mbio kila mmoja kwa kiasi chake, Kobe alikwisha wapa habari jamaa zake kuwa kuna mashindano. Alitaka kila jamaa yake mmoja akaye kwenye kichaka na atakapomuona sungura natembo, basi mmoja ajitowe kweye kichaka na kujifanya anakwenda mbio. Makobe wote walitangulia na kujificha vichakani katika kila kituo.

Safari ilipoanza tembo na sungura walijiona wako mbele. Walipokaribia kufika kwenye kichaka, walimuona kobe ameshafika. Sungura na tembo waliengeza mbio kuharakia ushindi. Sungura alikazana akijiona yuko mbele peke yake ili apate ushindi, tembo kuona hivyo akakata tamaa na kulegeza mwendo. Sungura alipofika uwanjani Kobe alichomoza na kujinyakulia ushindi bila ya hofu. Sungura alibakia



kuduwaa, tembo akabakia kuchanganyikiwa, wote walimuona kobe ni adui yao na wakalazimika kumuheshimu. Wote waliheshimiana.

#### 56. Simba Mzee na Sungura

Paukwa .....Pakawa

Hapo zamani za kale alikuwepo Simba mzee na sungura na wanyama wengine. Simba mzee alikuwa hawezi tena kuwinda kwa hivyo wanyama wote waliamua kumpelekea chakula. Sasa ikawa kila mnyama anayempelekea chakula haonekani tena kurudi. Wanyama wakafanya wasiwasi na ikafika siku wakaitisha mkutano. Sungura akasema kuwa ni simba mzee ndiye anayewala wanyama wanaopeleka chakula. Siku moja sungura akatengeneza sanamu na ikawa ni zamu yake ya kupeleka chakula kwa simba mzee. Alipofika akalipeleka sanamu simba akalirukia lile sanamu na wanyama wote wasikia zile kelele za simba na sanamu. Sungura akakimbia, tokea siku hiyo simba mzee akaachwa na nja mpaka kufa kwake. Baada ya hapo wanyama wote wakaishi raha mustarehe.

#### 57. Mwanamke aliyeolewa na Zimwi

Paukwa.....Pakawa.

Alikuwepo bibi, bwana na mtoto, mtoto huyo alikuwa ni wa kike, baada ya siku nyingi kupita mtoto alifikia umri wa kuolewa na kila aliekuwa akija kumchumbia alikuwa hamtaki. Katika kuchagua sana siku moja alimpata mwanamme mzuri, lakini hakuwa binaadamu.

Yule mwanamke alikubali kuolewa na yule mwanaume. Baada ya siku nyingi kupita mambo yalibadilika, watu walimwambia kuwa mumewo ni zimwi lakini hakuwa mwenye kusikia. Siku moja usiku amelala akasikia sauti ikisema “njoo tule nyama, njoo tule nyama”. Yule bwana alikuwa anawaita wenzake na wakati ule alijua kuwa mkewe amelala.

Yule mtoto akashtuka na kutoroka, alipofika kwao akawaeleza wazee wake na baadaye alipata mchumba mwengine akaolewa na wakaishi raha bustaarehe.

#### 58. Simba na Sungura

Paukwa .....Pakawa

Hapo zamani za kale alikuwepo simba na sungura katika msitu mmoja. Siku zikapita simba alikuwa akiwala mmoja baada ya mmoja hadi wakaanza kupungua msituni wakiwa na majonzi makubwa. Kukicha hali inazidi kuwa mbaya,hapo ndipo sungura aliamua kuwita wenzake na kupanga mipango ya kumtekeleza simba, ghafla mipango ilikuwa tayari ya kuuliwa simba. Baada ya muda mchache sungura alitoka na akajitia woga kwenda kwa simba lakini hakujali. Baada ya kufika alimkuta amelala usingizi na kuanza kumwita. Simba aliamka na kumuuliza kuna nini? Sungura akasema kuwa yuko mnyama na anasema kuwa hakuogopi.

Anasemaje? hakuogopi. Yuko wapi?, kisimani. Sungura wakaongozana na simba hadi kisimani. Simba akaanza kuchungulia kisimani na kumwita “wewe mbabe”, akiunguruma na kutoa meno na yule aliyemo kisimani anamuonyesha yake. Simba kuona hivyo akaingiwa na hasira na kujitupa kisimani na kupiga kelele “nakufa miye”. Simba akafa na wanyama wengine wakaishi katika raha mustarehe.

.

#### 59. Wazee Wakulima

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale walikuwepo wazee wawili waliokaa pamoja wakifanya kazi ya ukulima Walikubaliana kulima mahindi kwa pamoja ili waweze kupata chakula chao Wazee hawa walijulikana kwa majina ya mzee Toboa na mzee Janjaruka, wazee

hawa mmoja alikuwa ni mfugaji wa ngombe na mmoja mkulima. Mazao yao yalistawi sana. Mzee Janjaruka alikuwa anapeleka mifugo yake usiku katika shamba la mzee Toboa ili ngombe wake watowe maziwa mengi. Mzee Toboa alipeleleza na akagundua kuwa ni ngombe wa mzee Janjaruka, aliwakamata, wakagombana na kupigana vibaya. Baada ya hapo ikwa kila mtu hazungumzi na mwenzake. Basi baada ya siku kupita akatokea kijana mmoja anayeitwa Mwanaimani akawaekea kikao na kuwapatanisha. Pia aliwapa faida na hasara za watu ambao watakuwa hawasemi, hapa katika dunia na kesho mbele ya MwenyeziMungu.

Baada ya hapo wazee hao wote walisameheya na kuishi kwa kuaminiana kama ilivyokuwa zamani na wakamshukuru sana yule kijana aliyewapatanisha.

#### 60. Nguruwe na Komba

Paukwa .....pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo nguruwe na komba. Nguruwe alikuwa na uso wake mzuri uliokuwa ukivutia wanyama wote wa porini. Siku moja nguruwe alimuona komba akirukia miti porini, akamuuliza, “komba unawezaje kupanda miti kama hiyo na ukaweza kuruka kutoka mti hadi mti?” Komba akajibu kuwa haya ni maumbile yangu, ndivyo Mungu alivyonijalia na kuniumba. Nguruwe aliona wivu, na akamwambia na yeye afundishwe kupanda miti na kuirukia. Basi komba alianza kumfundisha nguruwe namna ya kupanda miti, akaanza na miti midogo midogo. Baada ya siku tatu, nguruwe akamwambia komba anataka arukiye miti mikubwa, komba akamwambia bado panda hiyo hiyo midogo kwanza. Baadaye nguruwe akamuona komba anarukia miti mikubwa sana na yeye hakuweza kustahamili na akaanza kupanda mti mkubwa mmoja uliomrefu, lakini alipojaribu kurukia mti wa pili alianguka kifudifudi mpaka chini. Pua ikapondeka pondeka na mifupa ya uso wake ikavunjika ikafanyika mfano wa bonde ambalo kila nguruwe analo mpaka leo.

## 61. Simba na Mkewe na Sungura na Mkewe

Paukwa.....Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo sungura na mkewe na simba na mkwe, wote walikuwa wakiishi mwituni. Sungura alitafuta sehemu akafyeka majani ili apate kiwanja cha kujenga nyumba .Simba alipokuja akakiona, akasema kuwa hiki ni kiwanja kizuri cha kujenga nyumba na akaanza kujenga kwa miti. Alipokuja sungura alifurahi na kusema kuwa hiki kiwanja cha maajabu kimeanza kujijenga wenyewe na yeye akanza kikikandika.

Siku ya pili alipokwenda, simba alishangaa na kusema kuwa hii ni nyumba ya maajabu imejikandika wenyewe na yeye alianza kuezeka. Siku iliyofuatia, sungura na mkewe waliikuta nyumba tayari na wakaanza kuihamia. Punde simba na mkewe wakafika na wakaelezana na sungura na mkewe mkasa wote nzima. Mwisho wote wakaamua kukaa pamoja. Baada ya siku chache Bwana sungura na mkewe wakaaza kuogopa kwa kusifika kwa simba kwa ukali mwituni. Sungura na mkewe wakapanga kumfukuza simba kwa ujanja. Bibi sungura akamwambia mumewe “leo mume wangu natamani maini ya kifaru” bwana akaitika hewalla bibi, na wale simba wanasikia. Sungura akenda porini akamkuta faru ameshakufa akatoa maini na akampelekea mkewe. Siku ya pili mke wa sungura akadai maini ya nyati, hali ikaendelea kama ile siku ya mwanzo, kuona vile simba na mkewe wakaogopa na wakaamua kuhama kwa kuhofia wasije kutolewa maini. Basi bibi sungura na bwana sungura wakaishi kwa raha mustarehe.

**Wasimuliaji wa hadithi**

- 1.Fatma Saleh Moh'd
- 2.Juairia Ali Abdalla
- 3.Umukuruthum Abeid Ali
- 4.Maimuna Salim Seif
- 5.Dilale Hassan Othman
- 6.Hashima Moh'd Omar
- 7.Sharia Hamad Bakar
- 8.Abdalla Idi Abdalla
- 9.Semeni Hamad Ali
10. Mariam Khamis
11. Asya Moh'd Pandu
- 12.Mwanapili P. Vuai
13. Abdillah Saleh Juma
- 14.Yakoub Said Ali
- 15.Aziza Said Khamis.
- 16.Abdillah S Juma
- 17.Sada Bakar Rajab
- 18.Tatu Issa Salim
- 19.Hadija Mumwa Vuaa
20. Iaila Aburahaman Abubakar
- 21.Haji Said Haji
- 22.Rahma Ramadhan Abdu
- 23.Asha Kombo Khamis

- 24.Khamis A. Faki
- 25.Hajra Mussa Ramadhan
- 26.Yusuf Haji Yussuf
- 27.Nyange Sheha Ngwali
- 28.Mariam S Kassim
- 29.Mwanaidi R. Abdalla
- 30.Zulfa S Maalim
- 31.Abass A Ali
- 32.Abubakar Suleiman
- 33.Asha Makame Salim
- 34.Bibie S Said
- 35.Zainab Sururu Vuai
- 36.Fat-hiya M Mussa
37. Said O Hussein
- 38.Mkasi Mgwali Hamad
- 39.Asma M Hassan
- 40.Rahma Shauri Hassan
41. Nassor S Ali
42. Ussi Khamis Khamis
- 43.Suleiman Rashid Mwita
- 44.Idris M Moh'd
- 45.Moh'd H Hamad
- 46.Zaituni N Ahmada
- 47.Juma M Kessi

- 48.Tatu J Ali
- 49.Hanaf M Kauli
- 50.Islam Said Mselem
- 51.Raya M Abdalla
- 52.Fatma M Hamad
- 53.Izat Abass
- 54.Rukiya Abdalla
- 55.Saumu Abeid
- 56.Halima Hemed
- 57.Ibrahim A Moh'd
- 58.Said B Kondo
- 59.Ubwa Hamid
- 60.Safia Pandu Sijawa.
- 61.Nassra H Nassor